# MAZUNGUMZO NA “KINGUNGE” WA ITIKADI YA UJAMAA

*Kingunge Ngombale Mwiru*
*1930-2018*

# MAZUNGUMZO NA “KINGUNGE” WA ITIKADI YA UJAMAA

*Kingunge Ngombale Mwiru*
*1930-2018*

**Kutoka Kavazini Na. 3**

**2019**



Mzee Kingunge akichangia mada katika Mhadhara wa pili wa Mwalimu Nyerere, ulioandaliwa na Kavazi la Mwalimu Nyerere 26.11.2015 katika ukumbi wa Tume ya Taifa ya Sayansi,kijitonyama

Kimechapishwa na Kavazi la Mwalimu Nyerere
Toleo la kwanza 2019
Chapisho la kwanza

© Kavazi la Mwalimu Nyerere

**ISBN: 978-9976-5483-0-3**

Kitabu hiki kimechapishwa kwa hisani ya Rosa Luxembourg Stiftung (RLS) inayofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Kijerumani.

Kimechapwa na Inter Press of Tanzania Ltd. Dar es Salaam

# DIBAJI

Kitabu hiki kimebeba mazungumzo niliyofanya na marehemu Mzee Ngombale kwa nyakati na madhumuni tofauti. Tarehe 27 Agosti 2009 nilizungumza naye kwa lengo la kuyachapisha mazungumzo hayo katika Jarida la *Chemchemi*, ambalo lilikuwa linachapishwa na Kigoda cha Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mazungumzo ya pili nilifanya naye kwa tarehe tofauti miaka mitatu baadae (19/06/2012, 7/08/2012, 10/08/2012 na 16/08/2012) kwa ajili ya kitabu cha wasifu wa Mwalimu Nyerere ambacho tunaandika wanazuoni watatu (Issa Shivji, Saida Yahya-Othman na Ng'wanza Kamata). Mazungumzo haya yamehaririwa na Saida Yahya-Othman na yanachapishwa kwa mara ya kwanza katika kitabu hiki.

Mzee Kingunge Ngombale-Mwiru ni kiongozi anayejulikana sana na Watanzania. Yeye ana nafasi ya kipekee katika historia ya kisiasa nchini kwa sababu ametumika, katika nyadhifa mbalimbali za Chama-tawala na Serikali, awamu zote nne za utawala. Umahiri wake unajulikana hasa katika medani ya itikadi na falsafa ya U-Marx juu ya usoshalisti wa kisayansi. Mzee Ngombale alikuwa mstari wa mbele katika kuandika rasimu za nyaraka muhimu sana na za kihistoria za Chama pamoja na Mwongozo wa TANU wa mwaka 1971 na Mwongozo wa CCM wa mwaka 1981. Chanzo na sababu za Chama kuandaa Miongozo hii miwili imeelezwa kwa ufasaha na Mzee Ngombale na kwa maoni yetu ni kumbukumbu muhimu ya kihistoria ambayo haina budi kuwekwa kwenye rekodi ya kudumu kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Pamoja na umahiri wake wa kuchambua kwa undani masuala ya kiitikadi, Mzee Ngombale pia alikuwa anajulikana kwa msimamo wake thabiti. Ndiyo maana wengi wetu tulishtuka kidogo alipochukua msimamo wa kuunga mkono mgombea wa upinzani katika uchaguzi wa 2015. Kama kawaida yake alielezea hadharani

sababu zake za kufanya hivyo, sababu mojawapo ni kwamba Chama chake kilikiuka taratibu za Chama chenyewe za kupendekeza mgombea wa urais. Inawezekana wengi wa mashabiki wake wasikubaliane na mantiki ya sababu alizotoa lakini pamoja na kutokubaliana naye, kwa maoni yangu, wachache sana wanaweza kuzipuuza sababu alizotoa.

Hoja za Mzee Ngombale wakati wote zinafikirisha na hii pia ilikuwa hoja ya kutufikirisha. Kama Mwalimu Nyerere, Mzee Ngombale alikuwa na kipaji na tabia ya kueleza kwa hoja misimamo yake. Katika siasa yenye mtazamo wa kimaendeleo, jambo hili ni muhimu sana na sisi sote (pamoja na wanasiasa) hatuna budi tujifunze kutoka kwa Mwalimu Nyerere na Mzee Ngombale namna ya kujadili mambo muhimu yahusuyo hatma ya nchi yetu kwa nguvu za hoja na sio hoja za nguvu. Vitisho, amri au maonyesho ya mabavu kamwe hayawezi kutusaidia kujenga muafaka wa kitaifa ambao ni muhimu kabisa kuikuza amani na utulivu na kutuletea maendeleo ya wengi na sio utajirishaji wa wachache.

**Issa Shivji**
Mkurugenzi
Kavazi la Mwalimu Nyerere
Januari 2019



*Katika maongezi haya na Mhariri Mkuu wa Jarida, Profesa Issa Shivji, Mzee Ngombale anazungumzia maisha yake ya kisiasa na mambo mengine mengi. Mazungumzo haya yalifanyika nyumbani kwa Mzee Ngombale kwa takriban saa tatu tarehe 27 Agosti 2009 na kuchapishwa katika Jarida la Chemchemi, ambalo lilikuwa linachapishwa na Kigoda cha Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

## 27 Agosti 2009

**IS:** Unajua tuna jarida la 'Nyerere Chair'.[1]

**KNM:** Aah!

**IS:** Ni jarida la Kiingereza.

**KNM:** Aah!

**IS:** Na tulilizindua mwezi wa nne. Hivi wewe ulikuwepo?

**KNM:** Kwenye uzinduzi? Hapana, sikuwepo.

**IS:** Aah! Ulikuja kesho yake.

**KNM:** Enh!

**IS:** Sasa jarida lile lilikuwa la lugha ya Kiingereza, kwa hiyo mpango wetu ni kuwa na matoleo mawili kwa mwaka, moja litatoka kila mwezi wa nne na la pili kila mwezi wa kumi. Toleo la mwezi wa nne litakuwa la lugha ya Kiingereza na lile la mwezi wa kumi litakuwa kwa lugha ya Kiswahili. Na hivi tupo katika maandalizi ya toleo la Kiswahili linalotarajiwa kuzinduliwa tarehe 13 mwezi Oktoba.

**KNM:** Ooh!

---

[1] Kigoda cha Taaluma cha Mwalimu Nyerere.

**IS:** Sasa kipengele mojawapo katika jarida kinaitwa 'Maongezi'. Sio mahojiano, ila ni maongezi tu. Tunazungumzia mambo mbalimbali katika hali isiyokuwa rasmi, na Bodi ya Wahariri iliamua kwamba tuzungumze na wewe kutokana na uzoefu wako wa uongozi kwa muda mrefu, awamu zote nne.

**KNM:** Na hata kabla ya hizo awamu.

**IS:** Kama nilivyozungumza awali, yatakuwa ni maongezi tu. Labda kwanza kabisa kwa muhtasari tu, tupatie historia yako.

**KNM:** Historia yangu kuanzia wapi? Mimi nimezaliwa Kilwa.

**IS:** Na Kilwa [katika Afrika Mashariki] ni kama Timbuktu ilivyo katika Afrika Magharibi.[2]

**KNM:** Nimezaliwa Kilwa ya bara, Kipatimu. Lakini wazee wangu walihama mapema kabla ya vita kuu vya pili. Mzee [baba yangu] alikuwa mwalimu. Lakini mwaka wa 1936 alikosana na mapadre. Unajua Kilwa Kipatimu ndio mahali pekee ambapo palikuwa na kanisa. Baba mkubwa, Mzee Ambrose ndiye alielipokea kanisa hilo. Baba na baba mkubwa walikuwa Waislamu, Lakini baba mkubwa aliwabadili dini ndugu zake wote na kuwa Wakristo.

**IS:** Kwa hiyo wewe ulipozaliwa walikuwa wamekwishabadili dini?

**KNM:** Walikuwa wamekwishabadili dini wakati wa Wajerumani. Baada ya kukosana na mapadre Baba aliondoka akaja Dar es salaam mwaka 1937, akaja kutuchukua kwa hiyo nimekua na kusoma kuanzia darasa la kwanza hadi la kumi Dar es salaam.

**IS:** Shule gani?

---

[2] Timbuktu iko katika nchi ya Mali. Kihistoria inajulikana sana kuwa ni mashuhuri kabla ya uvamizi wa Wazungu. Katika enzi zile Timbuktu ilikuwa kitovu cha ustaarabu na usomi wa Uislamu.

**KNM:** Nimesoma kuanzia darasa la kwanza mpaka la nne shule ya msingi Mchikichini iliyopo pale nyuma ya kiwanda cha bia [Breweries].

**IS:** Nimewahi kufika pale; si marehemu Ditopile nae kasoma pale?

**KNM:** Wale wadogo zangu wamesoma baadaye. Kuanzia darasa la tano hadi la kumi nilisoma pale Kichwele (Uhuru) enzi hizo miaka ya arobaini ilikuwa ikiitwa *African Central School* Hata Mzee Kawawa pia alisoma pale. Yeye alikuja pale darasa la tano mwaka 1942, wakati huo mimi nilikuwa naingia darasa la kwanza Mchikichini.

**IS:** *African Central School* ambayo iko pale Uhuru mchanganyiko?

**KNM:** Mbele ya kiwanda cha bia. Nilipoingia darasa la tano mwaka 1946, Kawawa alikuwa darasa la tisa na akawa *House Prefect* wangu. Tulianza kufahamiana tangu hapo.

**IS:** Na lugha ya kufundishia ilikuwa Kiswahili?

**KNM:** Hapana, kuanzia darasa la tano mpaka la sita ilikuwa Kiswahili na baada ya hapo ni Kiingereza. Baada ya kubahatika kupasi mtihani wa darasa la kumi, nikaenda Tabora. Kwa kipindi hicho, kufaulu katika shule ya Dar es salaam ilikuwa ni kazi ngumu kutokana na mazingira tata ya kusomea. Kwa mfano, kipindi chetu tulipasi watu wanne tu kati ya wanafunzi kumi na watatu.

**IS:** Na hao wanne unawakumbuka?

**KNM:** Bahati mbaya wenzangu wote wamefariki dunia sasa. Lakini nawakumbuka vizuri: Bori Lila….

**IS:** Bori Lila! Ndiyo.

**KNM:** Mume wake mama Hindu Lila. Ndugu Bori Lila tulianza nae tangu darasa la kwanza pale Mchikichini. Halafu kuna Juma Ali Lukali [Dar es salaam] na Dr. Maeda [Tanga], ambaye alienda

hadi Makerere. Mimi sikwenda Makerere kwa sababu nilikuwa napenda kwenda India kusomea sheria na uandishi wa habari.

**IS:** Baada ya kumaliza Tabora?

**KNM:** Ndiyo, baada ya Tabora. Niliamua hivyo, kwa hiyo niliandika '*direct employment'* kwa sababu siku zile tulikuwa tunapangiwa kabisa kazi ya kufanya. Nilimaliza Tabora mwezi wa kumi na mbili mwaka 1953, baadaye nikafanya *Cambridge School Certificate* kwa hiyo nikapangiwa kazi ya ukarani PWD[3] hapa Dar es salaam. Bahati nzuri tayari nilikuwa nina mwamko wa kisiasa tangu shuleni.

**IS:** Shule gani sasa, hapa au Tabora?

**KNM:** Kuanzia hapa Dar nilikuwa nimekwisha amka kisiasa; lakini Tabora mwamko uliongezeka. Unajua wakati ule kulikuwa na vita vya Mau Mau kule Kenya, sasa yale mapambano ya akina Jomo Kenyata yalituamsha sana.

**IS:** Na mlikuwa mnapata hizo habari?

**KNM:** Tulikuwa tunapata sana.

**IS:** Kupitia nini, redio au?

**KNM:** Wakati huo redio ya Dar es salaam ilianzishwa, lakini magazeti pia yalikuwepo, kama vile magazeti ya Mamboleo, Standard, Ngurumo na kadhalika. Kwa hiyo tulikuwa na mwamko sana. Pale Tabora katika somo la Uraia walimu wetu [Waingereza] walipata shida sana maana walikuwa wanajaribu kutupa kasumba za Waingereza kuhusiana na vita ya Mau Mau, lakini tulikuwa tunawakatalia. Kwa hiyo mimi nilikuwa tayari na mwamko kabisa. Nilipoanza kazi hapa [Dar es salaam] kulikuwa na chama cha watumishi wa serikali, Tanganyika African Government Servants Association, TAGSA. Wakati huo Rais wa chama hicho alikuwa ndugu Kawawa.

---

[3] *Public Works Department*.

**IS:** Ndiyo.

**KNM:** Lakini hakuwepo Dar es salaam, alikuwa amepelekwa Handeni. Kulikuwa na kambi ya Wakenya, hasa Wakamba, waliokuwa wameletwa Handeni kutokana na matokeo ya vita kwao. Na yeye kwa kuwa alikuwa Bwana Maendeleo ikabidi apelekwe kule. Bwana Ally Sykes aliyekuwa Katibu Mkuu wa TAGSA na wenzake waliniteua kuwa katika Kamati Tendaji Kuu ya TAGSA. Hivyo, mara tu baada ya kuanza kazi, nikaingia katika ngazi ya taifa ya TAGSA.

**IS:** Na wakati huo uliendelea kuwa mfanyakazi wa PWD?

**KNM:** Eeh, niliendelea kuwa karani. Mimi ndiye niliyekuwa kijana zaidi katika Kamati Tendaji Kuu ya TAGSA, kupigania haki za Waafrika. Kwa bahati nzuri, TANU ikaanzishwa tarehe 7 Julai 1954 na kaka Ali Sykes alikuwa kati ya wale kumi na saba walioanzisha TANU. Baada ya matangazo kuhusiana na kuanzishwa kwa TANU, tukamwomba kaka Ali aje atueleze. Baada ya wiki, kama Katibu Mkuu wa TAGSA, Kaka Ali alikuja kutueleza juu ya TANU. Alikuja na kadi za uanachama na mimi nikajiunga palepale.

**IS:** Na huo ulikuwa mwezi wa?

**KNM:** Mwezi huo huo wa Julai, kama wiki moja baada ya kuundwa TANU. Nikapewa kadi nyingine 100 za kwenda kutafuta wanachama, na eneo langu likawa ni kule PWD. Kwa hiyo hapo nikaingia moja kwa moja katika harakati za kisiasa. Lakini nikiwa kazini, nilikwenda kwenye usaili kwa ajili ya kwenda India kusoma sheria, nikafanikiwa nikapata udhamini, lakini wakati huo nikiwa nimeishakolea na harakati za siasa. Nikasema niende huko wakati vita imeshakolea hapa? Nikaacha.

**IS:** Hukwenda India?

**KNM:** Eeh, mwaka 1955 nilipata udhamini, lakini sikwenda nikaendelea na harakati za siasa. Ilikuwa ni kila nikitoka kazini

mida ya saa kumi na nusu nikaelekea makao makuu ya TANU pale *New Street*.

**IS:** Pale Lumumba?

**KNM:** Tulikuwa tunapaita *New Street*. Tulikuwa tukifika pale Mwalimu anatupa kazi sisi vijana tuliosoma. Kwa kipindi hicho darasa la kumi na mbili lilikuwa kubwa.

**IS:** Unaweza kukumbuka mara ya kwanza kukutana na Mwalimu ilikuwa lini?

**KNM:** Kwanza nilikutana nae katika mikutano ya chama iliyokuwa ikifanyika Arnatouglo kila Jumapili kwenye saa tano hivi. Mwanzoni, tulikuwa hatuendi vijana wengi ila sisi wachache tuliokuwa na mwamko ndio tuliotambulishwa kwa Mwalimu. Ali Sykes ndiye aliyetutambulisha kwa Mwalimu.

**KNM:** Ali Sykes ndiye aliyesimamia kuchapisha kadi na kila kitu. Kilichokuwa kinafanyika ni kwamba baada ya Mwalimu kumaliza kuhutubia ndio tunakwenda kumsalimia. Lakini mara nyingi makutano yetu yalikuwa jioni pale ofisini. Mara kwa mara alipokuwa na jambo ambalo linamtatiza alikuwa anatuita na kutuambia tulifanyie kazi. Halafu pale ofisini kulikuwa na magazeti kutoka Ghana.

**IS:** Aah!

**KNM:** Yalikuwa yanatoka katika chama cha Nkrumah kilichoitwa *The Convention People's Party*. George Padmore aliekuwa hodari sana kwa propaganda, ndiye aliyekuwa anatuletea TANU mara kwa mara magazeti kutoka Ghana. Wakati huo, Waghana walikuwa mbali sana katika harakati za kupigania uhuru, na tulikuwa tunasoma magazeti yale ili tujue wenzetu wanafanya nini.

**IS:** Mmh.

**KNM:** Hiyo ndio ilikuwa tabia yangu kama mpigania Uhuru wa nchi yetu. Baadae Mwalimu alitoa wito kwa vijana wasomi

kujitokeza kwenda kufanya kazi muda wote kwenye chama; nikaamua kuacha kazi yangu ya mwanzo. Haikuwa rahisi kwa sababu, kwanza, Mzee wangu hakupenda hata kidogo suala la mimi kuacha kazi kwa sababu mshahara wangu ulikuwa mzuri, na pia nilikuwa nasaidia familia pale Mzee alipokwama. Pili, kule kazini kulikuwa na tatizo, Wazungu walikuwa hawataki niache kazi.

**IS:** Mmh.

**KNM:** Kutatua tatizo la Mzee ilichukua miezi sita, kwa sababu nisingeweza kufanya maamuzi hayo bila ridhaa yake. Kwa msaada wa mama, hatimaye alikubaliana na wazo langu. Kwa hiyo, alinikabidhi kwa uongozi wa chama wa Bagamoyo ambako ndiko alikokuwa anaishi na anafundisha.

**IS:** Ilikuwa mwaka gani?

**KNM:** Mwishoni mwa mwaka 1956, nilikuwa nimekwishamueleza Mwalimu kwamba nashughulikia tatizo la nyumbani. Mwenyekiti wa TANU Bagamoyo akaamua kunipeleka Makao Makuu ya Chama Dar es salaam. Mapema mwaka 1957, Mwalimu akanipeleka Rufiji kuunda uongozi wa wilaya kama Katibu wa Chama wa Wilaya. Mwaka 1958 nikawa katika ujumbe wa msafara wa kwenda kwenye Mkutano Mkuu wa Tabora, mkutano wa kura tatu.

**IS:** Ndiyo!

**KNM:** Niliporudi kutoka Tabora, Kamati kuu ikawa imeamua kwamba niende kusoma nje. Mimi na wenzangu, (isler Mapunda na Shaaban Nyelwa Kisenge. Tukaondoka mwaka huo wa 1958 kwenda chuo cha Liberia –Cuttington College and Divinity School.

**IS:** Liberia?

**KNM:** Enh, tukaenda Liberia. Tulipofika Liberia tulikatishwa tamaa na mambo tuliyoyakuta. Sisi tuliondoka Tanganyika tukiwa na ari ya kupigania uhuru na uhuru kwetu ulikuwa ndio jibu la

matatizo yote. Tulipofika kule tulikuta nchi inaitwa huru, lakini mambo yaliyokuwa yakifanyika ndani yalikuwa hayaashirii uhuru.

**IS:** Enhe!

**KNM:** Tulikuta mgawanyiko kati ya wenyeji, *natives*, na *Americo-Liberian*, waliorudishwa kutoka Amerika. Mgawanyiko ulikuwa wa hali ya juu kiasi kwamba kulikuwa na sheria za wenyeji na waungwana, yaani *'civilised'*. Pia watu walikuwa wanafanyishwa kazi kinguvu, *forced labour*, kiasi kwamba kwa kipindi tulichofika tulisikia Liberia ilikuwa katika mgogoro na shirika la kazi duniani, *ILO*.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Cha kushangaza ni kwamba, hali hiyo ilikuwa imekubalika na makampuni ya Kimarekani hasa *Firestone Company*, ambalo lilikuwa na shamba kubwa kuliko yote duniani la mpira. Kampuni hii ilikuwa na wafanyakazi zaidi ya 35,000 ambao walikuwa wanapatikana kupitia mikataba iliyokuwa inafanywa kati ya serikali na kampuni hii. Licha ya makampuni, viongozi serikalini nao walikuwa wanamiliki mashamba ya mpira ambayo yalikuwa yanahitaji wafanyakazi. Kwa mfano, Rais alikuwa na wafanyakazi wapatao 3,000, huku Makamu wa Rais alikuwa na wafanyakazi zaidi ya 2,500. Taarifa hizi zote tulikuwa tukizipata kwa kificho kutoka kwa wanafunzi wenzetu.

**IS:** Na hao walikuwa wanafunzi wa Kiliberia?

**KNM:** Eeeh! Baadhi yao walikuwa hawakubaliani na mambo hayo, lakini wasingeweza kujitokeza waziwazi, kwa hiyo tukaanza kuchukua hatua. Mimi nilikuwa tayari na mawazo ya kisoshalisti tangu niko hapa nyumbani. Nilikuwa nimekwishaanza kusoma kitabu cha *The Communist Manifesto*, *Das Capital*, ingawaje ilikuwa ni vigumu kukielewa.

**IS:** Ulianza kusoma hapa hapa?

**KNM:** Ndiyo. *Das Capital* aliniletea rafiki yangu mmoja hivi mwaka 1956 aliporudi likizo kutoka India alikokuwa anasoma kilimo. Na tulipofika chuo kikuu cha Liberia tuliendelea kusoma zaidi vitabu vinavyohusu mawazo mbalimbali ya kisoshalisti. Tulipofika chuoni hapo, ilitubidi tufanye mtihani unaoitwa *Placement Test.* Mtihani huo haukuwa kwa ajili ya kupima uwezo wa kitaaluma tu, *academic level*, bali pia utamaduni na mwelekeo wa kiitikadi, *cultural and political level and orientation*. Baada ya kufanya mtihani huo, kikundi chetu [cha Watanzania] kilionekana tofauti na wanafunzi wengine.

**IS:** Ok!

**KNM:** Baada ya kugundua kuwa sisi tuna mtazamo wa kisoshalisti, walimu waliamua kutupa masomo mengine tofauti na wanafunzi wengine. Masomo hayo yalikuwa yanalenga kubadili mtazamo wetu. Mfano, walianzisha somo la falsafa ambalo halikuwepo katika mtaala wa chuo. Kwa hiyo sisi tulikuwa na ushawishi mkubwa sana pale chuoni kiasi kwamba tuliwafanya wanafunzi wa Liberia walianza kuuliza masuali ya msingi kuhusu mfumo uliokuwepo. Kwanza ni kuhusu ubaguzi kati ya *Americo-Liberians* na wenyeji; kisha suala la kufanyishwa kazi kinguvu na pia matatizo ya usawa.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Wanafunzi wenyeji walioonekana kuwa na akili nyingi walilazimishwa kubadili majina yao na kupewa majina ya Ki-*Anglo-Saxon*. Lakini baada ya kutuona tunatumia majina yetu ya Kiafrika kwa kujiamini, wale watoto wa wenyeji waliamua kurudia majina yao ya jadi [ya Kiafrika]. Haya mabadiliko yaliyojitokeza chuoni yalisababisha tuingie katika mgogoro na uongozi wa chuo. Kwa kipindi hicho mimi nilikuwa kiongozi wa wanafunzi kutoka Afrika Mashariki, [Tanganyika, Kenya, na Zanzibar]. Sasa tukawa na msuguano sana na mamlaka, wakatuona sisi watu hatari sana mpaka Rais Tubman akaja kwenye mahafali na kutoa onyo kali kwamba mhadhiri yeyote mwenye fikra kama zetu ataondolewa na vijana wenye fikra hizo

pia wakijulikana watafukuzwa chuoni. Kwa hiyo tuliokuwa tunazungumzwa ni sisi wanafunzi wa Kitanganyika; tukawa na mpango wa kukimbia.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Kwa bahati nzuri ulikuja ujumbe wa wanafunzi kutoka Dakar, kwenye Chama Cha Wanafunzi wa Federation of Black African Students in France. Hawa vijana walikuwa wakitembelea vyuo vikuu katika nchi za Afrika ya Magharibi zinazozungumza Kiingereza, na walipofika Liberia tukakutana. Baada ya kukutana nami walifurahi sana kwa sababu walisema katika mzunguko wao wote kwa mara ya kwanza walikutana na mtu alieyezungumza lugha moja, mtazamo mmoja wa Ki-*Marxist*. Ilikuwa imebaki miezi sita tu…..

**IS:** Kumaliza kozi yako?

**KNM:** Nikawaambia siwezi kuendelea kwa sababu Mkuu wa Chuo amepewa kazi moja tu ya kupambana na mimi. Wakaniambia likitokea lolote niende Dakar ili wanitafutie *scholarship*. Ikafika wakati ikabidi niondoke kwa sababu walikuwa wameshafanya mpango wa siri wa kunirudisha nyumbani.

**IS:** Ni mamlaka ya Liberia?

**KNM:** Eeh! Bahati nzuri kulikuwa na kijana wa Kiliberia aliyekuwa anafanya kazi katika ubalozi wa Uingereza, ambaye alinitumia taarifa kunieleza juu ya mpango huo. Nilimfuata Mkuu wa Chuo, nikamuuliza juu ya suala hilo, na nikamwambia kwamba siko tayari kurudi nyumbani kwa sababu si wao wala Waingereza walionileta Liberia ila ni Chama changu tu kitakachoamua mahala pa kunipeleka. Niliondoka kisiri, na serikali na uongozi wa Chuo ulikuja kujua baada ya mimi kufika Conakry, [Guinea].

**IS:** Sasa huku nyumbani, Chama kilikuwa na taarifa hizo?

**KNM:** Baadae nilipofika Dakar niliwatumia taarifa na Mwalimu alipopita Dakar nikaonana naye. Niliendelea na masomo yangu hapo Dakar ambayo yalikuwa yananipeleka mara kwa mara nchini Ufaransa nilikokuwa nafanyia utafiti wangu wa '*Opinion Polling'* katika *programme* ya saikolojia ya jamii, *social psychology*, katika Chuo Kikuu cha Sorbonne. Katika chuo hicho, niliunganishwa na profesa wa ki-*Polish* kutoka idara ya *French Institute of Public Opinion.* Nilikaa huko hadi mwishoni mwa mwaka 1966.

**IS:** Mwishoni mwa mwaka 1966? Kwa hiyo ulikaa Dakar kwa miaka sita?

**KNM:** Miaka mitano na kitu. Nilitoka kule kama mwanafunzi wa *Doctorat de Troisieme Cycle*, [Third Cycle Doctorate] Niliporudi [mwaka 1969] sikuwa na nia ya kukaa, nilirudi kwa mapumziko mafupi kuiona familia kwa sababu nilikuwa nimekaa nje kwa muda mrefu. Lakini nikakuta tatizo la chuo cha Kivukoni ambapo ilikuwa inadaiwa kuwa wahadhiri Wazungu walikuwa wanadai kwamba hapakuwepo na Mwafrika anayeweza kufundisha siasa. Kwa hiyo Chama kikaniomba nibaki nifundishe. Nilikubali kufundisha kwa muda [part-time] ili niendelee na utafiti wangu. Lakini haikuwezekana kufundisha kwa muda kwa sababu wanafunzi waliponikubali sana waliniomba nifundishe muda wote.

**IS:** Nani alikuwa *Principal* wakati ule?

**KNM:** Alikuwa Cunningham, yule Mkanada. Walimu wakati ule walikuwa Waingereza, Wairish, Mjerumani mmoja, Wamarekani na Mkanada Cunningham. Wamarekani na Waingereza walikuwa wengi na wao ndio waliokuwa wahadhiri wa muda wote [*full-time lecturers*]. Na hiyo ndiyo sababu mojawapo iliyosababisha wanafunzi waendelee kunihitaji. Pia Mwalimu aliagiza mimi nianzishe somo la Azimio la Arusha na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Kwa hiyo nikaingia moja kwa moja kwenye harakati.

**IS:** Kwa hiyo hukumaliza *Doctorate*?

**KNM:** Sikumaliza kabisa. Tena wakati ule Tanzania ilitakiwa kutoa Katibu Mkuu wa *Pan-African Youth Movement*. TANU Youth League ikasema hawana mtu mwingine isipokuwa mimi wa kushika nafasi hiyo. Ingawaje mimi sikupenda, lakini ndio ulikuwa uamuzi wa Kamati Kuu. Hivyo nikateuliwa kuwa Katibu Mkuu wa *Pan African Youth Movement* (PAYM). Baada ya kufanya kazi huko kwa muda mfupi, Kamati Kuu iliniita tena hapa nyumbani kutokana na matatizo ya Jeshi la Kujenga Taifa *[National Service]*. Tatizo la kwanza lilihusu hoja ya kuimarisha elimu ya siasa katika JKT ili kukidhi matarajio na viwango vya vijana wanaojiunga na JKT kwa mujibu wa sheria yaani ex-form six na ex-vyuo vikuu. La pili kusaidia makamanda kuweka nafasi ya nidhamu ya kujituma, badala ya kuweka mbele nidhamu inayotokana na hoja za kikamanda tu.

**IS:** Kule *Pan-African Youth Movement*?

**KNM:** Eeh! Niliendelea *Pan-African Youth Movement*. Lakini muda mrefu zaidi nilikuwa hapa nyumbani. Baadaye Mwalimu akaona niwe Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa TANU. Halafu ndio likaja tatizo la mwaka 1971.

**IS:** Nafikiri ulikuwa Katibu Mkuu tangu 1968?

**KNM:** Hapana, mwaka 1970. Kwa sababu kuanzia mwaka 1968 mpaka mwaka 1970 nilikuwa JKT. Kilichotokea mwaka 1971, kwanza ni lile tatizo la Iddi Amin. Baada ya kuangusha serikali ya Obote alituvamia mara kwa mara na kumuua *RPC* wetu Hans Poppe. Tatizo la pili ni lile la kusini, Frelimo walikuwa wanaendesha vita vya ukombozi wa Msumbiji na Wareno wakatangaza kuwa watatumia haki ya kufuatia.

**IS:** *Right of Pursuit!*

**KNM:** Kwamba kama Wamarekani walivyokuwa wakifanya Vietnam, kutoka Vietnam ya Kusini kwenda Vietnam ya Kaskazini, basi nao walipanga kufanya vivyo hivyo, kuingia

Tanzania wakitokea Msumbiji. Na kweli walikuwa wanaingia, wanapiga na kuua watu wetu. Ilibidi hatua za haraka zichukuliwe, na Mwalimu akataka kunituma Kagera kwa muda wa miezi sita kwenda kuhamasisha watu kama Katibu Mkuu wa Vijana na kuwaandaa pindi ikitokea Iddi Amin kutuvamia. Lakini mimi nilishauriana na Mzee Kawawa, aliyekuwa ameagizwa na Mwalimu, kwamba nilikuwa tayari kwenda Kagera lakini tatizo hilo lilikuwa kubwa na lisingeweza kutatuliwa kwa mimi kwenda Kagera. Kwa hiyo nikashauri kwanza kiitishwe kikao kikuu cha *NEC* ili kujadili hali ya ulinzi na usalama wa taifa katika mtazamo mpana wa kusini na kaskazini.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Kwamba tukilitazama hivyo ndipo tutapanga nini kifanyike, na moja wapo ni kwenda huko Kagera kuhamasisha watu ikitokea tumeshambuliwa. Bahati nzuri, Mzee Kawawa alipokwenda kumueleza Mwalimu, Mwalimu akakubaliana na wazo hilo kisha akaitisha mkutano wa *NEC*. Nikiwa kama Katibu Mkuu wa *TYL* nilijiandaa sana ili katika mkutano ule niwashawishi wajumbe kwa suala moja kubwa sana ambalo ni suala la wananchi kufundishwa silaha na Ulinzi wa Umma, *People's Militia*.

**IS:** *People's Militia*! Ndiyo!

**KNM:** Huko nyuma Umoja wa Vijana ulidai suala hilo lakini halikukubaliwa kwa kuwa viongozi wengi wa siasa na vyombo vya dola walikuwa hawajaelewa umuhimu wake. Kwa hiyo nilijiandaa kweli na kwa bahati nilipata nafasi nzuri.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Mwishoni mwa mwaka 1970, niliongoza ujumbe wa vijana wa Tanzania kwenda Senegal katika kongamano la *Pan-African Youth Movement,'* kwenda kukabidhi Ukatibu Mkuu ili nchi nyingine ishike uongozi. Katika msafara wangu nilikuwa na wajumbe watano akiwemo Jenerali Natepe, Kanali Kimbau na Charles Kileo. Mwaka huo huo mwezi Oktoba Guinea Conakry

ilikuwa imevamiwa na Wareno pamoja na wanajeshi wa mamluki, lakini wavamizi walishindwa vibaya kutokana na kushiriki kwa walinzi wa mgambo wa Guinea wakishirikiana na jeshi lao la taifa.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Kule kwenye mkutano mkuu wa *PAYM*, baada ya kukabidhi Ukatibu Mkuu tuliwashawishi washiriki kwamba Senegal isipewe Ukatibu Mkuu. Hali hii haikuleta picha nzuri kwa sababu nilisoma pale na dola ya Wasenegal walitegemea kwamba ningekuwa upande wao. Ulikuwa ni uamuzi wa *Liberation Movements* zote kwamba Senegal isipewe Ukatibu Mkuu kwa sababu umoja wa vijana wa Senegal ulikuwa ukifuata mtazamo wa Senghor ambao haukuwa unapinga ubepari. Kwa hiyo tukakubaliana tuipe Guinea.

**IS:** Guinea?

**KNM:** Eeh, Guinea Conakry.

**IS:** Aah!

**KNM:** Kwa jinsi walivyoweza kupambana na hao wavamizi wa Kireno na kuwashinda. Tukashinda katika Mkutano Mkuu na ikaamuliwa kwamba Katibu Mkuu mpya atoke Guinea. Baadaye wakaniomba niende rasmi kwa Rais Sekou Toure kumuarifu kwamba Mkutano Mkuu wa vijana wa Afrika umekuja kuungana na vijana na wananchi wa Guinea kusheherekea ushindi wa Guinea dhidi ya ubepari, na pia kuleta ujumbe kwamba vijana wa Afrika wameichagua Guinea kuchukua kiti cha Ukatibu Mkuu. Tulipofika Guinea tulipokelewa vizuri na *Politbureau* ya *Parti Démocratique de Guinée* ya Sekou Toure, tukapata nafasi ya kuzungumza na wale viongozi wa *People's Militia*, tukapata nafasi ya kukaa na kuzungumza na Dakta Kwame Nkrumah, na halafu tukapata nafasi ya kukaa na Amilcar Cabral, wote hawa walikuwa bado wako hai wakiishi Conakry.

**IS:** Ndiyo!

**KNM:** Cabral alikuwa rafiki yangu na tulikuwa tunafahamiana vizuri.

**IS:** Na ilikuwa kabla ya kukutana naye huko Conakry?

**KNM:** Nilifahamiana naye nilipokuwa huko Chuo Kikuu cha Dakar kwa sababu alikuwa akipita pale na pia alikuwa na makada wake pale Chuo Kikuu. Alipokuwa akipita pale ilikuwa lazima anitafute kwa sababu alikuwa anampenda sana Mwalimu kutokana na misimamo yake. Kwa hiyo tukalijadili sana suala la *People's Militia* na niliporudi hapa nikawa nimewiva.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Kule kwenye NEC nikajaribu sana kujenga hoja katika kupendekeza suala hilo. Na ikawa bahati kubwa sana Mwenyekiti wa Mara, Mzee Nyalandu Chacha, na Ndugu Sokoine wakaliunga mkono sana. Mzee Kawawa yeye msimamo wake juu ya suala hili ulikuwa imara sana maana kule Mtwara na Lindi alianzisha 'Malisha'.

**IS:** Kwani Sokoine alikuwa tayari mwanakamati wa NEC?

**KNM:** Hakuwa mjumbe wa NEC. Mwalimu alikuwa amealika mawaziri na manaibu wote kwenye kikao kile cha NEC na ikawa vizuri sana.

**IS:** Nafikiri yeye alikuwa Naibu Waziri?

**KNM:** Ndiyo, alikuwa Naibu Waziri wa Ulinzi. Hawa wawili [Sokoine na Chacha] na Mzee Kawawa walipoliunga mkono, suala la *People's Militia* likakubalika. Kwa hiyo tulipokwenda kuandaa Mwongozo ule tukaliweka suala hilo vizuri.

**IS:** Hebu Mzee Ngombale tuambie, kamati gani, na nani aliyekuwa katika kamati iliyoandaa Mwongozo?

**KNM:** Siwezi kuwakumbuka wote vizuri, lakini mwenyekiti alikuwa Mzee Kawawa. Pia nawakumbuka Hashim Mbita [Katibu Mtendaji Mkuu] na Sarakikya.

**IS:** Sokoine je?

**KNM:** Sokoine hakuwemo ila Babu alikuwemo.

**IS:** Alikuwemo kwenye kamati?

**KNM:** Ndiyo. Kwa kuwa mimi ndiye niliyewakilisha hoja kwa sura zote yaani kisiasa, kiuchumi na kiulinzi, wanakamati wakaniomba nikaandae rasimu ya mwongozo mwenyewe. Nikakubali lakini nikaomba Hashim Mbita tushirikiane. Tukauandaa, tukauleta, ukapita vizuri, kisha tukampelekea Mwalimu. Lakini Mwalimu akaondoa kipengele cha mwisho ambacho kilikuwa kinahusu utaifishaji wa majumba. Unakumbuka nyumba zilitaifishwa.

**IS:** Zilitaifishwa.

**KNM:** Ndiyo, zilitaifishwa na tuliweka katika kipengele cha mwisho.

IS: Katika Mwongozo?

KNM: Eeh! Tulikuwa na hoja ya kisiasa kwamba mpaka wakati ule [1971] ukitembea kuanzia Mnazi Mmoja kuelekea pwani nyakati za usiku, mji ule ulikuwa wa Waasia. Ukimwona Mwafrika ni mtumishi.

**IS:** Wafanyakazi wote wanaondoka jioni.

**KNM:** Ndiyo, wote wanaondoka. Tayari hilo lilikuwa tatizo huko Oysterbay kulikuwa kumekwisha malizika kwa sababu watu weusi walikwenda kule baada ya Wazungu kurudi makwao.

**IS:** Viongozi waliingia kule.

**KNM:** Eeh! Tatizo lilikuwa katikati ya mji [*Business District*]. Hoja yetu ilikuwa ni kwamba, tukiendelea na hali hiyo kuna siku hali italipuka, tutauana bure. Mwalimu aliiona hoja yetu, akaisoma, na kukubaliana nayo. Lakini hakuona haja ya hoja hiyo kuwa katika Mwongozo kwa sababu, ukishachukua hatua ya kutaifisha, tatizo la nyumba linakwisha. Mwongozo ni chombo ambacho kinaongoza watu muda mrefu. Baada ya kipengele hicho kuondolewa, Mwongozo ukapitishwa.

**IS:** Mzee Ngombale, sasa mimi nakumbuka kulikuwa na mambo mawili katika Mwongozo, hili la *People's Militia* kama ulivyoelezea kwa ufasaha kabisa, na la pili lilikuwa lile la ibara ya 15. Hili liliingiaje?

**KNM:** Ibara ya 15 inalaumu uongozi wa kinyapara. Ibara hiyo tuliiweka kwa makusudi na ilikubalika katika kamati yetu katika NEC na Mwalimu mwenyewe alikubali.

**IS:** Walikubali katika kamati yenu hamkuwa na mjadala juu ya hili?

**KNM:** Hapana, wakati tunaandaa Mwongozo alikuja Babu na wajumbe wengine tukapata muda wa kujadili. Katika mambo tuliojadili, ni pamoja na hili la ibara ya 15. Tatizo lilikuja kwa upande wa menejimenti kwenye viwanda na sehemu nyingine za kazi kwa sababu Mwongozo uliamsha vuguvugu kwa upande wa wafanyakazi la kutaka haki ya kuwakilishwa [Right of Representation]. Haki ya usawa na kadhalika. Kwa hiyo sehemu ile ya viongozi wanyapara, ikawachochea wafanyakazi kuwagomea wale viongozi ambao walikuwa wanachukua maamuzi bila kushirikisha wafanyakazi.

**IS:** Na wafanyakazi walitumia ibara ile?

**KNM:** Ndiyo, walitumia.

**IS:** Na kulikuwa na vuguvugu kuanzia mwaka 1971 hadi 1974.

**KNM:** Eeh! Vuguvugu kubwa, kwamba lazima wafanyakazi washirikishwe. Na unakumbuka wakati ule [1972], Mwalimu alitoa sera ya ushirikishwaji wafanyakazi [*Worker's participation*]. Baada ya Mwongozo Mwalimu aliniita na kuniambia kwamba kwa kuwa mimi ndiye niliyeanzisha suala la *People's Militia,* atanipeleka mkoani niwe Mkuu wa Mkoa na Katibu wa Mkoa ili kusimamia uanzishwaji wa ulinzi wa mgambo. Kwa hiyo nikawa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, kipindi hicho Pwani na Dar es salaam zilikuwa mkoa mmoja. Uanzishwaji wa mgambo nao ulikuwa na matatizo kama dhana.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Kulikuwa na kundi la viongozi wa taifa waliofikiria wanamgambo watokane na wanachama wa TANU tu. Mimi nilikuwa nasema kwamba, wanamgambo watokane na wananchi wazalendo, wananchi wenye mwamko wa ulinzi wa taifa lao. Na katika kutekeleza wajibu wangu kama Mkuu na Katibu wa Mkoa niliitisha mikutano ya wafanyakazi katika sehemu zao za kazi na kuwahamasisha ili wajiunge na ulinzi wa mgambo kwa msingi wa uzalendo wao. Tofauti hii ya msimamo kati yangu na baadhi ya viongozi wenzangu wa kitaifa ulilazimu kuitishwa Kamati ya Ulinzi ya Chama ya taifa. Baba wa Taifa ndiye aliyemaliza mvutano wa kimsimamo uliokuwepo alipoeleza kuwa wananchi watajiunga na ulinzi wa mgambo kwa msingi wa uzalendo wao wa kuipenda nchi yao na kuwa tayari kuilinda na kuitetea na sio kwa misingi ya itikadi ya Chama tu.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Kwa hiyo mimi ndiye nilieanzisha ulinzi wa mgambo nchini hapa nikiwa *RC* na Katibu wa TANU Mkoa wa Pwani.

**IS:** Aah! Na suala hili la kwamba wanachama tu ndiyo waajiriwe mlilitatua vipi?

**KNM:** Kama nilivyoeleza awali, nilimtafuta Mwalimu nikamweleza juu ya mvutano, na kwamba kuna suala hili, na nikamweleza juu ya mtazamo wangu na ule wa upande mwingine. Nikamwomba ahudhurie kikao ili aweze kufafanua, sababu yeye ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama. Katika kikao tofauti za mitazamo ilijitokeza waziwazi. Mwalimu alieleza kwa nini msingi wa mgambo uwe ni uzalendo na si msingi finyu kama ule wa Chama pekee.

**IS:** Sasa ningependa kuuliza masuali mawili. Moja ni kuhusu vuguvugu la wafanyakazi kati ya mwaka 1971 na 1974. Historia yetu hasa ya tabaka la wafanyakazi inaonyesha kwamba, mwanzo wafanyakazi walianza kwa migomo ambayo haikuwa imeandaliwa vizuri, lakini baadae walianza kuiandaa kwa ufanisi

zaidi. Mimi nakumbuka Mei Mosi ya mwaka 1974, Mwalimu alitoa hotuba ambapo aliuliza 'Unapogoma unamgomea nani?' Kwa kweli alijaribu kuzungumzia juu ya vuguvugu, na kwa kiasi fulani nafikiri hili liliwavunja nguvu wafanyakazi. Sijui wewe unakumbuka nini juu ya suala hili?

**KNM:** Unajua mimi ninavyokumbuka, tatizo la wafanyakazi wakati ule lilikuwa kwamba wafanyakazi walikuwa na mwamko zaidi kuliko viongozi wao. Katika kipindi kile sehemu ya uongozi wa wafanyakazi ulikuwa wakinituhumu kwamba mimi ndiye niliyekuwa nachochea migomo ya wafanyakzi. Lakini kilichokuwa kinatokea ni kwamba, wafanyakazi wakiwa na matatizo, viongozi wao walikuwa hawasaidii kupata ufumbuzi bali walikuwa wanaweka mbele sheria. Kwa hiyo walikuwa wanashindwa kuendeleza mapambano na harakati za wafanyakazi. Tofauti yao na mimi ni kwamba, nilikuwa nawauliza matatizo yao na kuwasaidia kutafuta ufumbuzi wa matatizo hayo.

**IS:** Suali la pili ni la kibinafsi zaidi. Kwanza ni kama ulivyotueleza, na hata katika makala yako ya mwaka 1967, iliyotolewa katika jarida la *Mbioni*,[4] ulitahadharisha kwamba kujenga Ujamaa ni mapambano na kuna watu ambao watapinga mapambano ya kitabaka nchini. Kwa kweli huu ni mtazamo wa Kimarxist na haufichi hapa.

**KNM:** Ndiyo, Baada ya kuandika makala hiyo, wale walimu wa Kimarekani wa pale Kivukoni walishangazwa nilivyoonyesha mtazamo wangu hadharani. Kwani kwao Wamarekani, ukiwa Mmarxist lazima ujifiche.

[4] Angalia Kingunge Ngombale Mwiru, 'The Arusha Declaration on Ujamaa na Kujitegemea and the Perspectives for Building Socialism in Tanzania', katika *Mbioni* (Jarida la Chuo cha Kivukoni, Juzuu III, na. X, Machi 1967, uk. 2-27) Imechapishwa tena katika John Saul na Lionel Cliffe (wahariri), 1973, *Socialism in Tanzania*, vol. 2, pp. 52-61, Nairobi: East African Publishing House.

**IS:** Sasa suali langu lilikuwa, tunajua Mwalimu hakuwa Mmarxist na alikuwa wazi kwa hilo. Sasa katika hilo, je, uliwahi kuwa na mgogoro wa kiitikadi na Mwalimu? Na kama ulikuwepo, je uliathiri mahusiano yenu?

**KNM:** Suali hilo gumu sana. Tuliwahi kutofautiana lakini tulitofautiana katika hali ya kawaida kama ambavyo mimi na wewe tunaweza kutofautiana. Mimi na Mwalimu tulikuwa na uhusiano mzuri sana, ambao haukuathiriwa na mitazamo yetu ya kiitikadi licha ya kwamba msaidizi wake. Mama [Joan] Wicken, alionyesha kutonikubali.

**IS:** Kwa sababu mama Wicken alikuwa *Fabian*?

**KNM:** Eeh! *Fabian socialist.* Alikuwa hanitaki haswa. Hata niliporudi, viongozi wote wa chama walikuwa wanataka niende Kivukoni isipokuwa yeye.

**IS:** Na yeye alikuwa mtu mzito sana pale Kivukoni kwa sababu alikuwa mjumbe wa ile *Cultural Trust.*

**KNM:** Eeh! *Education Trust!* Mwaka 1967 ni Mwalimu mwenyewe aliyetaka nihusishwe moja kwa moja na mambo ya ufundishaji wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, na akaanza kuniletea watu wa kuwafundisha Kivukoni, wakiwemo wenyeviti wa matawi ya mji wa Dar es salaam, wazee wazamani waliopigania uhuru, na vijana wa jeshi TPDF na JKT. Kila alipokuja kuzungumza na wanafunzi wangu na wakimuuliza masuali, kulikuwa hakuna matatizo kati yangu naye. Ila tatizo lilikuwa wakija viongozi wengine.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Mwezi wa kumi mwaka huo huo. Mimi, [Henry] Mapolu na wengineo, *Assistant Tutors*, tulienda kuonana na Mwalimu na tukajadili sana kuhusu nini kifanyike ili kueneza siasa ya Ujamaa. Mwishowe tulikubaliana kwamba tuwafundishe watu wote hasa viongozi kwa sababu watu wengi hawakuwa na uelewa juu ya suala zima la Ujamaa. Kwa kifupi naweza kusema kwamba mimi

na Mwalimu hatukuwahi kuwa na mgogoro. Nafikiri moja kati ya sababu ni kwamba, Mwalimu alikuwa na upeo mkubwa na pia alikuwa mkweli.

**IS:** Sasa hao viongozi wenzio waliokuwa hawakubaliani na wewe, walilichukuliaje suala hilo?

**KNM:** Mwanzoni mwa mwaka 1973 nilishitakiwa na viongozi wenzangu kwamba nilibadilisha Chuo cha Kivukoni kutoka Chuo cha TANU kuwa chuo cha *Marxism-Leninism.* Shitaka hilo lilikuwa zito kiasi kwamba viongozi hawa wakaanza kusherehekea kwamba ningefukuzwa kwenye Chama. Nikaitwa kwenye Kamati Kuu ili nijieleze, walionishitaki wakatoa mashitaka yao dhidi yangu. Tuhuma kubwa ilikuwa kwamba mimi nilikuwa nafundisha kuwa chama cha TANU kwa mwendo wake wa *mass party* hakingeweza kutufikisha kwenye Ujamaa. Ni kweli, kwani niliamini ili tufanikiwe kujenga Ujamaa lazima tuwe na Chama cha aina ya *vanguard party*, na hivyo ikalazimu nieleze mtizamo wangu kwa uchambuzi. Baada ya kuichambua mifumo yote miwili ya vyama na kuiweka katika mazingira ya nchi yetu, nilihitimisha kwa kusema kuwa Tanzania tunahitaji *a mass party with a vanguard*. Mwalimu na kikao kizima wakakubaliana na msimamo huo na mvutano ukaisha. Mimi na Mwalimu tulikuwa na mahusiano mazuri sana kutokana na ukweli kwamba, tuliheshimiana kimtizamo, kidini, kiitikadi, na kadhalika. Je, ulikuwa na jambo lolote la ziada ulitaka kulisikia?

**IS:** Hapana! Mimi naona tuelekee kwenye jambo lingine sasa. Tuzungumzie Azimio la Arusha. Kufikia miaka ya sabini, Azimio la Arusha lilikuwa limefikia ngazi ya juu yaani muongo huo wote kuanzia mwaka 1967 mpaka miaka ya 1977 na 1978, halafu vikaja vita vya Uganda, nafikiri ni mwanzo wa kuporomoka kwa uchumi. Na baadaye katika miaka ya themanini tukapata matatizo ya kiuchumi. Kwa maoni yako, unafikiri kwa nini Azimio la Arusha halikufanikiwa kama ilivyotarajiwa katika kipindi hicho cha matatizo ya kiuchumi na baadaye Serikali na Chama

vikaamua kubadili sera na mtazamo? Unadhani chimbuko la matatizo lilikuwa wapi?

**KNM:** Nionavyo mimi, Azimio la Arusha lilikuwa ni wito wa kujenga Ujamaa. Lakini nadhani kulikuwa na mapungufu mengi. Kwanza, tulichukulia kuwa ili kujenga Ujamaa lazima njia kuu za uchumi zishikwe na serikali na vyombo vyake, *state ownership*. Vilevile kuwepo ushirika wa wananchi wenyewe. Nadhani hatukulichukulia suala la kujenga Ujamaa kama ni suala la kukuza nguvu za uzalishaji-mali [*the development of productive forces*] katika jamii. Kwa hiyo tukazungumzia masuala mawili, *state ownership* na *cooperative ownership*, na kwa sababu hatukuzungumzia suala la kukuza nguvu za uzalishaji-mali, suala la umuhimu wa maarifa hatukulipa uzito mkubwa, ingawa Azimio la Arusha lenyewe linasema kwamba masharti ya maendeleo ni juhudi na maarifa. Na ndiyo maana katika Ujamaa Vijijini ilikuwa tu ni suala la wananchi kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wote. Lakini suala la maarifa sio kukaa au kuishi pamoja tu, bali je wanafanya kazi vipi? Suala la kanuni za kisasa za kilimo bora hazikutiliwa mkazo. Kwa mfano…..

**IS:** Mmh!

**KNM:** La kwanza mimi ninaloliona ni kwamba tulianza na tatizo, tulishindwa kuangalia *dynamics* za maendeleo katika jamii. Yaani, kipi kinachochochea na kusukuma maendeleo katika jamii. Tangu mwanzo, vyama vya ushirika havikuhamasishwa kutumia mbinu na nyanja za kilimo za kisasa ndio maana matokeo yake ni kwamba, ushirika haukutufikisha mbali. Kwa mfano, Kanda ya Ziwa walikuwa wakifanya vizuri kipindi cha ukoloni ukilinganisha na kipindi cha sasa.

**IS:** Lakini mwaka 1976 tulipiga marufuku ushirika na tukaleta mamlaka za serikali [*state authorities*].

**KNM:** Ndiyo! Kwanza tuliua serikali za mitaa [*local government*] mwaka 1972, halafu tukaua ushirika mwaka 1976. Zote hizi zilikuwa hatua zisizo za kidemokrasia. Ujamaa

unaosisitiza *state ownership* ni mbaya kwa sababu uzoefu umeonyesha hapa kwetu na hata kwingineko, rushwa huzagaa, na rushwa ikishaingia inazaa kutokuwepo kwa ufanisi. Mimi ninachoweza kusema ni kwamba tulikuwa na nia njema, hasa Mwalimu, lakini hatukuwa tumejizatiti vizuri.

**IS:** Sasa Mzee Ngombale, katika suala hili la nguvu za uzalishaji-mali na umuhimu wa maarifa (*the role of Science and Technology)* nafikiri tutakubaliana kwamba haya si masuala ya kiufundi bali ni ya kijamii zaidi.

**KNM:** Mmh!

**IS:** Ukiangalia kilimo chetu, ulishawahi kuandika na kufanya uchambuzi mzuri sana katika suala hili kwamba hauwezi kutenganisha njia za uzalishaji (*means of production*) na mahusiano ya uzalishaji (*productive relations*). Na ukizungumzia mahusianao ya uzalishaji, unazungumzia mahusiano ya kitabaka (nani anayezalisha na nani anayenyonya na kulimbikiza). Sasa ukitaka kuendeleza kilimo, sayansi na teknolojia, bila shaka kama jamii, utakuwa na ulazima wa kuwa na ulimbikizaji (*accumulation*). Sasa kama akiba (*surplus*) yako, nguvu kazi yako, lakini mtaji – ziada (*surplus*) wako haubaki katika nchi na kutumiwa katika maendeleo, huwezi ukapata maendeleo ya nguvu za uzalishaji mali. Kwa hiyo moja kwa moja tunaona kwamba, mfumo wetu ulikuwa ni sehemu ya mfumo wa kibepari wa kimataifa. Ingawa tulitaifisha, je, tulibadili mahusiano ya uzalishaji? Kama ulivyosema kuwa kutaifisha haina maana kwamba ni ujamaa.

**KNM:** Hapana, bado!

**IS:** Sasa hauoni kana kwamba hili ndio lilikuwa tatizo kubwa? Kwa sababu Azimio lilitaifisha kila kitu mpaka kufikia hatua ya kuumiza watu.

**KNM:** Mwaka 1971 nilipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa (RC) wa Pwani, wenzangu serikalini wakaamua kutaifisha mabucha ya Dar

es salaam. Nilihangaika sana kama Mkuu wa Mkoa kwa sababu ilinibidi kusimamia upatikanaji wa nyama.

**IS:** Je, chama kilikaa chini na kufanya tathmini kuangalia kwa nini Azimio la Arusha halikufanikiwa?

**KNM:** Ilipofika mwaka 1992, tuliunda kamati ya kuandaa muelekeo wa sera za Chama katika miaka ya tisini. Kamati hiyo iliundwa kwa ajili ya kuandaa sera ya miaka hiyo ya tisini. Kazi ya kwanza ya hiyo kamati ilikuwa ni kuchambua ufanyakazi wetu kwa misingi ya Azimio la Arusha mpaka wakati ule. Na hasa tulichambua sekta ya Umma na vilevile sekta ya ushirika. Siyo tu tulifanya uchambuzi wa ndani, pia tulijadili matokeo katika nchi za kisoshalisti yaliyosababisha kuanguka kwa serikali za nchi hizo.

**IS:** Kwa hiyo hii ilikuwa ni baada ya utawala wa Mwalimu?

**KNM:** Mwaka wa 1990, tulifanya uchambuzi wa kusambaratika kwa serikali za nchi za kisoshalisti katika NEC ya mwezi wa pili, wakati Mwalimu alikuwa bado ni Mwenyekiti wa Chama. Mwisho tukaja kujadili kama tuendelee na mfumo wa Chama kimoja au mfumo wa vyama vingi, na tukamwambia Mwalimu aanzishe huo mjadala. Mada ya uchambuzi wa suala hili liliwasilishwa na ndugu Benjamin Mkapa aliyekuwa katibu wa NEC wa mambo ya nje.

**IS:** Kabla ya hiyo, si tathmini hasa ya uchambuzi wa Azimio la Arusha ilifanyika mwaka 1981?

**KNM:** Mwaka 1981 haukuwa uchambuzi hasa, ila ulikuwa ni mkusanyiko wa matatizo yaliyotufanya tudai mjadala. Utakumbuka vita vya Kagera vilitufilisi na hali ya kiuchumi ikawa mbaya sana. Mwalimu akasema kwamba, baada ya miezi kumi na nane mambo yangekuwa nafuu, lakini hayakuonekana kuwa nafuu. Lakini kipindi kilekile ndio Jumuiya ya Afrika Mashariki ikawa imevunjika, halafu bei za mafuta zikawa zimepanda sana. Kwa hiyo hayo ndio matatizo yaliyotufanya tujadili hali ilivyo, kipindi hicho demokrasia ilikuwa finyu katika

chama, kwa sababu wajumbe wengi wa NEC walikuwa hawatokani na uchaguzi bali uteuzi. Pia kulikuwa na matatizo kama ya wakati huu, kuna watu waliokuwa wanadharau nadharia ya chama huku wakisema kwamba sisi tuna mawazo mafupi ila vitendo vyetu ndio virefu. Lakini vilevile katika dola, wabunge wengi walikuwa wanateuliwa, kwa hiyo ule mjadala wa mwaka 1981 ulikuwa unatambulisha masuala ya kutaka demokrasia zaidi katika chama na hata katika vyombo vya dola. Vilevile ukatoa maelekezo zaidi juu ya umuhimu wa nadharia na umuhimu wa kujikosoa na kukosoana katika shughuli zetu, badala ya kufichiana na kuheshimiana sana. Lakini vilevile ndio uliozaa suala hili la haki za binadamu kuweza kuhusishwa waziwazi katika katiba. Mwezi Septemba mwaka huo huo, Warioba na Msekwa waliongezwa kwenye kamati kwa sababu ya uzoefu wao katika masuala ya katiba na sheria ili kuweza kuangalia ni jinsi gani vyombo vya serikali [*state organs*] vinaweza kupanuliwa.

**IS:** Hiyo unayoizungumzia ni ile ya Halmashauri ya kuagiza kuwa kuwe na mjadala wa kitaifa na baadaye ndiyo tukarekebisha katiba kuweka haki za binadamu?

**KNM:** Baada ya mwongozo ule, kukawa na mjadala uliopelekea marekebisho ya katiba.

**IS:** Kabla ya huo wito wa NEC kulikuwa na Mwongozo wa mwaka 1981, miaka kumi baada ya mwaka 1971. Mimi sijawahi kuona waraka wa Chama kama huo wa mwaka 1981, kwa sababu huu ndio hasa ulikuwa uchambuzi wa yaliyotokea baada ya Azimio la Arusha. Na unaibua masuala ya msingi sana mbali na hayo ya demokrasia na haki za binadamu. Msimamo na mtazamo wa waraka huo ni kusema kwamba, kwa kweli chini ya mwavuli wa Azimio la Arusha, tulichojenga sio ujamaa bali ni Ubepari. Unasema, ‘ni kuwa jitihada zetu za kuunda na kupanua sekta ya umma haikuambatana na jitihada ya kutosha kuwaelimisha, kuwaandaa, kuwajenga wafanyakazi na viongozi wa kazi katika misingi ya kufanya kazi kwa nidhamu na ari, msingi ya uzalendo na uaminifu kwa umma. Hali hii imeathiri uzalishaji na utoaji wa

huduma katika sekta hii' (ibara 34). Ibara ya 35 inasema, 'Zaidi ya hivyo, wakati mwingine, katika miaka kumi na minne tangu Azimio la Arusha, Chama, Serikali na vyombo vyake vimetumika kukuza sekta ya kibepari nchini katika viwanda, biashara, usafirishaji, ujenzi na kadhalika na Ubepari huo uliopanuka katika kipindi hiki umeimarisha vitendo vya kuvuruga na kudhoofisha sekta yetu ya Umma.'

**KNM:** Sasa unamwambia yule aliyeandaa!

**IS:** Zaidi ya hapo, nazungumzia jambo ambalo sijawahi kuona kabisa katika nyaraka za Chama: 'Uchambuzi huu hukiwezesha Chama kuelewa migongano ya maslahi ya tabaka ambayo imejitokeza nchini. Migongano hii ina mizizi yake katika mgongano wa msingi kati ya ujamaa na ubepari, kati ya maslahi ya wakulima na wafanyakazi kwa upande mmoja, na ya ubinafsi, ubwenyenye na ubepari ambao umekuwa ukijengeka tangu Azimio la Arusha kwa upande mwingine' (ibara ya 50). Kwa hiyo, waraka huu unasema kwamba sisi tulichofanya ni kujenga ubepari ndani ya ujamaa na ndani ya mashirika ya umma. Pili, kumekuwa na mapambano ya kitabaka (migongano wa maslahi ya kitabaka). Nilichotaka kuuliza ni kwamba, Mwongozo huo ulienda mbali zaidi ya Azimio na hata Mwongozo wa mwaka 1971?

**KNM:** Ndiyo! Mwongozo huo ulikuwa wa kiitikadi zaidi kuliko miongozo iliyopita.

**IS:** Nilichotaka kujua ni chimbuko lake, ilitokeaje hii?

**KNM:** Kama ilivyokuwa katika Mwongozo wa mwaka 1971, mimi nilihusika na kuanzisha mjadala wa mwaka 1981. Kwanza mimi nilikuwa Mbeya wakati ule, nikaja kwenye NEC, rafiki yangu akaniita akaniambia kwamba, kuna ujumbe wangu kutoka kwa [kiongozi mmoja, jina linahifadhiwa] unaosema kwamba, *mood* ya Mwalimu siyo nzuri na hatakubali mijadala mikali, kwa hiyo ameniambia kwamba, usianze mambo yako. Lakini nikamwambia, sikiliza, kwanza, hiyo haiwezekani kuwa *message*

kutoka kwa Mwalimu na la pili, mimi nimejiandaa kuja kuzungumza kuhusu hali ilivyo sasa hapa nchini kwa hiyo kama [huyo kiongozi] anataka kunitisha mimi huwa sitishiki, na nitaendelea na mpango wangu, na kwa Mwalimu siendi. Kwa hiyo nikajiandaa, na tulivyofika kwenye NEC nikanyoosha mkono na kumwambia Mwalimu kwamba, tumeona ajenda za mkutano, lakini mimi nina pendekezo. Hali ilivyo nchini ni nzito, kwa hiyo ningeomba tujadili hali ilivyo sasa nchini halafu baadaye tutapitia hayo mambo ya ajenda. Mwalimu akasema, 'Unafikiria hivyo?' Nikamwambia mimi nafikiria hivyo. Akaniuliza kama nipo tayari, nikamjibu ndiyo. Akasema, ni kweli kwamba hali inastahili izungumzwe, na kisha akaniruhusu kuanza mjadala. Ingawaje sikuwa nimeandaa *notes*, nilikuwa nimeandika vidokezo ambavyo viliniwezesha kuzungumza kwa takriban saa mbili. Baada ya hapo, Mwalimu akaahirisha kikao. Akiwa nje, akatuma mtu aje kuniita, na nilipofika nje akaniambia, 'Maneno yako safi sana! Sasa unaweza kuendeleza mjadala mzuri? Kwa sababu tusiende ndani halafu watu waanze kuongea mambo ya hovyo hovyo.' Nikamwambia kwamba nitajaribu kuwashawishi lakini wewe mwenyewe unajua *composition* ya watu wetu. Tukarudi saa tisa na wakajitokeza watu fulani na kuchangia changia, lakini Mwalimu alikuwa ameshaamua. Baada ya pale akafunga mjadala na kuunda kamati iliyoitwa 'Kamati ya *programme*' iliyohusika na kuandaa *programme* ya Chama. Katika kamati hiyo tulikuwepo mimi (Katibu na *Rapporteur*), Syovelwa (Mwenyekiti), Moses Nnauye, Kisumo, Getrude Mongela, Maalim Seif, na wengine. Na baadaye Msekwa na Warioba wakaongezwa kwenye kamati. Baada ya kupitishwa na Halmashauri Kuu, kuliitishwa Mkutano Mkuu kwa ajili ya Mwongozo huo. Tulimpelekea Mwalimu *draft*, akakaa nayo kwa muda wa mwezi mmoja, baadaye akatuita na kutuambia kwamba, hatabadilisha hata kidogo. Akasema ataitisha Mkutano Mkuu wa Chama kwa sababu alikuwa anataka ile document ipitishwe na Mkutano Mkuu. Kwa hiyo Mkutano Mkuu ukafanyika mwezi wa kwanza mwaka 1982. Lakini pale kwenye mkutano, Mwalimu

akapiga *coup*, alinionea sana, kwa sababu jana yake mimi na Syovelwa tulikwenda kumuona na kumwambia kwamba, Mkutano utafanyika kesho yake, tukapatana naye vizuri kwamba yeye ndiye atakayewasilisha. Lakini dakika kumi kabla ya mkutano kuanza, akanifuata na kuniambia kwamba Mwalimu amesema mimi niwasilishe yeye hatowasilisha ila atasema tu maneno machache kwa ajili ya ufunguzi. Nikasema haiwezekani kwa sababu nilikuwa sijajiandaa. Akasema, 'Yeye ndiye amesema, kwa hiyo mimi siwezi kubadili maneno yake na ameshatoka Msasani anakuja.' Ikanipa tabu kweli, nikamngoja pale nje, alipofika, tukaenda kwenye ofisi ndogo na nikamwambia Mwalimu kwamba, umesema niwasilishe lakini sijajiandaa na hapa nilikuja tu kusikiliza. Akasema kuwa yeye pia hajaandaa kwa hiyo mimi ndiye niliyekuwa nastahili kuwasilisha. Ilibidi nikubali.

**IS:** Uchambuzi huo ulikubaliwa na Chama?

**KNM:** Eeh! Acha Chama, Mwalimu mwenyewe alikaa nao kwa muda wa mwezi mmoja.

**IS:** Mwalimu katika mwelekeo wake, kitu ambacho alikuwa hakubaliani nacho kabisa ni suala la mapambano ya kitabaka. Na huu Mwongozo wa chama kwa mara ya kwanza uliweka wazi suala la mapambano ya kitabaka. Wewe ulizungumzia mwaka wa 1967, ukaita lile tabaka kama *political bureaucratic class* ambalo linakubaliana na ubeberu. Na dhana ile unaikuta katika Mwongozo na unasema wazi kwamba tulichojenga ni ubepari ndani ya mashirika ya umma, na kuna mgongano wa maslahi kati ya matabaka haya na wafanyakazi na wakulima.

**KNM:** Aliusoma na akakubaliana nao. Kwa jinsi alivyokuwa hodari, alikutana nasi na akatuambia hana la kubadili ila yeye kama Mwalimu angeweza kuongeza nukta na kadhalika. Vinginevyo, ilikuwa kazi nzuri. Lakini akasema, 'Tatizo langu, viongozi wangu wanaelewa haya?' Ndio maana akataka Mkutano Mkuu uitishwe.

**IS:** Vipi kuhusu wanakamati wenzio, hawakulipinga hili?

**KNM:** Kamati ilikuwa imeundwa na watu waelewa na pia mimi na baadhi ya wenzangu tulikuwa hodari katika kushawishi na kutetea hoja.

**IS:** Wakati mlipofanya uchambuzi mlikuwa tayari mmechelewa?

**KNM:** Unajua, tatizo ni uwezo wetu wa kujenga na kuandaa makada na uongozi. Hilo ndio lenye matatizo. Mambo mengi tumeshindwa kwa sababu hatukushirikiana vizuri katika kuandaa watu. Mambo ya kubadili nchi yanataka watu wenye ari ya kujituma, wawazi, waaminifu, na kadhalika.

**IS:** Uchambuzi huo ulikuwa sahihi ingawa haukueleza namna nzuri ya kutatua matatizo. Kwa hivyo, ubepari uliojengeka ndio hatimaye ukashinda si ndivyo?

**KNM:** Na ubepari kwanza hauna nguvu…

**IS:** Ni ubepari uchwara [*comprador*].

**KNM:** Kama tunakuwa na watu wenye fikra moja, kuna uwezekano mkubwa wa kubadili nchi, lakini *opportunism* ndiyo kubwa, na tumepuuza sana upande wa Chama. Kwa mfano, hili suala la kuchanganya wafanyabiashara katika siasa.

**IS:** Kuhusu hilo, suala la wafanyabiashara, kipindi chote cha Azimio la Arusha Chama kilijitambulisha kama chama cha wakulima na wafanyakazi, na baada ya Azimio la Zanzibar, Chama kikafungua milango yake kwa wengine hasa kwa maana ya wafanyabiashara. Na jambo hilo kwa mara ya kwanza liliwekwa wazi katika *Fourth Congress* ya Chimwaga. Kuanzia hapo wale wasiokuwa wakulima na wafanyakazi wakaruhusiwa kujiunga na chama. Hiki kilikuwa kipindi cha Mzee Mwinyi na aliyetoa hotuba kusema kwamba tufungue milango alikuwa Kingunge Ngomable Mwiru. Tena kwa ufasaha kabisa, na mimi nakumbuka vizuri sana kwa sababu nilikuwa nasikiliza kwenye

redio, ukatoa mfano wa Engels ambaye alikuwa ni mwanaviwanda [*industrialist*],[5] kuhalalisha kuwa akina Reginald Mengi na Rajani waruhusiwe kuwa wanachama. Unalielezaje hilo?

**KNM:** Tuanze na maamuzi ya Zanzibar kwa sababu haya nayo yanaleta mkanganyiko. Kwanza yale maamuzi tuliyazungumza mara ya kwanza mwezi wa pili mwaka 1990, Mwalimu akiwa mwenyekiti. Na kabla ya kuyazungumza yeye ndiye aliyeniita mwishoni mwa mwaka 1989 akiwa na Mzee Mwinyi, akaniambia ana tatizo na katiba kwa sababu alifikiri hana sifa ya uanachama kutokana na kuwa na mali nyingi sana. Alinieleza kuwa alipostaafu uraisi Watanzania walimchangia ng'ombe na mali nyingine nyingi. Baadaye akaniomba kama Mkuu wa Itikadi nikaisome katiba niangalie sifa za uanachama na kisha niandae mapendekezo ya kuhuisha katiba ya Chama. Katiba ile ilikuwa imeandaliwa na Kamati ya watu ishirini, kumi kutoka bara na kumi kutoka Zanzibar. Katiba ya TANU masharti ya kuwa mwanachama yalikuwa mawili tu, kuwa mkulima au mfanyakazi. Sisi wanakamati (ya watu ishirini) tukajifanya wajamaa zaidi kwa hiyo tukachukua miiko ya uongozi ya Azimio tukaiweka na kuiorodhesha kwamba ndio masharti ya uanachama na sio ya uongozi. Kwa hiyo, nilimuelewa Mwalimu aliposema kwamba hana sifa za uanachama.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Lakini hatukuwa sahihi kwa sababu kwenye Azimio la Arusha linazungumzia miiko ya viongozi na lengo lake lilikuwa

---

[5] Frederick Engels, mwanafalsafa wa Kijerumani alikuwa mwenzie Karl Marx ambao kwa pamoja ni waasisi wa nadharia ya usoshalisti wa kisayansi. Ili kumsaidia aendelee kuandika juzuu zake juu ya mfumo wa kibepari na pia kuendelea na mapambano ya kisiasa, hususan kuunda umoja wa tabaka la wafanyakazi, Engels aliendelea kufanya kazi katika kiwanda cha baba yake ili aweze kumsaidia Marx kifedha. Marx mwenyewe hakuwa na kazi ya kuajiriwa.

ni kuwazuia viongozi wasitumie nafasi zao kwa manufaa yao binafsi. Kwa hiyo nikapata mawazo ya kuondoa ile miiko kwenye masharti ya uanachama. Lakini la pili, tukatazama suala la sifa za mwanachama. Kusema kwamba mwanachama awe mkulima au mfanyakazi inatosha? Kuna masuali, kwa mfano, kijijini kuna mfanyabiashara mwenye duka lake. Uendeshaji wa duka tu ndiyo shughuli yake. Je, huyo ni mkulima au ni mfanyakazi? Na watu wa namna hii wapo katika maeneo mbalimbali. Mwingine anaishi kwa kuandika vitabu, sasa ni mkulima au ni mfanyakazi? Kwa hiyo tukasema tuongeze kipengele kwamba, mwanachama awe mkulima, ama mfanyakazi au mtu mwenye shughuli yoyote halali ya kujitegemea kiuchumi.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Lakini mazungumzo ya NEC yaliingia kwenye masuala mapana zaidi, masuala ya mali na vinginevyo. Mwezi wa pili mwaka 1990 nilipokuja kuwasilisha ile mada, mjadala ulikuwa mkali sana. Mazungumzo yalionyesha kuwa uelewa wetu wa nadharia ya ujamaa ulikuwa mdogo. Kwa mfano, mjumbe mmoja alisema kwamba katika ujamaa mali ni haramu! Pia tulijadili mambo ambayo mtu anaweza kufanya kwa uhuru na bila wasiwasi. Licha ya mjadala kuwa mgumu na Mrefu, Mwalimu aliufurahia na kuagiza kwamba baada ya mjadala ule mada ikaandaliwe vizuri na kuwasilishwa tena kwenye mkutano wa NEC ambao ungefuata. Mkutano huo wa NEC ulifanyika Zanzibar baada ya Mwalimu kuwa amekwisha jiuzulu uenyekiti wa Chama. Kwa ujumla yaleyale tuliozungumza kwenye kikao cha Mwalimu ndiyo yaliyojadiliwa katika mkutano huo na kupitishwa. Sasa watu watasema kwamba Azimio la Zanzibar liliua Azimio la Arusha, lakini siyo kweli.

**IS:** Lakini miiko tunayoizungumzia sio kwa watu wa kawaida, ni kwa viongozi. Na kiongozi alikuwa ameelezwa vizuri katika Azimio. Lakini katika katiba iliyotokana na Azimio la Zanzibar, kama mlipitisha au hapana, ilitafsiriwa kwamba, miiko ya

uongozi nayo imefutwa. Kwa hiyo viongozi sasa wakaingia kwenye biashara.

**KNM:** Hapana! Ndiyo maana tulipoweka sawa hili suala la masharti ya uanachama, suala la viongozi tukaliweka kwenye katiba ibara ya 18 na 19, zisemazo kwamba ni mwiko kwa kiongozi kutumia nafasi yake ya madaraka au ya mwenzake kwa faida yake binafsi ama kwa upendeleo. Kipengele kingine kinaeleza kuwa ni mwiko kwa kiongozi kupata mapato ya kificho kwa kiongozi. Sasa hii haijachukua miiko ya Azimio la Arusha kwa sababu, ile miiko ukiitumia leo haina maana. Kwa sababu mingine inasema usiwe na hisa katika kampuni yeyote, kwa mfano.

**IS:** Kwa nini haina maana?

**KNM:** Sasa leo utasema kuwa na hisa katika kampuni ni kosa?

**IS:** Kama wewe ni kiongozi.

**KNM:** Eeh! Kwa nini?

**IS:** Kwa wakati ule ilikuwa ni wazi kwamba, wewe ukiwa katika uongozi huwezi ukawa na hisa katika mashirika ya kibepari.

**KNM:** Kwanza, wakati ule suala la hisa lilikuwa ni la kinadharia, nani alikuwa na hisa?

**IS:** Mtindo huo ulianza baada tu ya uhuru. Makampuni ya nje na hata ya ndani yalitumia viongozi kuchukua hisa ili kuhalalisha vitendo vyao.

**KNM:** Lakini bado ilikuwa kinadharia sana, watu wengi walikuwa hawajui. Katika uchumi wa kisasa, njia ya kumiliki mali inatendekaje bila kumiliki hisa? Unaposema viongozi wasimiliki hisa, unamaanisha wasiwe na mali kabisa?

**IS:** Ndiyo iliyokuwa miiko ya Azimio la Arusha. Wewe ukiwa na nyumba na unaishi katika nyumba hiyo hapakuwa na tatizo hata wakati wa Azimio la Arusha, bali kama una nyumba na unapangisha, hilo lilikuwa tatizo.

**KNM:** Ndiyo maana nasema, yale masharti ya Azimio la Arusha

yamepitwa na wakati. Ukiyaweka leo na kufanya kuwa masharti, hayaendani kabisa na wakati.

**IS:** Hayaendani na wakati kwa sababu ya mfumo tulioukumbatia baada ya mwaka 1985. Baada ya Mwalimu kung'atuka, tulifungua soko huria na kukumbatia uliberali….

**KNM:** Lakini hata Mwalimu alipokuwa hai, alishawahi kununua hisa.

**IS:** Kama Mwalimu alisitisha kuwa mjamaa, nadhani hilo halituhusu. Lakini ninachosema ni kwamba, tukubali kwamba hili liliendana na mfumo huo tuliokubali. Ni kweli tulishinikizwa, lakini pamoja na kushinikizwa, wale ambao uliwazungumzia hapa [mabepari], ndiyo wakaanza kuonyesha makucha yao. Utakumbuka Mzee Ngombale, tulipoeneza sera ya ubinafsishaji watu wa kwanza kuja mbele na kusema kwamba watachukua mali hizo walikuwa ni wale wale viongozi wa mashirika ya umma.

**KNM:** Ndiyo! Sisi katika NEC tulikubaliana kuwa kama utataka kuendelea na masharti ya Azimio la Arusha vile yalivyo, utakuwa hauko sahihi na hauendani na wakati. Ngoja nikupe mfano. Ule ule mwaka wa 1967, sharti la kutokuwa na nyumba ya kupangisha lilikuwa limekwisha kuonekana kwamba siyo sahihi. Tulianzisha mafunzo kwa mabalozi wa nyumba kumi. Sasa kila Jumamosi baada ya kazi hiyo ya kuwafundisha mabalozi tulikuwa tunaonana na Mwalimu ili kumpa ripoti. Ripoti ya kwanza ilikuwa ya Mwandoro ambaye alimwambia Mwalimu kwamba 'kule ulikonituma, mabalozi wa nyumba kumi wote ndio wenye nyumba za kupangisha, na tulipowasomea hili sharti walitushangaa kweli'. Ikabidi Mwalimu atoe maelezo kwamba katika kujenga ujamaa lazima kuwe na lengo na kanuni. Na kama tusipoangalia vizuri hizi kanuni zinaweza kutuzuia kufikia malengo. Hivyo Mwalimu aliagiza kuwa sharti hili litekelezwe kwa uangalifu. Hili linatuonyesha kwamba tangu mwaka 1967 sharti hili lilikuwa sio sahihi.

**IS:** Hilo siyo tatizo kwa sababu unaweza kutofautisha mapato ya mwanachama wa kawaida anayefanya kibarua usiku kama mlinzi na asubuhi kama kondakta. Hilo linaweza kutofautishwa, lakini kilichomaanishwa siyo hicho. Rodney alitoa dhana nzuri sana alipokuwa anazungumzia kuhusu wafanyakazi [*working people*]. Lakini watu hasa waliokuwa wanabanwa katika Azimio la Arusha walikuwa ni viongozi wa juu.

**KNM:** Lakini sasa kwa sababu tuliwaorodhesha na mpaka tukamuorodhesha balozi wa nyumba kumi….

**IS:** Hilo ndilo tatizo. Kama tulivyofanya katika mabucha, ni suala hilo hilo. Na hao waliokuwa wanaorodhesha na kutoa kauli kama hizo, hawakuwa wajamaa, walitaka kuhujumu uchumi na walikuwa wanatoa mifano kama hiyo [ya watu wa kawaida] kwa maslahi yao.

**KNM:** Sasa nimalizie kwenye jambo hili la mwaka 1992 [mwelekeo wa sera za CCM katika miaka ya tisini]. Nilikuwa nasema kwamba, tulifanya uchambuzi wa uzoefu wa utekelezaji wa Azimio la Arusha tukakuta tatizo la sekta ya umma, tatizo la rushwa na tatizo la ukosefu wa ufanisi [*inefficiency*]. Tukatazama nchi nyingine tukaona matatizo ni hayo hayo isipokuwa kwa nchi za China na Vietnam. Baadae tukaja na uamuzi kwamba ule msimamo wa Azimio la Arusha wa kwamba ili kujenga ujamaa lazima njia kuu za uchumi zishikwe na dola una matatizo. Pia siyo sahihi kufikiri kwamba bila *state ownership* Ujamaa hauwezekani. Kwa hiyo tukasema kwamba, lengo la ujamaa na kujitegemea katika miaka ya tisini na kuendelea ni kuona kwamba wananchi wenyewe wanamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao - mtu mmoja mmoja, kwa kupitia vikundi vya watu, kwa kupitia vyama vya ushirika vya aina mbalimbali, kwa kupitia kampuni za wananchi ambao maelfu ya watu watakuwa wana umiliki au hisa, na kwa kupitia wananchi kumiliki hisa katika mashirika ya ubia. Na mpaka sasa ndivyo tunavyosema kwamba lengo siyo *state ownership*, bali lengo ni wananchi wenyewe kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao kwa njia mbalimbali.

**IS:** Mmh!

**KNM:** Najua baada ya ule uchambuzi uliandika na kunikosoa na kuniita mtu hatari sana, lakini sikutaka kukujibu kwa sababu wewe ni rafiki yangu sana. Nikasema acha watu waseme na kuona upande mwingine unasemaje, Hivi lilikuwa jarida gani?

**IS:** *Family Mirror*.

**KNM:** Eeh! *Family Mirror*. Lakini nasema kwamba ukitazama vizuri muelekeo wa sera za CCM katika miaka ya tisini utaelewa mengi kuhusu ujamaa kwa sababu kuna ufafanuzi mzuri. Katika mwelekeo wa sera za CCM katika miaka ya 2000 mpaka 2010 tumepiga hatua zaidi. Haitoshi tu kusema kwamba uchumi umilikiwe na kuendeshwa na wananchi wenyewe kwa sababu watu wetu ni masikini kwa ujumla. Ukisema tu lengo la ujamaa ni wananchi wenyewe kumiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao kwa njia mbalimbali bila ya kuwaundia mazingira yatakayowawezesha kumiliki na kuendesha uchumi, itakuwa maneno tu. Kwa sababu wale wenye uwezo, wale waliosemwa katika mwongozo wa mwaka 1981 [mabepari], ndio watakaochukua kila kitu.

**IS:** Sasa mzee Ngombale, historia nzima inatufundisha kwamba lengo la ujamaa, hata wakati wa Azimio la Arusha, halikuwa *state ownership*. Lengo la ujamaa ni kufuta unyonyaji wa kitabaka. *State ownership* ni chombo cha kutufikisha kwenye ujamaa. Unaweza kuwa na *state ownership* na bado ukawa na mfumo wa kibepari na unyonyaji. Na ndiyo nilichosema mwaka wa 1972. Na tunaposema kwamba lengo la ujamaa ni wananchi wenyewe kumiliki na kuendesha uchumi wao wenyewe [*people's capitalism*], ni suala lililozungumzwa katika miaka ya thelathini, limepitwa na wakati.

**KNM:** Kwa nini?

**IS:** Berle na Means [waandishi wa Kimarekani] waliandika kitabu kilichokuwa kinazungumzia *people's capitalism,* jinsi gani maelfu ya watu wanaweza kumiliki hisa.[6] Hii ni historia ya kale na haibadili mfumo wa kibepari kwa sababu tunajua licha ya kwamba maelfu wanaweza wakawa na hisa asilimia 10 na wengine wote wa asilimia moja moja, bado watakao miliki kampuni ni mabepari. Tunajua wazi kwamba hiyo *people's capitalism* ilikuwa inatumiwa kuhalalisha ubepari.

**KNM:** Tunatambua mtu mwenye hisa 10 hawezi kulingana na wa hisa 50, na wananchi wetu wengi si tu hawana asilimia moja moja, bali hawana mitaji, na kwa hiyo ushiriki wao katika uzalishaji unakuwa mdogo kabisa. Ndio maana tumeanzisha sera ya uwezeshaji ili wananchi waweze kushiriki na kupambana katika mfumo wa kibepari. Tunawawezesha wananchi kwa mikopo ili wamiliki njia za uzalishaji mali, na ilani ya CCM inaelezea hili suala vizuri kabisa.

**IS:** Mzee Ngombale, tatizo hapa ni mfumo, unaposema unawawezesha wananchi, suali la msingi unawawezesha kupitia nini? Utawawezeshaje wananchi wakati mtaji wako unamilikiwa na mabepari wa kimataifa, kwa lengo la kulinda maslahi yao. Ndani ya mfumo huo tunajua dola ndio linaloongoza nchi na wale watakaowezeshwa ni ma*comprador*. Inatambulika wananchi sio *homogeneous*, na wanaopata mtaji ni wale wanaoweza kuendeleza mfumo wa kinyonyaji.

**KNM:** Ni kweli nguvu ya ubepari wa kimataifa ni kubwa. Hata hivyo bado uko mwanya kwa wananchi katika kila nchi kuungana na kupambana na kupata ushindi hatua kwa hatua dhidi ya ubeberu. Sera za uwekezaji wa wananchi kiuchumi ikiongozwa na itikadi sahihi ya ujamaa na kujitegemea na njia muafaka za *organisation*, kwa mfano, ushirika, unaweza kutuhakikishia

[6] Adolf Berle na Gardiner Means, 1932/2017. *The Modern Corporation and Private Property*. Harcourt, Brace & World/Routledge.

maendeleo ya ujamaa yanayoambatana na kukua kwa nguvu za maendeleo katika jamii.

**IS:** Haya yote unayoyasema hayaonekani popote katika sera wala mwelekeo wa Chama na Serikali. Ukweli ni kwamba tumekumbatia ubeberu bila kuhoji. Kumbuka, lengo la siasa ya ujamaa ni kuondoa mahusiano ya unyonyaji katika uzalishaji mali na baina ya mtu na mtu. Na dola ilijaribu kusimamia hilo. Sasa, leo nguvu ya dola katika nchi iliyojikita katika matabaka itamlinda nani? Hakika sio mwananchi! [Saa za kufuturu ilifika na maongezi ilibidi yafungwe, ingawa Mzee Ngombale hakuafikiana na Shivji kuhusu hoja hii ya *people's capitalism* au ubepari wa umma].

*Mazungumzo haya yalifanyika kwa tarehe tofauti miaka mitatu baadae (19/06/2012, 7/08/2012, 10/08/2012 na 16/08/2012) kwa ajili ya kitabu cha wasifu wa Mwalimu Nyerere ambacho kinaandikwa na wanazuoni watatu*

## 19 Juni 2012

**IS:** Labda tungerudia kidogo tu. Ulizaliwa?

**KNM**: Nilizaliwa Kipatimu, wilayani Kilwa, mwaka 1932, tarehe 30 Mei. Baba yangu alikuwa mwalimu; siku zile walikuwa wanaita walimu wa *Grade II*.

**IS**: Katika shule ya msingi?

**KNM**: Shule ya msingi.

**IS**: Shule ilikuwa  ni ya serikali?

**KNM**: Hapana, shule ya misheni.

**IS**: Na mama?

**KNM**: Mama yangu mimi hakusoma. Tena wote wawili mwanzoni walikuwa Waislam, lakini baadaye baba mkubwa aliingia Ukristo, akamuingiza mdogo wake ambae ni baba yangu mimi. Na yeye katika kutafuta mchumba akampata mchumba ambaye ni Muislam, akamshawishi, walivyopendana, na yeye akaingia Ukristo. Kwa hiyo alikuwa mwalimu. Alisomea hapa Kigurunyembe, Morogoro, *late 1920s*.

**IS**: *1920s* kulikuwa na hiyo shule ya kufundisha walimu – ya Kigurunyembe?

**KNM**: Eee. Kigurunyembe.

**IS**: Kwa hiyo imeanza zamani?

**KNM**: Eee… ya Kanisa Katoliki. Sasa, lakini sikukulia Kipatimu, Kilwa. Mzee wangu, Mzee Ngombale, alikosana na wakubwa wake wa kanisa pale, akaacha kazi. Akaondoka mwaka 1936.

**IS**: Wewe ukiwa bado mdogo?

**KNM**: Eee.

**IS**: Kwa hiyo hukumbuki kabisa hali ya kijijini pale?

**KNM**: Aaa… lakini baadae nilirudi. Manake alitoka yeye baada ya kukosana nao, akaenda Utete, akafanya kazi kwa DC kama karani. Lakini askofu wa Dar es Salaam, ambae alikuwa ndio vilevile mkubwa wa kanisa la Kipatimu, alivyopata habari kwamba huyu mwalimu Morris Ngombale ameacha ualimu… na yeye alikuwa rafiki yake kwa sababu alimfundisha Morogoro, yule askofu kabla ya kupata uaskofu alikuwa mwalimu katika *Teacher Training College* ya Kigurunyembe. Basi akamfuata Utete, akazungumza na DC kumuomba 'Bwana mi namuhitaji mwalimu wangu'. Ndio baada ya baba kukubaliana na yule askofu akaja Dar es Salaam. Askofu akamchukua, akaja nae Dar es Salaam. Kwa hiyo alianza hapa kufundisha katika shule ya misheni.

**IS**: Hapa hapa Dar es Salaam?

**KNM**: Enh. Kwanza alifundisha vijijini huko, Uzaramo, katika kijiji kimoja karibu ya *Ruvu Station*. Halafu sisi tukaja mapema tukawa nae kabla hatujaanza shule; akatuleta Dar es Salaam tukaanza shule. Yeye akafundisha kule halafu akaacha, akaja kufundisha hapa hapa Dar es Salaam kwenye shule yetu – *primary school*. Ilikuwa moja tu ya Waafrika, Mchikichini. Kwa hiyo akawa mwalimu hapo Mchikichini mpaka mwaka 1945; akapata *transfer* kwenda Miono, Bagamoyo.

**IS**: Wewe uliingia shuleni ukiwa na miaka mingapi?

**KNM**: Oh mimi nilichelewa, niliingia shuleni, darasa la kwanza nikiwa na miaka kumi.

**IS**: Na hiyo shule ilikuwa inaitwaje?

**KNM:** Mchikichini Primary School… iko hapa nyuma ya kiwanda cha bia.

**IS**: Ndio, nimewahi kwenda pale.

**KNM**: Eee. Ndiyo shule yangu hiyo tangu darasa la kwanza mpaka la nne, wakati ule mwisho wake la nne. Baada ya pale mnafanya mtihani wa darasa la nne. Wale wanaofaulu – na ulikuwa mtihani wa *Eastern Province* yote – wanaofaulu wanakwenda barabara ya Mchwele pale, siku hizi wanaita Uhuru Mchanganyiko. Ile wakati wetu sisi ilikuwa inaitwa *African Central School* – darasa la tano mpaka la kumi. Kwa hiyo ndio nikaenda pale darasa la tano.

**IS**: Sasa mzee ulipoingia katika shule ya Mchikichini pale unakumbuka vizuri?

**KNM**: Nakumbuka sana.

**IS**: Na walimu walikuwa akina nani, unaweza ukakumbuka majina yao?

**KNM**: Eee. Mwalimu wetu mkuu alikuwa mzee Thomas Grantham, maarufu sana … Sasa walimu wengi nimewasahau. Na mmoja ninaemkumbuka sana ni mwalimu Ramadhani Kazimoto, alikuwa mmoja wa walimu wangu darasa la kwanza. Alikuwa machachari sana ndio maana namkumbuka sana. Lakini kuna mwalimu mwingine, Raphael Zayumba, namkumbuka. Marehemu wote, manake ni miaka mingi … Na mwalimu Joseph Bilali, alikuwa mwalimu wangu wa Kiingereza.

**IS**: Lugha ya *instruction* ilikuwa ni Kiswahili?

**KNM**: Kiswahili, halafu mwanzo wa Kiingereza – sisi tulianzia darasa la tatu Kiingereza. Lakini walikuwa mahodari; kwa mfano mwalimu huyo, Joseph Bilali alikuwa hodari sana. Kwa sababu darasa la tatu, la nne… la nne mimi na wenzangu tulikuwa tayari, tulikuwa tunafanya hata *debate* kidogo. Eee. Mwalimu wa Kiingereza anatoka kule *African Central School* anakuja kusimamia ka-*debate* ka Kiingereza. Kwa hiyo huyu alikuwa hodari.

**IS**: Na unaweza ukakumbuka wanafunzi wenzako ambao baadaye wakaja kuwa *prominent*?

**KNM**: Eee… Mmoja, kwanza yupo, marehemu sasa, alikuwa mwalimu Borilila. Yeye tulikuwa wote darasa la kwanza, tulikuwa tunashindana sana katika uwezo. Yeye, mzee wake alipata *transfer* nadhani kwenda Morogoro, kwa hiyo akaenda Morogoro akendelea kusoma huko. Tukaja kukutana darasa la tano, kwa sababu alipofika darasa la nne tukafanya mtihani wote; yeye kafanya kule tukakutana pale. Yeye tuliendelea wote mpaka Tabora *Standard Twelve*. Tukafanya *Cambridge Certificate* pamoja, yeye akaendelea kwenda Makerere. Baadaye akawa mwalimu wa sayansi mzuri sana, maarufu sana.

Yuko Juma Ali. Yeye tuliendelea wote; darasa la nne tukapasi wote tukaenda darasa la tano; darasa la kumi tukapasi wote tukaenda Tabora. Mwaka wetu sisi, wa darasa la kumi tulikuwa wanne kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora. Na ilionekana tuko wengi manake kwa kawaida Dar es Salaam ilikuwa haitoi watu wengi.

**IS**: Dar es Salaam ilikuwa haitoi watu wengi kwenda Tabora?

**KNM:** Eee haikupasi, eee. Haikuwa nzuri hata kidogo. Na ndio maana baada yetu sisi, miaka miwili baadaye Waingereza walihamisha shule, wakaihamishia Mzumbe. Kwa hiyo ile Mzumbe ilijengwa *in fact* kuchukua nafasi ya Dar es Salaam. Dar es Salaam ikafanywa *middle school*. Ile *secondary aspect* ikapelekwa Mzumbe.

**IS**: Na wakati ule ilikuwa ni *early 40s*? Kulikuwa na vuguvugu lolote la kisiasa hivi ..? Wewe kama mtoto unakumbuka nini?

**KNM:** Unajua kipindi kile, kwanza, kilikuwa kipindi cha vita, sehemu ya kwanza. Ilikuwa Vita Kuu ya Pili [ya Dunia]. Hilo tulikuwa tunalifuatilia kwa sababu ... na hapa Dar es Salaam kulikuwa na mazoezi ya kujiandaa kwa kujihami. Kwa hiyo mazoezi mpaka yanahusisha raia, wananchi wa kawaida. Sehemu kubwa ya Dar es Salaam kwa mfano, ilikuwa bado ni viunga vya

minazi na nini… Karibu kote kulichimbwa mahandaki na nini... Na tulikuwa tunaelezwa kwamba ikitokea matatizo, ilikuwa wakati ule inavumishwa kwamba – nadhani ni baada ya *Pearl Harbour*, nadhani – kwamba kuna uwezekano Wajapani wakaja wakapiga mabomu hapa na nini, wakashambulia. Kwa hiyo tulikuwa hata watoto tunaelezwa kwamba, 'Zikitokea ndege zinakuja kufanya fujo kimbilieni kwenye mahandaki'. Hilo moja, lakini baada ya 45, nakumbuka zaidi mgomo wa wafanyakazi, hasa makuli wa Bandarini. Hayo ni matukio katika miaka ya 40 ambayo tuliyaona na … kwamba kuna tafrani mitaani huko.

**IS:** Na wanafunzi mlichukuliaje kwa jumla? Wewe mwenyewe fikra zako?

**KNM**: Aaa… wakati ule bado tulikuwa… tulikuwa tunalichukulia tu kwamba… ah! wafanyakazi wanadai haki zao, kwamba hawa wazungu wanawapunja, wanawaonea. Na kulikuwa na watu waliokufa kule. Kwa hiyo watu walikuwa wanazungumza mtaani. Kwa hiyo msuguano huo naukumbuka.

**IS**: Na katika maeneo ya Dar es Salaam, suala zima la utawala na ubaguzi unakumbuka nini kama mtoto? Wewe ulikuwa unaishi wapi? Wanafunzi wengi walikuwa wanaishi wapi?

**KNM**: Sasa shule yetu ilikuwa… sasa ile ya sekondari… ya *primary* ilikuwa *day* kabisa… ile *African Central School* ilikuwa ya mchanganyiko, wengine walikuwa *day*, wengine walikuwa *boarding*. Sisi tulikuwa *day*, lakini wengine walikuwa *boarding* kwa sababu ilikuwa inachukua vijana wa *Eastern Province* nzima, yaani mkoa wa Mashariki ambao kwa sasa hivi ni pamoja na Morogoro yote, mkoa wa Pwani wote, wa Dar es Salaam wote, na kwa kweli walikuwa wanachukua vilevile sehemu kubwa ya Lindi. Ndio maana mzee Kawawa alikuja kusoma Dar es Salaam hapa *African Central School*. Alikuja mwaka 42 lakini alitokea…

**IS**: Kwa hiyo yeye alitangulia?

**KNM**: Eee, yeye anaingia darasa la tano, mimi naingia la kwanza – Mchikichini. Lakini nilikuwa simfahamu lakini sasa hivi katika

*records*… manake baadaye *of course* nilikutana nae, naingia darasa la tano, yeye yuko la tisa.

**IS**: Wewe unakumbuka ulikutana nae?

**KNM**: Eee. Na alikuwa *prefect* wangu, *house prefect*. Kwa hiyo tulifahamiana. Alikuwa *prefect* la tisa, la kumi. Mwaka wao hao walipasi wawili, yeye na mwenzake mmoja, kwenda Tabora.

**IS**: Na mzee Kawawa pia aliwahi kwenda Tabora?

**KNM**: Alikwenda Tabora, eee. Alikwenda kule, alifanya *Cambridge School Certificate* akapasi.

**IS**: Na wengine nani unawakumbuka kutoka *Central School*?

**KNM**: Kutoka *Central School* unajua ni wengi sana kwa sababu wengine walikuwa mbele lakini wakawa maarufu baadaye, kwa mfano marehemu Zuberi Mtemvu, alikuwa mbele yangu karibu miaka mitatu… *no,* minne; marehemu Hamza Azizi, alikuwa IGP wa zamani, nae alikuwa mbele yangu vile vile…

**IS**: Na ilikuwa ni ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana?

**KNM**: Hapana, ilikuwa ni wavulana watupu. Wasichana wa Kiafrika, manake wakati ule shule zilikuwa za ubaguzi, walikuwa pale Msimbazi na Uhuru, kona pale. Lakini sasa pale walikuwa wanasoma darasa la kwanza mpaka la sita. Isipokuwa, baadaye ikatokea sasa msichana mmoja akaonyesha akili kali sana, kwa hiyo iliwalazimisha Waingereza wampatie nafasi. Sasa, nafasi Dar es Salaam ilikuwa haipo ya wasichana kuendelea, akaletwa kwa wavulana. Kwa hiyo akaletwa darasa la saba, *Central School*.

**IS**: Peke yake?

**KNM:** Eee, mwanamke peke yake; marehemu Tatu Nuru. Alikuwa na akili nzuri sana. Kwa hiyo alikuwa anakuja. Alisoma pale. *Of course* alikuwa wakati ule anakuja kutoka nyumbani amevaa baibui, akifika mlangoni pale anavua baibui, anabakiwa na *uniform* za shule. Akitoka shule anavaa baibui yake ndio anapita mitaani.

**IS**: Kwa hiyo kulikuwa na watoto wa Kiislam pia katika shule?

**KNM**: Ndio walio wengi.

**IS**: Ndio walio wengi *Central School*?

**KNM**: *Central School*, ndio. Walio wengi walikuwa ni Waislam kwa sababu, kwa Dar es Salaam, walio wengi walikuwa Waislam. Ukichukua watu wa *Eastern Province* wengi ni Waislam kwa hiyo mimi nimesoma katika shule ambazo, kwa Dar es Salaam shule zetu toka *primary*, Waislam ndio walikuwa wengi.

**IS**: Sasa tuseme ukiwa *Central School*, kabla ya kwenda Tabora, uliwahi kusikia jina la Mwalimu Nyerere?

**KNM**: Hapana kabisa.

**IS**: Na mliwahi kusikia kuhusu chama cha *African Association*?

**KNM**: Ndiyo. Miaka ya mwisho wakati tunafika kwenda la kumi… aah! sasa wakati huo na sisi tulikuwa tunakomaa hata katika kuelewa mambo ya siasa. Kwa hiyo, tulikuwa tunajua kwamba kuna Chama cha Waafrika kinaitwa TAA; hatukujua undani wake, lakini tulijua… kwa mfano mzee John Rupia tulikuwa tumnajua, mzee wa *Mission Quarter* pale. Na mimi nilikulia *Mission Quarter* kwa hiyo tulikuwa tunajua mzee John Rupia ni katika viongozi wa TAA. Na hata wakati fulani walikuja watu kutoka Afrika ya Magharibi, Waafrika, watu walisimka kidogo; kina mzee John ndio waliokutana nao. Lakini lililokuja kujitokeza likafanya watu washtuke kidogo, kwa sababu ni Waafrika – weusi, sasa watu waliambiwa: ‘Hawa jamaa ndugu zetu hawa wametoka Afrika ya Magharibi.’ Wakati ule nadhani walikuwa wanatoka *Gold Coast*, Ghana ya sasa; wamevaa nguo zao zile za nyumbani. Sasa Waswahili wanajua hawa Waafrika wanajua Kiswahili tu, kwa hiyo wakaanza kuwasalimu kwa Kiswahili; wale jamaa wameshindwa kujibu, wanajibu Kiingereza. Sasa hilo likawa ndio mazungumzo mjini: ‘Si alisema bwana, wale watu hawajui Kiswahili?’; ‘Itawezekanaje, Mwafrika hajui Kiswahili?’ Watu wanaona ajabu kweli kwamba kuna

Waafrika hawajui Kiswahili. Kwa hiyo tulijua wakati ule kwamba ipo TAA, lakini wengine tulishaanza kujua mambo ya dunia vilevile.

**IS**: Hasa nini ambacho unakumbuka vizuri kama mtoto, ambacho kiliku-*strike*?

**KNM**: Kwanza vuguvugu la Kenya – wananchi wanadai ardhi yao – lililoingia mpaka kwenye vita ya MauMau. Lilianzia wakati ule sisi tuko darasa la tisa na la kumi katika kipindi kile.

**IS**: Kwa hiyo mlikuwa mnasikia kwenye redio?

**KNM**: Kwenye redio na kwenye magazeti.

**IS:** Gazeti gani la Kiswahili lilikuwa linasomwa wakati ule?

**KNM**: Kulikuwa na *Ngurumo*; kulikuwa vilevile na *Mamboleo*. *Mamboleo* lilikuwa la serikali, lakini *Ngurumo* lilikuwa *private*.

**IS**: *But* wanafunzi walikuwa wanalisoma hilo?

**KNM**: Eee na wananchi kwa jumla. *Mamboleo* lilikuwa gazeti la propaganda. Kwa hiyo walikuwa wanatoa bure, [limeandikwa] 'Ukisoma mpe mwenzako'. Kwa hiyo watu walikuwa wanafuatilia. Na sisi tulikuwa tunajua mambo ya kule lakini tulikuwa tunajua hata vita ya Korea tulikuwa tunafuatilia.

**IS:** Vita ya Korea, baada ya mapinduzi ya China?

**KNM**: Eee. Nakumbuka wakati huo nilikuwa darasa la kumi mwaka 51. Tulijadiliana darasani. Kulikuwa na mwalimu ambae Waingereza walikuwa hawampendi, wana mashaka nae kwamba ni mtu wa mrengo wa kushoto na anahoji ukoloni – mwalimu wetu wa *history*.

**IS:** Unaweza kukumbuka jina lake?

**KNM**: Eee, ndio. Mwalimu Steven…Steven Mhando.

**IS**: Aaah! Ambae baadaye alikuja kuwa…

**KNM**: *Foreign Minister*, waziri wa mambo ya nje. Yule alitusaidia sana, manake katika *history*, aliifanya ikawa na maana zaidi ya historia; akaipa maudhui ya kisiasa. Na kulikuwa na wakati anatufundisha kwa mfano *industrial revolution*, anafundisha halafu akimaliza anasema, 'Sikilizeni haya niliyokufundisheni, haya ndio ya kwenye mtihani. Mje mjibu hivyo. Lakini sasa nataka kukwambieni ukweli. Kesho asubuhi ntakuja kukuelezeni'. Sasa anakuja pale anamwambia kijana mmoja apande asimame kwenye *desk* atazame dirishani, na mwingine apande kwenye desk atazame dirishani upande wa pili wa chumba; manake walikuwa wanamwekea shushushu wa kutaka kujua anasema nini. Kwa hiyo anasema, 'Ninyi tazameni kama kuna watu wanazungukazuguka huko'. Sasa yeye huku anaanza kutueleza juu ya ukoloni na ubeberu, na kwamba hawa wamekuja hasa kufuata nini.

**IS**: Na vijana walichukuliaje?

**KNM**: Ee! Sasa ndio akawa anatuamsha. Hilo darasa tukawa tunalipenda kweli, tunasubiri atupe vipande namna hiyo. Anasema, 'kwa nini wamekuja hawa?' Anatueleza, anatueleza; anatupa mifano ya Afrika Kusini anasema: 'Tazama wamekwenda kule wamewadanganya watu washike biblia, wameshika biblia wanasali wao wamechukua ardhi yao yote, kuja kuamka nchi imekwenda!'

**IS**: Na hiyo ulisikia mara ya kwanza kutoka kwa mwalimu Steven?

**KNM**: (Kicheko) ee, mwalimu Steven Mhando. Basi, kwa hiyo miaka ile miwili, darasa la tisa na la kumi, mimi ilinisaidia sana kupata mwamko.

**IS**: Na hasa kwa mwalimu Steven?

**KNM**: Ehee. Huyo alikuja kuniongezea sana lakini nilikuwa na mwamko wangu na mimi huko. Nahojihoji mambo mengi tu, nilishaanza kuhojihoji mambo mengi.

**IS**: Hasa ulikuwa unasoma nini wewe nje ya mambo ya darasa?

**KNM**: Aaah, hapana. Hatukuwa na facilities kubwa za vitabu. Mimi vitabu, *of course* nilikuwa nasoma kitabu chochote ninachokipata, lakini nilipotafuta sana vitabu Tabora kwa sababu tulikuwa angalau na *library*. Hapa hatukuwa na *library*, lakini Tabora tulikuwa na *library*. Na wakati ule mimi sasa suala la ukoloni limeshanichosha, na fikra zangu zilikuwa ni suala la kupambana na ukoloni. Lakini sasa nilikuwa natafuta maarifa, kwa hiyo nilikuwa natumia muda mwingi sana *library* kutafuta vitabu, vitabu gani vinaweza kuniongezea maarifa? Basi nakwenda kutafuta vitabu vya *political science*, lakini unakuta *Introduction to Political Science* na vitu kama hivyo. Mimi Tabora nilisoma kwa kuhangaika tu. Hata [Albert] Einstein nilimsoma [nikiwa] Tabora katika vitabu vile nilivyokuta *library*, *theory* yake *on relativity*, nasoma nasoma, najaribu kuelewa hivi anasema nini huyu?

**IS**: Hiyo ilikuwa mwaka gani?

**KMM**: 1952 na 1953 ndio nilikuwa *eleven and twelve.* Nilisoma wengi tu, nimemsoma Jodd[?], nimemsoma [Sigmund] Freud … Nilikuwa natafuta tu, na *in fact* pale Tabora, sio mimi tu, lakini baadhi ya wanafunzi walikuwa na mwamko mkubwa wa kisiasa, na wakati ule ndio mapambano nchini Kenya, ya Mau Mau yamepamba moto sana. Waingereza wakaamua kuja ku-*check* kwenye *library* kwa kufikiria kuna vitabu mle ambavyo vina uchochezi. Na walichukua baadhi ya vitabu ambavyo havina lolote, mimi niliviona havina mambo. Lakini *Provincial Education Officer* ndiye alikuja, walichukua vitabu pale.

**IS**: Wakati wewe ukiwa Tabora, mwalimu mkuu alikuwa nani?

**KNM**: Mr. [John] Crabbe.

**IS:** Unaweza kunielezea jinsi Tabora ilivyokuwa *organised* na mlikuwa mnafanya nini, taratibu zake… *system* yake?

**KNM**: Mi nadhani ilikuwa sekondari tu ya kawaida. Lakini waliijenga kwa lengo la kuandaa watu wenye kasumba ya ubora. Kwa sababu hata wakazua na wimbo pale, tuliukuta: '*Tabora School, Kichwa cha Tanganyika'*. Manake ni kuwajenga tu wale wanafunzi ili wajione kwamba wao wanaandaliwa kuongoza nchi. Watu bora!

Lakini walikuwa na mazingira mazuri ya kusoma; walikuwa na walimu wazuri, wote mchanganyiko – Wazungu wenyewe Waingereza na walimu Watanzania. Na palikuwa vilevile na nidhamu – nidhamu kali kidogo. Lakini vilevile walikuwa wana-*combine* masomo na burudani; wali-*organise* vizuri, pamoja na michezo. Headmaster mwenyewe, Mr. Crabbe, alikuwa anasimamia mpira, halafu anasimamia *athletics* na nini. Kwa hiyo, walikuwa na utaratibu wa *training* ambao ni mzuri katika maana kwamba unazingatia mambo yote yanayohitajika: upande wa taaluma – hiyo ilikuwa kali, lakini vilevile burudani na mambo mengine yote yenye maslahi ya *development* ya vijana.

**IS**: Kulikuwa na ubaguzi wa aina yoyote pale?

**KNM**: Hapana. Manake kwanza kwenda pale Tabora wakati ule pale *eleven* na *twelve* kwa sababu shule za sekondari – *junior secondary* – mwisho darasa la kumi - zilikuwa chache: Dar es Salaam, Tanga, Moshi, nadhani Bwiru, Kagera, Iringa, na Mpwapwa nadhani, ah  na Dodoma. Halafu wote ndio wanapeleka vijana wao pale, Tabora, lakini kwa msingi wa *academic performance*. Na ulikuwa mchanganyiko mzuri: watu wanachanganyika, tulikuwa hatujuani. Wengine tulikuwa *narrow*, mtazamo wetu finyu, hatuwajui watu wala hatujui makabila. Ma'ke we umekulia Dar es Salaam hapa, wewe unajua wote wenzako tu basi. Kule sasa ndio unakuta makabila: hawa unaambiwa Wachagga, hawa Wahaya, hawa Wasukuma. Lakini kulikuwa hakuna ubaguzi. Mimi sikuona wala sikuwahi ku-*notice* hata kidogo. Kote mnakochanganyika mnakwenda vizuri.

**IS**: Na ulipoenda Tabora, uliwahi kusikia tena jina la Nyerere, kwamba alipitia Tabora au kitu kama hicho?

**KNM**: A-a. Mimi ninavyokumbuka… hapana. Mimi binafsi sikuwahi [kusikia jina la Nyerere] Tabora. Mimi Mwalimu nimekuja kumfahamu alipounda TANU. Eee. Imeundwa TANU, tukapata habari.

**IS**: Wewe ukiwa wapi?

**KNM**: Sasa nilipomaliza Tabora, mimi nilikuwa nimepanga nisiende Makerere; mimi nilipanga kwenda India. Nilitaka kuchukua sheria. Sheria na *journalism* ndio vilikuwa … [chaguo langu]. Na niliamua hivyo kwa sababu, sijui nilikutana na nani aliniambia: 'Bwana, ukitaka kupambana na Waingereza, sheria! Wenzetu wa Gold Coast na Nigeria wanawaweza Waingereza kwa sababu wanajua sheria.' Na mimi nikasema, 'Basi na mie nitachukua sheria na *journalism'*. Kwa hiyo nikachukua *direct employment* baada ya kufanya *Cambridge School Certificate* nikawa karani hapa, 1954.

**IS**: Ukawa karani wa …?

**KNM**: Karani *PWD*, *Public Works Department*. Unapangiwa, manake siku zile mnapangiwa moja kwa moja na serikali. Basi, mwezi Mei 1954 nimefanya *interview* ya kwenda India. Alikuja *Indian High Commissioner* hapa. Alikuwa *based* Nairobi, akaja hapa kuongoza kamati yake ya *interview*. Kwa hiyo nikafanya interview, nikaambiwa majibu baadaye.

**IS**: Na serikali ya wakoloni ilikuwa ikiwaruhusu Waafrika kwenda India kusoma?

**KNM**: Ndio. Na tena tulifanya *interview* kwenye *department of education*. Pale mbele ya Kirimanjaro Hotel ndio kulikuwa na jengo pale la *department of education*.

**IS**: Mlikuwa wangapi, unaweza kukumbuka?

**KNM**: Aah! Siwezi, kwa sababu watu walioomba hatukuwa wengi niliowaona pale lakini huwezi kujua. Sasa ndio mwezi Julai tarehe 7 [1954] TANU ikaundwa. Ndio tukapata habari. Sasa baada ya kuanza kazi kule PWD mwezi Januari mwaka

1954. Nadhani mwezi wa pili hivi nikakutana na Mzee Ali Sykes. Akaniambia: ‘We bwana, we si umeshamaliza masomo?’ Nikamwambia: ‘Ndiyo’. ‘Uko wapi?’ Nikamwambia niko PWD nimeanza kazi …

**IS**: Mlikutana ghafla tu?

**KNM**: Hatukukutana kwa bahati tu, lakini kwa sababu namfahamu – yule kaka yetu wa hapa mjini. Akaniambia: ‘Sasa wewe bwana nataka tukutane Arnatouglo,’ alisema, ‘Jumamosi tuna mkutano. Nataka uje.’ ‘Mkutano gani?’ ‘Nataka uje bwana ntakueleza’. Basi nikenda, saa kumi. Akaniambia: ‘Bwana, hapa tuna *Tanganyika African Government Servants Association (TAGSA)*, chama chetu wafanyakazi wa Kiafrika, cha wafanyakazi, kudai haki zetu.’ Akasema, ‘We bwana napenda, unafaa, wewe uingie kwenye Kamati yetu ya Taifa kwa sababu wewe PWD ni eneo la muhimu sana. Kwa hiyo nakupendekeza kwenye Kamati’. Yeye alikuwa ndiye katibu mkuu wa ile TAGSA. Na rais alikuwa ni Mzee Kawawa; yeye lakini wakati huo alikuwa hayupo. Alipelekwa *transfer* nadhani Urambo ama Handeni. Nikamwambia, ‘Basi, maadamu wewe kaka unasema ninafaa…’ Akasema: ‘Bwana wewe unafaa bwana, twende!’ Basi akaenda kwenye kikao, akazungumza nao wenzake, wakanikaribisha. Wakanambia, ‘Bwana sisi tumeona uwe mjumbe wa Kamati ya Taifa’. Kwa hiyo nikawa mjumbe wa kamati hiyo ya TAGSA.

Sasa TANU ilipoanzishwa, na kwa kuwa Mzee Ali Sykes alikuwa mmoja wa waanzilishi, na sisi tulijua kwamba baada ya kuanzishwa yeye ndiye alikuwa *active* katika kutekeleza yale maamuzi ya uanzilishi, tukamwomba aitishe kikao cha TAGSA, ile Kamati, aje kutueleza ujio wa TANU, chama kipya. Aaa, yeye alikuwa *sharp* sana. Akapanga mkutano, akaitisha, tukakutana. Na wakati ule akaja kamili kwa sababu yeye ndiye alikuwa anachapisha kadi za kwanza za TANU na alikuja nazo. Kwa hiyo mimi ndio nikajiunga pale, nikajiunga na akanipa kadi mia moja za kwenda kuanza kazi ya *recruitment*. Kwa hiyo baada ya pale

majibu yakaja, ya India, kwamba nimekubaliwa kwenda India. Sijui nilikuwa niende Agra? Nikasema, ‘Sasa ninakwendaje huko na hapa tumeanza harakati nilikuwa nazitafuta za kupambana na wakoloni sasa nikimbie niende huko…’ Nikasema, ‘Hapana. Kusoma nita-*postpone*’ lakini hii ya kupigania uhuru siwezi ku-*postpone’*. Kwa hiyo nikaacha habari ya kwenda India, nikabaki *activist*. Sasa ndio nasema kuanzia pale nikamfahamu Mwalimu.

**IS**: Kwanza kusikia jina lake?

**KNM**: Kwanza walipoanzisha tukapata jina, kwamba yeye ndiye rais na ndiye mwalimu wa Pugu sekondari, nikasema ahaa. Basi mimi nikaanza tabia: nikitoka kazini saa kumi unusu – siku zile tunakwenda kwa baiskeli – nakwenda ofisini, siku hizi wanaita Lumumba, zamani ilikuwa *New Street*. Nakwenda pale makao makuu…

**IS**: Bado ukaendelea na kazi yako ya PWD?

**KNM**: Eee, naendelea na kazi yangu ya ukarani.

**IS**: Lakini hao waajiriwa wa serikali walikuwa hawaruhusiwi ku… [kujihusisha na siasa?]

**KNM**: Mwanzo Waingereza walikuwa *taken unawares*, kwa hiyo tuliingia. Tuliingia. Baadaye wakatuitisha *secretly* kwamba *surbordinate staff* tu ndio wanaoruhusiwa, *above that* marufuku. Mimi aliniita bwana mkubwa mwenyewe, *director*, ananiambia: ‘Wewe, *I have been informed that you are either an agent of TANU or a full member of TANU*. Tell me what you are!’ Nikamwambia: ‘*I am neither*’. Nikambabaisha tu, nikamwambia sio *member*. Akasema, ‘No! *What are these people talking about*?’ Basi, mwisho akaniachia. Lakini mimi nikawatazama tu, nikawa naendelea na kazi yangu ya *ku-recruit*, nika-*recruit* wote kwenye jumuiya yetu kwa sababu kule kulikuwa kuna wafanyakazi wengi kweli wa kawaida – madereva, manake *division* ya *engineering* ndiyo ilikuwa inahusika na *Coast Region* yote katika mambo ya barabara na *construction*, mambo ya *furniture* na nini, zote zilikuwa huko huko, eneo hilo hilo la

kwetu. Kulikuwa na watu zaidi ya mia nane sijui, wanaofanya kazi pale – wote wale rafiki zangu.

Wale Wazungu wakiondoka na Wahindi – tulikua na Wagoa – na *hief clerk* wetu alikua ni Goa, mzee mzuri sana, Mr. Demelo. Wakiondoka mimi mwenzao nimeshawaambia Waswahili: 'Subirini, subirini, ngoja waondoke wote'. Wakiondoka, mimi nafanya mkutano. Siku moja mzee Demelo, sijui aliambiwa na nani, akajitia ameondoka na baiskeli yake halafu akarudi. Akanikuta mimi nipo kwenye mkutano wa hadhara. Hakuniuliza kitu, na mimi wala sikujali, nikafanya kama sikumuona, nikaendelea tu. Siku ya pili akaniita akaniambia, '*Mr. Ngombale, you are getting into trouble, you don't know these people, the British. Ask us, we know them. They can destroy your future these people. Why are you holding mass rallies like that so openly*?' Nikamwambia: '*I was just informing them, you know, about certain things'.* Akasema, *'No no no. Don't do that. You are too young*'.

**IS**: Kwa hiyo kila jioni ulikuwa unakwenda ofisi ya TANU. Enhe?

**KNM**: Eee, na jambo moja zuri pale vilevile ni kwamba tulikuwa tunaletewa magazeti kutoka *Gold Cost*. Walikuwa na propaganda, akina Nkrumah, walikuwa na propaganda kali sana. Wanatuletea magazeti yao ya kuonyesha jinsi wanavyopambana kule. Basi tukifika pale jioni, kama hakuna kitu cha kusaidia pale ofisini, tunasoma propaganda za *Gold Cost*, jinsi wanavyoendelea na mapambano yao ya uhuru. Wenzetu walikuwa *more advanced*. Kwa hiyo inatupa *inspiration* kubwa. Na Mwalimu akiwepo pale wakati mwingine tunaomba kumwona, kama tuna masuali tunamuuliza; na alikuwa na tabia mwanzoni, Jumapili kama yupo Dar es Salaam Anatouglu pale, akitoka kanisani tu anakuja anafanya mkutano wa ndani. Basi vijana tunajaa mle ndani tunamsikiliza.

**IS**: Hebu nieleze mkutano wa kwanza kabisa ulipokutana na Mwalimu kama ukiweza ku-*visualise*.

**KNM**: Ilikuwa pale Arnatouglo, baada ya ule mkutano tulimsogelea, tulimfuata kule mbele mimi na wengine wengi. Tulikwenda pale kumwamkia na kumpa mkono. Anakuuliza: 'Wewe unatoka wapi? Wewe uko wapi? Wewe unafanya nini?' Basi, anazungumza, [kisha] tunaondoka. Baadaye [nilikutana nae] pale ofisini. Kulikuwa na *issue*, ilileta kidogo maneno: Mwalimu alialikwa kwenye hafla ya, nadhani ya *High Commissioner* wa India. Sasa kule alitoa hotuba.

**IS**: Pale *High Commissioner* wa India?

**KNM**: Eee. Manake alikuwa anatembelea *East Africa*, *base* yake ilikuwa Nairobi. Alipokuwa hapa, Mwalimu alialikwa. Basi, akatoa hotuba. Sasa, kilichowasisimua watu, katika hotuba yake Mwalimu akasema yeye hatajali kama katika Tanzania inayojitawala Waziri Mkuu akiwa Muasia ama Mzungu. Yeye hatajali kwa sababu ni uamuzi wa watu. Sasa, ilipoandikwa ile …

**IS**: Hiyo ilikuwa ni mwaka gani?

**KNM**: Nadhani ni mwaka 1955 kama sio 1954 mwishoni. Sasa ilipoandikwa ile kwenye magazeti watu wakasema, Waswahili wakasema, ile 'sitajali kama Muasia ama Mzungu anakuwa Waziri Mkuu wa Tanganyika inayojitawala.' Watu wakaanza kuulizana: 'Sasa huyu bwana anaonaje, yeye hajali vipi? Kwani tunapigania uhuru ili iweje? Tena aje tena Mzungu, aje Muasia kuwa Waziri Mkuu? Itawezekana wapi?' Sasa ikawa imeleta maneno mitaani. Na wakati ule Waswahili, unajua, walikuwa makini sana. Wengine [walikuwa] hawajui kusoma gazeti, lakini kama ameona kama kuna picha, ama ameambiwa kumeandikwa maneno ya Kenyatta ama ya Nyerere atakaa nje pale, anamtafuta kijana anayeonekana kasoma atamwita: 'Kijana, njoo. Hebu nisomee hapa, wamesema nini hapa?' Mimi nilikwishaitwa mara mbili tatu, barabarani tu mitaani, umsomee. Sasa hili ni moja katika mambo watu wali-*take interest*: 'Kwa nini Mwalimu Nyerere anasema hivi?' Ikawa ni *issue*.

Na sisi baadhi yetu tukawa tunapigiana simu, simu za kazini zile, unamwambia mwenzako: ‘Bwana eee leo tukienda kule tumuulize kwa nini amesema hii *statement*?’ Basi tukaenda. Tulipofika pale ofisini, bahati nzuri tukamkuta. Tukamwambia karani mmoja, alikuwa anaitwa Julius, namkumbuka sana, amwambie Mwalimu Nyerere tunaomba kumwona. Basi kwa sababu yule karani naye alikuwa kijana anajua tulikuwa tunazungumza nini akawa amem-*brief*. Basi, Mwalimu akatoka.

**IS**: Wakati ule Mwalimu bado alikuwa anavaa kaptura?

**KNM**: Ee, alianza na kaptura, baadaye, sasa maneno yanasema, wazee walimshauri avae suruali. Lakini kwa muda mrefu alikuwa anavaa kaptura. Basi akatoka: ‘Ee, vijana mnasemaje? Njooni, mko wangapi? Muingie ofisini hapa.’ Akatuona kumbe tuko wengi karibu kumi akasema: ‘Basi kumbe hamwezi kukaa ofisini hapa.’ Basi akatuambia: ‘Enhee, nasikia mna suali.’ Tukamwambia ‘Ndiyo.’ Tukamweleza: ‘Watu wanashangaa umesema hivi. Sasa watu wanataka maelezo.’ Basi akatupiga *lecture* pale – *lecture* nzuuri *on democracy*. Nzuri, fupi, lakini *very clear*. Halafu akahoji: ‘Hivi haya mapambano yetu tunayofanya tunafanya nini? Kwanza nyie mnajua katiba yetu tumeandika nini: Tunapiga vita ubaguzi – ubaguzi wa rangi, wa kikabila, wa kidini, sawasawa?’ ‘Sawa’.

‘Sasa lakini sisi viongozi wetu katika TANU tunachaguana kwa kura. Na katika nchi tutaweka utaratibu wa kupiga kura, kuchaguana kwa kura, tujue watu wanampenda nani ashike madaraka haya, madaraka haya, n.k. Sawasawa?’ ‘Sawa’. ‘Sasa katika nchi hii tuko sisi Waafrika – watu weusi. Lakini tunao wenzetu wenye asili ya Asia, na kuna wengine hapa wa asili ya Ulaya. Sasa watashiriki katika mchakato. Kwanza, katika kudai uhuru; baadhi yao wameshajitokeza wanatuuunga mkono, na tunapigana pamoja. Kwa hiyo, katika harakati za kushika maradaka tutakuwa wote. Sasa tunapofanya uchaguzi, wapiga kura ni wananchi, na katika demokrasia wengi wape. Sasa kama katika kura hizo aliyepata kura nyingi ni Muasia, sasa nyinyi

mnasemaje, mnasema mtakataa? Mnakataa kwa niaba ya nani nyinyi? Kwa sababu waliopiga kura, kama mnasema Waafrika, walio wengi ni Waafrika. Na umesema wengi wape. Sasa nyinyi mnasema: 'Lakini haiwezekani.' Haiwezekani kwa sababu gani? Huyo Mwafrika mweusi mliomuweka hakupata kura, maana yake walio wengi hawamtaki! Sasa ninyi mnataka mlazimishe?'

Basi akatupiga pale, akatupiga, [*lecture*] tena yeye hodari wa kueleza. Tukasema: 'Sisi mbona tuko naye, kumbe hatukuelewa tu.' Kwa sababu na sisi tuliodai tumesomasoma tulikuwa hatukuelewa, alikuwa na maana gani. Ndio kwa kweli nikaanza kuwa na *interest* zaidi na Mwalimu kwamba huyu bwana hodari sana wa kufikiri huyu. Na ndio kutoka hapo nikawa nakuwa na *confidence* zaidi juu yake kwamba huyu ni mtu wa kumtegemea kweli.

Baada ya pale ilikuwa ni *process* kwa sababu baada ya pale mimi niliacha ukarani, nilijiuzulu. Nilizungumza nae Mwalimu nikamwambia mimi naacha, manake Mwalimu alitoa wito: 'Vijana mliosoma njooni tusaidiane kumwondoa mkoloni huyu'. Kwa hiyo nikaamua kuacha. Nikaacha kazi ili nifanye kazi *full time* kwenye Chama. *Of course*, nilipata matatizo kidogo na mzee wangu, hatukuelewana, na mimi nilijua kwamba tusingeelewana. Kwa hiyo, nilijiuzulu kwanza halafu ndio nikamwarifu kwa sababu ningekwenda kumwomba ruhusa, angekataa. Manake yeye alikuwa, kujiunga na TANU alijua nilijiunga, alikuwa akasema: '*Fine, very good*!', Lakini kuacha kazi? Ee! Lakini nikamwachia mama yangu ndiye aliweza ku-*deal* nae. Aliniambia, 'Mwache kwanza wewe. Msigombane'. Manake alikasirika kweli. Mamangu akaniambia, 'Basi wewe tulia. Mimi nita-*deal* na baba ako. Atakubali tu, hawezi kukataa'. Lakini *it took us six months*; wanajadiliana, wanabishana wakati mwingine. Na mimi siku-*join* moja kwa moja Chama; sikwenda kuripoti kwa Mwalimu kwa sababu ingekuwa sasa namdharau Mzee.

Kwa hiyo nikawa na-*hang around* kidogo lakini nafanya kazi za Chama, lakini *on a voluntary basis*. Na mimi ili nisiishi ….

manake nilikuwa sina pesa pale za kuji-*sustain* kwa miezi sita, kwa hiyo zile pesa nilizokuwa nazo nilikuwa na rafiki yangu mmoja mwalimu nikamwambia tufanye biashara. Tukaanza kuuza nyanya sisi. Tukaenda Morogoro, tulikuwa na marafiki pale, tunanunua nyanya mnadani tunasafirisha, tunakuja nazo hapa, Kariakoo, tunaziuza. Tunapata faida, faida kubwa tu, kwa hiyo inatu-*sustain*. Zikitaka kuisha zile pesa tunakwenda tena tunanunua tunakuja tunauza. Nilifanya hivyo. Hata Dodoma nilikwenda kununua nyanya. Wale wafanyabiashara wa nyanya waliniogopa mwanzoni, walifikiria ni *CID* kwa sababu nilikuwa nakwenda kwa treni. Sasa katika treni mle mimi lazima nitakuwa na kitabu changu nasoma. Ah! Sasa walikuwa hawaelewi: 'Huyu kijana namna gani? Anaonekana kasoma lakini anafanya biashara ya nyanya. Mnh! Si kweli.'

Ilikuwa mwaka '56 hiyo. Sasa pale Dodoma kukawa, safari hiyo ika-*coincide*, kulikuwa na mkutano. Mwalimu anatoka Arusha kuja Dodoma, mimi hapa wakaniomba nisaidie Dodoma pale ku-*organise* mkutano. Sasa pale kwenye mkutano ni lazima utaonekana; wafanya biashara ndio wanasiasa wa kwanza, wadogowadogo wale. Eee, ndio *supporters* wa TANU. Ah! Sasa wakaniona kule, niko kule mbele napangapanga mambo. Ala! Ndio wakanigundua. Sasa tulipokutana tena kwenye treni, kwa sababu na wao walikuwa wanachukua mizigo yao kwenye treni, wakanifuata. Wakaniambia: 'Wewe tulikuwa tunakuogopa kweli wewe. Tulikuwa tunadhania CID, kumbe wewe mwenzetu wewe.' Nikawaambia: 'Mwenzenu vipi?' 'Ah! Wewe mtu wa TANU wewe. Si ulikuwa kule na Mwalimu?' Nikasema, 'Eee sawa. Kama nyie watu wa TANU basi kwa hiyo mimi mwenzenu.'

**IS**: Lakini wakati ule watu wakizungumza kuhusu Mwalimu wanamtajaje? Kama rais wa TANU au mwenyekiti au mheshimiwa?

**KNM**: Kwanza walianza 'mwalimu', mwalimu, Mwalimu Nyerere.

**IS**: Kwa sababu Mwalimu alikuwa mwalimu?

**KNM**: Ehee. Lakini baadaye ikaja wanasema 'mheshimiwa,' enh, ingawa wakoloni hawakuipenda. Katika wale rafiki zangu niliosoma nao mpaka Tabora, toka hapo, Juma Ali yeye baada ya *Cambridge* alifanya *journalism* lakini gazeti la serikali. Sasa wananchi wanamwita Mwalimu 'mheshimiwa', yeye akamwandika mheshimiwa kwenye gazeti. Eh! *He wastaken to task*! Enh. Aliitwa, alipata taabu kweli! Bado kidogo afukuzwe kazi. Waliogopa tu wakoloni inaweza kuwa*damage* wao.

Kwa hiyo baada ya muda mzee tukaelewana kwa hiyo nikaja kuanza kazi *full time* kwenye Chama makao makuu hapo.

**IS**: Na wakati ule katika makao makuu alikuwa nani mwingine kiongozi?

**KNM**: Pale alikuwepo… *acting* katibu mkuu alikuwa *the late* Elias Kisenge. Kulikuwa na mweka hazina Mzee Idd Faiz, mzee mmoja alikuwa ni *retired old man*, mtu mzuri sana. Walikuwepo Mzee Zuberi Mtemvu, alikuwa ni mmoja wa makatibu wasaidizi; Mbuta Milando alikuwa mmoja wapo. Hapakuwa na watu wengi – walikuwa wachache tu. Isipokuwa sasa, baadaye kwa sababu 1958, tulipofanya mkutano mkuu wa Tabora, pale Chama tulijiimarisha zaidi pale; ndiyo baadhi ya wajumbe wakateuliwa kuja ku-*man positions* makao makuu.

**IS**: Na wewe ulienda kwenye mkutano wa Tabora?

**KNM**: Ee. Kutoka Rufiji. Nilikwenda na *delegation* yangu ya Rufiji. Manake nimekaa makao makuu halafu Mwalimu akanipeleka Rufiji kuanzisha wilaya ya Chama. Kwa sababu kabla ya wakati huo Rufiji kulikuwa na – tulikuwa tunawaita – *collectors* wa michango. Kulikuwa hakuna wilaya ya Chama. Kwa hiyo akanipeleka mimi kuanzisha wilaya, kwa hiyo kuanzisha *organs* za Chama mpaka *level* ya mkutano mkuu wa wilaya, na *leadership* nzima ya wilaya.

Sasa kwenye mkutano mkuu, wa wilaya tulikwenda watu watatu: mwenyekiti, makamu mwenyekiti na katibu – mimi ndiye nilikuwa katibu wao – tukaenda Tabora.

**IS**: Na mkutano wa Tabora unaukumbukaje?

**KNM**: Eh! Mkutano wanasema ni wa kihistoria, ni wa kihistoria kweli.[7] Kwa sababu, kwanza, kwa kweli ndio kwa mara ya kwanza sasa Chama kimekuwa kimeshajiwekea mtandao wa nchi nzima vizuri tangu kianzishwe. Na uwakilishi kwa hiyo umekuja kitaifa kabisa, karibu kila wilaya ilikuwa na uwakilishi kwenye mkutano mkuu.

Ule mkutano ni mhimu kwa sababu ya nini? *Issues* zilizozungumzwa. Na *issue* kubwa ilikuwa ya uchaguzi. Waingereza walivyoona *momentum* ya TANU, waliona ni bora waanze hatua za ku-*democratise* kidogo, kupunguza pumzi ya ile *organisation* manake inakuja kwa nguvu mno. Kwa hiyo wakazua ule utaratibu wa kupata wajumbe wa *Legislative Council (LEGCO)*. Lakini kwa msingi kwamba, wakati watu wanagombea, viti vigombewe kwa mtazamo wa *multiracialism*. Na hii inaonyesha jinsi wakati ule Waingereza walikuwa wamebeba wazo la kuanzisha jumuiya zenye watu wa rangi mchanganyiko; ilikuwa ni kampeni maalum ya Waingereza. Walifikiria pengine ndio jawabu. Kwa hiyo *South Rhodesia*, kwamba ili kuhifadhi uwepo wa ma-*settler* wa kizungu, basi waweze ku-*entrench* hiyo *multiracial society* na *multiracial structure* katika uendeshaji wa nchi: wakaanzisha kule *Capricorn Africa.*[8] Hiyo ina-*advocate multiracial structures* katika hizi nchi za *Central* na *Eastern* Africa. Na walikuwa wanajaribu kuiuza hiyo Kenya, Uganda na Tanganyika. Na ujumbe wao waliuleta hapa.

---

[7] For a detailed account of this meeting see Mohamed Said, *Uamuzi wa Busara wa Tabora*.

[8] Capricorn Africa Society.

Mi nilihudhuria Arnatouglo pale mkutano, walikuja wajumbe watatu kutoka *Southern Rhodesia* ili kukutana na uongozi wa TANU. Kwa hiyo na sisi baadhi yetu tukakaribishwa tuambatane na Mwalimu kuzungumza nao. Walikuwa na hilo la lazima kuwe na sura ya watu wenye rangi mchanganyiko katika utawala wa nchi.

Kwa hiyo ndiyo wakaja na huo utaratibu wa uchaguzi wa kura tatu. Sasa utaratibu huu uliposikika kwenye jamii ya TANU haukupendwa, ulipingwa sana. Sasa inaelekea Mwalimu alikuwa ameu-*study* vizuri, yeye akaelewa namna ya ku-*deal* nao tofauti na wale waliosema *simply* ni suala la ku*reject*. Kwa hiyo pale Tabora ilikuwa kazi ngumu kidogo kwa sababu kulikuwa na watu mahodari sana wa kujieleza ambao walikuwa wamejipanga kukataa TANU kushiriki kwenye uchaguzi ule. Na Mwalimu alijua hatari yake kwa hiyo alifanya uamuzi wa busara sana. Akaona: hawa wasemaji hawa lazima ku-deal nao vizuri. Na hawezi ku-deal nao sawasawa kama atakuwa yeye msemaji na yeye mwenyekiti. Lakini vilevile akiwa mwenyekiti anaweza kuonekana hawapi haki sana wale [ili] wajieleze inavyotakiwa. Kwa hiyo ndio maana akapendekeza pale kwamba yeye aache kiti, apewe mwalimu Kihere wa kutoka Tanga, yeye [Mwalimu] akae pale kama mjumbe. Na mjadala ukawa mgumu - mwanzoni, ilionekana kundi lile linalopinga, hoja zao zinakubalika sana kwa sababu zilikuwa zimejaa jazba.

**IS**: Walikuwa akina nani hasa waliokuwa wanapinga?

**KNM**: Waliokuwa *articulate* sana *essentially* ilikuwa ni marehemu Bhoke Munanka, marehemu Richard Wambura na marehemu Edward Barongo toka Kagera huko.

**IS**: Zuberi Mtemvu hakuwepo?

**KNM**: Zuberi aliachiwa ofisi hapa Dar es Salaam. Kwa hiyo yeye hakuhudhuria mkutano. Aliachiwa ofisi. Inawezekana Mwalimu alijua kwamba ana njama zake kwa hiyo akaona asije kuwavuruga wajumbe, akaambiwa akae kwenye ofisi.

Sasa, mambo yalivyobadilika: baada ya Mwalimu kueleza, taratibu, kwa hoja na alitumia maarifa makubwa. Baada ya akina Munanka kuelezaaa, ndipo yeye akaeleza. Alipomaliza kueleza akamshauri mwenyekiti kikao kiahirishwe, akaomba, kusudi watu wakatafakari. Lakini vilevile alitaka apate nafasi ya kukutana na watu wenye *influence*. Na ile *lobbying* aliyoifanya -ita mmoja mmoja, – ita bibi Titi – zungumza naeee…

**IS**: Bibi Titi alikuwa hajazungumza bado?

**KNM**: Alizungumza lakini hakuwa na *position* kali kama ya akina Munanka. Akamwita akazungumza nae. Mwalimu akamwomba Mzee John Rupia na yeye azungumze na wengine, manake wakagawana; hata mzee Kihere wa Tanga nae, Mwalimu akamwambia, 'Zungumza [na] wale unaoweza'; taratibu, taratibu, taratibu. Tulivyo-*convene* tena…

**IS**: Katika hili wewe ulikuwa *approached*?

**KNM**: Hapana. Mimi nilikuwa mdogo sana. Lakini mimi nilikwisha-*make up my mind* kuungana na Mwalimu. Kwa sababu hoja za akina Munanka zilikuwa na maana kama ukiwasikiliza wao tu. Eee, umekutana nao wao, mko huko pembeni, halafu hujazungumza na mtu mwenye hoja hasa. Lakini baada ya kumsikiliza Mwalimu na maelezo yake na makosa tutakayoyafanya tukiacha nafasi ile, basi mwisho wote tukaelewana kwamba hakuna njia nyingine. Kwa sababu Mwalimu alitupa mfano mzuri sana, kasema, 'Sikilizeni. Simba ni mnyama mwenye nguvu sana, na ni hatari. Lakini ni hatari kama wewe nyumba yako ni mbavu za mbwa. Nyumba si nyumba, ni vijiti tu umepangapanga na nini, aah! Tena bora uache hapo ukapande mti, ukajifiche hukoo kwenye mti juu, kwa sababu ataingia tu, atapiga kumbo – kumbo tu atakuwa ndani. Lakini mtu mwenye ngome, amejenga ngome yake ya mawe, na milango yake ya chuma; simba na ukali wake wote na nguvu zake zote na mingurumo yake yote, anayonguruma, hao watu humo ndani watalala. Hawana wasiwasi kwa sababu maisha yao hayapo hatarini.'

Akasema, ‘Sasa nyinyi sikilizeni: hawa wakoloni wametupa mtego. Ile *LEGCO,* ni ngome ile. Inalindwa na jeshi. Inapofanya maamuzi yake mule ndani huwezi wewe kuwazuia wale, kwa sababu uwe  na majeshi ya kupambana na serikali. Na sisi hatuna. Sasa mkoloni ametutega. Kama tukifuata mapendekezo ya wenzetu hawa, tususe tusishiriki, uchaguzi utafanyika. Sisi tukisusa sio kwamba Mwingereza atafuta na uchaguzi; uchaguzi utafanyika, na kuna chama chake alichokiunda mwenyewe, UTP, wataweka watu. Wataweka wagombea wao, haohao - Muasia, Mzungu, Mwafrika. Watawapata, kwani hakuna Waafrika UTP? Kwa hiyo watapata hao hao, watawaweka, watafanya uchaguzi, watatangazwa wameshinda, wataingia kwenye Baraza. Na watatutungia sheria sisi wengi. Sisi itakuwa kazi yetu kufanya maandamano na kulalamika, wao wanakaa ndani wanatutungia sheria. Ndivyo mnavyotaka?’

‘Sasa mimi nasema, tunachotakiwa kufanya sisi, si anataka wajumbe watatu?  Sisi tunao Waasia ambao tunaungana mkono katika suala hili la uhuru, tuna Wazungu wanaotuunga mkono katika suala la uhuru, na Waafrika. Kwa hiyo, kweli tutashindwa kuweka watu watatu watatu? Tutaweka watu wa TANU watatu na tutashinda sisi. Kule kwenye Baraza lao tutajaa sisi, kwa hiyo sheria zitakazopitishwa tutazipitisha sisi. Tunaelewana? Sasa, lazima tuchague: tunataka tumpe nafasi Mwingereza aendelee kututawala; sisi kazi yetu tuwe nje kulalamika na kupiga kelele, yeye kaweka vibaraka mle ndani, ama anakojivunia mle tukushike sisi? Na mnajua tukishika sisi kule ndio tumeshika njia ya kwenda kwenye uhuru wetu.’ Aka! Watu wakasema, ‘Bwana, haya maneno ndiyo maneno ya busara haya!’ Ndiyo tukafanya vile. Kwa hiyo ule mkutano ulikuwa muhimu sana, kwanza, kwa uamuzi, lakini la pili vilevile ulijenga *confidence* kwa chama cha TANU.

**IS**: Katika kufanya uamuzi kulikuwa na upigaji wa kura?

**KNM**: Aah! Hapana, hatukupiga manake ilikuwa *consensus*. Baada ya mjadala ule ikawa ni *consensus*, wote tukakubaliana.

Likaja suala la uhuru lini. Waliuliza, mjumbe mmoja aliuliza, kwa sababu Mwalimu Nyerere alipokwenda Umoja wa Mataifa mwaka ’57 alitoa kauli kule kwamba Tanganyika inaweza kuwa huru ndani ya miaka kumi na miwili. Sasa watu hawakupenda ile. Mingi. Kwa hiyo wakamhoji mwenyekiti, ‘Wewe bwana kule Umoja wa Mataifa ulisema tupate uhuru ndani ya miaka kumi na miwili. Kwa nini umesema hivyo? Sisi tunataka uhuru sasa hivi, tumechoka.’ Ah! Tena walisema maneno makali na yupo mama mmoja, mama Matola, wa Mbeya, yeye akatuambia, ‘Sasa sikilizeni ninyi wanaume hasa, mna tabia – wakati mwingine mnakuwa waoga nyie. Sasa mimi nawaambieni: kama mnaogopa kupambana nae mkoloni, sisi wanawake tuko tayari kuwaweka tena matumboni kwetu; tutawawekeni matumboni kwetu, tutapambana sisi mpaka tunapata uhuru halafu tuwawazaa tena kama tulivyowazaa.’ Aah! Waswahili pale wakakasirika wakasema amekufuru: ‘Wewe mama umetudhalilisha. Haiwezekani.’ Ikawa kivumbi pale! Lakini mwisho, Mwalimu akasema, ‘Sikiliza. Mimi nikienda kule nazungumza kwa kutazama vilevile mazingira ya kidunia. Chifu Marealle, ambae ni kipenzi chao Waingereza, na walimtuma wao – alikwenda huko Umoja wa Mataifa kabla yangu. Kwenda kule alipoulizwa akasema Tanzania haiwezi kupata uhuru, *not before 15 years*. Sasa yeye kaweka miaka kumi na mitano. Na huyu Waingereza wamem-*present* kule kwamba ndio mtu mwenye busara na ni mtu mzima kuliko mimi. Mimi naonekana bado kijana, yule mtu mzima ana busara sana. Sasa mimi nikisema mambo ninayoyaona hasa, mimi ningeweza kuwaambia wale: ‘Ndani ya miaka mitano sisi tunachukua nchi yetu’. Waingereza wangesema, ‘Mnaona? Huyu ni kijana, hajui kitu. Yule mtu mwenye busara amekwambieni hapa, lazima miaka angalau 15 ipite; sasa yeye anakuja hapa, ‘miaka mitano tu!’’ Kwa hiyo hili nilisema kusudi nionekane kidogo na mie nina busara, ninawawakilisha vizuri. Lakini kama ninyi mko tayari, hata leo tuseme: ‘*Independence now*!’ Mimi niko tayari’. Kwa hiyo tukakubaliana pale, *‘Independence now*!’

**IS**: *I see*? Kwenye mkutano wa '58?

**KNM**: Ee, 58 tukakubaliana: '*Independence now*!' Lakini *of course* ukisema *independence now* haiji palepale, lakini inasukuma; na kweli ilisukuma manake *sixty-one*, tumepata. Kwa hiyo, mkutano ulikuwa mkubwa sana. Sasa, Mtemvu, aliposikia tumepitisha kura tatu, yeye alifikiri wananchi watatukatalia. Lakini unajua, kwanza Mtemvu *was not bright at all*, hata shuleni. Kwanza alifeli darasa la tisa, akachomokachomoka akaenda sijui Dodoma, akarudia, akajaribu *Standard Ten* sijui aka-*scrape through*, akaenda *eleven* Tabora, akaondolewa. Hakuweza kufika *Standard Twelve* kufanya *Cambridge School Certificate*, kwa sababu mpango wa elimu wa Waingereza ulikuwa unachuja kweli kweli. Kwa hiyo yeye akafanya maamuzi wakati Chama kule kimeshikamana. Kwa hiyo alivyotangaza huku, sisi tulikuwa bado Tabora, akatangaza ameunda Chama.

**IS**: Wala hamjarudi bado?

**KNM**: Aanh, bado, na kikao kinaendelea. Basi, Mwalimu akampigia simu Abbas Sykes, huyu balozi mstaafu, akamwambia, 'Ndugu yangu Sykes, nenda uka-*take over* ofisi ya Chama. Chukua funguo zote na kila kitu kutoka kwa Mtemvu'. Kwa hiyo, Abbas akaja aka-*take over* ofisi. *You see, what transpired* ni kwamba Mtemvu alikuwa *political*, na wazee wa Dar es Salaam walimpendelea afanye kazi karibu na Mwalimu. Kwa sababu, pamoja na kwamba yeye ni mwenyeji wa Morogoro, lakini ni mkulia wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, hata wazee wake walikuwa hapa. Sasa ile kuwa na Mwalimu, anakwenda nae Zanzibar na nini, akafikiria lile waridi linakuambukiza na yeye kwa kuwa yuko na waridi lile na yeye atanukia katika *popularity*, kwamba atapotoka watu watamfuata. Lakini *he made a miscalculation* kabisa.

**IS**: Watu waliomuunga mkono ni akina Chifu Kunambi?

**KNM**: Eee, Chifu Kunambi. …… Ah! Katika Chama, nilivyomwona mimi wakati ule, alikuwa anaonekana ni kwamba

*he was second to Mwalimu* katika watu waliosoma. Na nadhani hiyo nayo alikuwa anai-*feel*. Kwa hiyo, nadhani *feelings* zake zile za nafsi zilimpeleka pabaya. Unajua alipata *cris* Morogoro kwa sababu ya kujaribu kuipinga TANU?

**IS**: Ndio.

**KNM**: Enh, walikuwa *confronted* na *mob* mpaka mama yule alikuwa *mishandled* kabisa na wananchi *publicly* kwa sababu ali-*miscalculate*. Sasa Mwalimu alisimamia ndoa yao, ndoa ya Kunambi. *They were quite close* lakini *of course* Kunambi ni mkubwa zaidi kwa umri, na Makerere alitoka mapema zaidi nadhani. Lakini akafanya *blunder* pale, aah! wananchi wa Morogoro wakamuadhir sana.

**IS**: Sawa, mimi naona tumefikia mahali pazuri, bila shaka utakuwa umechoka. Sasa tutakaporudi ndio tutaanza na ile safari yako kwenda nje sasa.

**KNM**: Aaah, *okay*.

**IS**: Kwa sababu ilitokea karibu na wakati huo, sio?

**KNM**: Baada ya mkutano wa Tabora. Kwa sababu Kamati Kuu iliamua kabla hatujaenda Tabora kwamba niende.

**IS**: Kamati Kuu iliamua?

**KNM**: Enh. Kwa hiyo baada ya mkutano mkuu wa Tabora ndio Mwalimu akatangaza rasmi. Tulifanya mkutano Morogoro pale na wananchi, kwa hiyo akaeleza mipango ya Chama na nini: 'Sasa, nataka kukutangazieni hapa kwamba Chama chenu kimeamua vijana wetu watatu tunawapeleka nje kusoma – tunawapeleka Liberia.' Sasa, wawili tulikuwepo pale – mimi na marehemu Gisler Mapunda.

**IS**: Ahaa, Gisler Mapunda! Wakati ule?

**KNM**: Eee, ndio tulikuwa wote. Sasa [Mwalimu] akasema, 'Vijana wale palee'…

**IS**: Wa tatu alikuwa nani?

**KNM**: Wa tatu alikuwa Nyelwa Kisenge. Kisenge alikuwa katibu wa wilaya ya Bagamoyo; Gisler Mapunda alikuwa katibu msaidizi wa ofisi ya Chama mkoa wa *Eastern Province*, ulikuwa ndio mkoa wetu na mimi nilikuwa katibu wa Wilaya ya Rufiji. Basi akatutangaza pale rasmi, kwa hiyo tukarudi hapa tukajipangapanga, tukaenda Liberia.

**IS**: Sawa, kwa hiyo tunamalizia hapa.

## 07 Agosti 2012

**IS**: Kamati kuu ndio iliyowachagua nyie watatu kwenda Liberia. Turudie pale. Mlienda kwenye chuo gani?

**KNM**: Sasa, baada ya kuteuliwa na Kamati Kuu ya TANU, ndio tukasafiri mwezi Juni mwaka ’58 kwenda Liberia.

**IS**: Na hii ilikuwa ni *group* ya pili?

**KNM**: Ndio, kundi la pili. Kundi la kwanza, mwaka ’57, walikwenda wenzetu Paul Rupia na marehemu Makata. Paulo kutoka Dar es Salaam na Makata kutoka Tanga. Utakumbuka Paul Rupia ni mtoto wa *Vice-President* wa TANU, Mzee John. Kwa hiyo mwaka huo wa 1958, ndio Kamati Kuu ikaamua tupelekwe makada wa Chama ambao wanashughulikia suala la kupigania uhuru wakati wote. Mimi nilikuwa Katibu wa Wilaya ya Rufiji na ndugu Gisler Mapunda akiwa Katibu msaidizi katika ofisi ya Chama ya mkoa wa jimbo la Mashariki, *Eastern Province*, wakati ule Morogoro, na ndugu Shaaban Nyelwa Kisenge akiwa Katibu wa Wilaya ya Bagamoyo.

Sasa kule Liberia walikuwa na vyuo vikuu viwili – *University of Liberia*, chuo kikuu cha serikali pale Monrovia, makao makuu; na *Cuttington College and Divinity School* ambayo ilikuwa ni chuo cha kanisa, kinamilikiwa na kanisa la Kimarekani. Tulipofika tukakuta kile chuo [Cuttington] ni kidogo, kinafundisha masomo ya *arts* ya kawaida kwa watu wanaochukua *degree*, na vilevile kinafundisha watu ili wapate digrii za masuala ya dini ya Kikristo. Walikuwa na utaratibu, wanafunzi wapya wanapewa mtihani wa kuwajua wamefikia kiwango gani na wanaelewa nini n.k. Wanaita wenyewe *placement test*. Tulifanya sisi watatu kwa sababu tulikuwa tumechelewa *semester* ya kwanza, tumefika pale mwanzoni wa *semester* ya pili. Baada ya kupewa mtihani ule wale wakuu wa chuo wakaona sisi watupe kama vile upendeleo kwa sababu walituanzishia mchepuo wa masomo maalum, yaani …

**IS**: Ni filosofia lakini *programme* maalum?

**KNM**: Eee, *programme* maalum ya falsafa, ambayo walikuwa hawafundishwi watu wengine kwa sababu falsafa zaidi walikuwa wanafanya kwenye *divinity*, yaani mafunzo ya dini ambako wanajifunza thiolojia na falsafa. Lakini kwenye *arts* za kawaida kulikuwa hakuna digrii ya falsafa. Ni sisi watatu, kwa hiyo tukawa na darasa la watu watatu, na mwalimu wetu mmoja tu akawa ndiye anatufundisha masuala ya falsafa. Anasimamia *programme* yetu…

**IS**: Na walikuwa nani hasa, vitabu vya akina nani, falsafa ya nani?

**KNM**: Falsafa, tulianzia kwa Magiriki wa jadi, wa zamani, akina Socrates, Plato, n.k. Tulizunguka sana kwa sababu tulikuwa na nafasi watu watatu kwa hiyo mwalimu akiona ana *interest* ya jambo fulani anapanua. Sasa, masomo yalikuwa mazuri, sisi wanafunzi wa kutoka Tanganyika wakati ule tuliongezeka tukawa wengi kidogo, mwaka 1958 tukatimia watano, mwaka 1959 wakaja wenzetu wengi, tukawa zaidi ya 15. Lakini mwaka huo walikuja kundi kubwa kidogo la vijana kutoka Kenya, lakini tulikuwa vilevile na jamaa wa Nigeria na Ghana. Kwa upande wa Afrika Mashariki, pamoja na sisi wa Tanganyika, tulikuwa na mwenzetu mmoja kutoka Zanzibar, ambaye alikuja pamoja na waliotoka kwenye TANU kwa sababu ya uhusiano uliokuwepo kati ya TANU na *Afro Shirazi Party* tangu wakati ule wa kupigania uhuru. Sasa, sisi kwa upande wetu wa Watanganyika tulikuwa tunatumia vilevile nafasi yetu ya kuwa pamoja kule kuzungumzia mambo ya siasa za huku kwetu, ambazo ni siasa za kupigania uhuru kwa wakati ule.

Sasa tulipofika mwaka 1959, katika mazungumzo yetu tukaona kuwa kuna haja ya kutoa mawazo kwenye chama chetu juu ya Tanganyika huru iwe na sera ya msingi ya aina gani. Na kilichotufanya tufike hapo ni kutokana na mambo tuliyoyakuta Liberia wakati huo. Sisi tulikuwa wapigania uhuru, *freedom fighters*. Na katika fikra zetu na matarajio yetu, uhuru ndio utakuwa suluhisho la hali yetu Waafrika kunyanyaswa na

kukandamizwa na kuonewa. Kwa hiyo suala la usawa na utu, tuliona suluhisho lake uhuru. Na kwa hiyo tulipokuwa tunakwenda katika nchi, tuliambiwa ni nchi ya Kiafrika ambayo ni huru, matarajio yetu vilevile yalikuwa makubwa kuona ahaa! Tutaona mambo katika nchi ambapo Waafrika wenyewe wanaendesha mambo yao.

Sasa, tulipokewa vizuri sana kwa sababu Waliberia ni wakarimu sana, walitupokea vizuri sana. Na hasa vilevile wakati ule Afrika Magharibi ilikuwa mbali sana, kwa sababu mawasiliano yalivyokuwa yalikuwa tofauti. Kwa hiyo kusikia kuna vijana wanaitwa Watanganyika, wanatoka Tanganyika: aah! wanastaajabu kabisa. Tulikuta mahali pamoja, mtu mmoja mtu mzima sana, tumekwenda na kundi halafu tukatambulishwa pale, 'Hawa ni rafiki zetu wanatoka Tanganyika'. Yule mtu mzima akashtuka sana, akasema, '*What! From Tanganya-i-ka*?' Wakamwambia, '*Yes*.' Akasema, '*The world is getting smaller and smaller'*. Alipiga kelele hasa, anasema: 'Tanganyika? Kweli dunia inazidi kuwa ndogo!'

Kwa hiyo tumefika kule lakini yako mambo yakatufanya tutafakari upya kwa sababu tuliyoyaona hayakufanana na matarajio yetu. Kwanza tukakuta jamii imegawanyika katika matabaka. Kule Liberia kulikuwa kuna watu wanaitwa wenyeji – *natives* ndio neno wanalotumia, *natives*. Na kundi la pili ni la watu ambao wazazi wao walitoka Marekani, walikuwa miongoni mwa wale watumwa walioachiwa huru baada ya vita ya wenyewe kwa wenyewe ya Marekani, mwisho wakakomesha na utumwa; kwa hiyo watumwa wakapata uhuru. Basi baadhi ya watumwa walioachiwa huru, mashirika fulani yakafanya mpango wakatafutiwa mahali katika Afrika, kwa hiyo wakaletwa Liberia. Na jina lenyewe wakapewa hilo la nchi ya uhuru. Sasa hili kundi la wazaliwa waliotokana na hao watoto wa watumwa wa zamani wa Kiafrika waliokuwa Marekani lilikuwa ni kama kundi la pekee, na walikuwa wakijiita wenyewe *Americo-Liberians*, Waliberia wa Kimarekani. Sasa hawa ndio walikuwa wanaitwa

wastaarabu, watu *civilised*, waungwana. Hawa wengine, *natives*. Na kwa tafsiri nyingine ndio wasiokuwa wastaarabu maana yake. Sasa hilo tukalikuta, na kwa sehemu kubwa hawa *Americo-Liberians* kwa wakati ule ndio waliokuwa wameshika madaraka mbalimbali, kuanzia ya kiserikali, ya kisiasa, lakini hata ya kitaalam, na kadhalika.

Sasa hata sheria, kulikuwa na sheria kwa ajili ya *natives*. Hata uendeshaji wa mahakama, kwenye mahakama hizi za *natives* mtu yoyote anaweza, mtu ambaye hakusomea sheria anaweza akajiandikisha akawa yeye ni wakili. Lakini zile mahakama za waungwana zile mambo yote yanakwenda kisasa kama zinavyokwenda katika nchi nyingine. Kwa hiyo hilo jambo likatushtua sana.

**IS**: Na hii hamkujua kabla ya kwenda Liberia?

**KNM**: Hatukujua. Hatukujua kwamba nchi moja, wengine ni wanyonge tu wengine ni wastaarabu. Na hiyo ilikuwa na maana nyingi kwa sababu hata majina ya watu – pale Chuoni palikuwa na utani – sisi majina yetu ni yale ya kawaida, mimi pale Ngombale, wanauliza, '*What's your name*?' 'Ngombale' '*What*? Ngombale?' Huyu Mapunda, huyu Kiseri, wanasema kwa utani, '*Country people*!' – washamba maana'ke. Sasa sisi lakini tunajivunia majina yetu. Sasa pale katika mazingira yao wenyewe ilikuwa mtoto wa ki-Liberia anayetokana na *natives*, ana jina la ki-*native*. Akitaka akubalike katika mazingira ya elimu na shughuli za kisasa inabidi abadili jina, awe na jina *Anglo-Saxon* - Smith, Johnson, Tubman - hapo ndiyo. Na hawa *Americo-Liberians* walikuwa wakati mwingine na tabia ya kuwachukua watoto wa *natives* na kuwalea hata kuwasomesha lakini wanawabadili majina, wanawapa majina ya ki-*Anglo-Saxon;* asije na jina lake la kishamba. Kwa hiyo tulikuta hali pale Chuo Kikuu.

**IS**: Sasa hii mliipata kutoka kwa wenzenu Waliberia au mli-*observe* tu nyie wenyewe?

**KNM**: Aa, tuli-*observe* majina lakini tulielezwa na wenzetu. Hiyo kuwepo kwetu pale na kwamba sisi tulikuwa tunaona kuwa na jina lako la Kiafrika ni jambo la sawasawa kabisa, ndivyo inavyostahili, wakati wao wameambiwa kuwa na jina la ki-*native* ni kudhihirisha kwamba wao ni dhalili, walionee haya; kwa hiyo lazima achukue jina la ki-*Anglo-Saxon*. Pale palianza kuwa na vurugu pale, watu wanaacha majina waliyopachikwa wanachukua, baadhi ya wanafunzi, wanachukia majina yao. Wanaanza kubadili majina kwa sababu walianza kuona kwamba, 'Ah! Lakini hawa wenzetu wanasema kweli bwana.'

Kwa hiyo nasema hilo moja lilitushtua, la matabaka. Lakini la pili ni bado kulikuwa na unyanyasaji unaouona katika nchi zinazotawaliwa. Kwa mfano pale, wakati ule mwajiri mkubwa alikuwa mmoja, alikuwa ni kampuni ya *Firestone*, kampuni ya mpira. Kampuni kubwa! Walikuwa na shamba linaloajiri, wakati ule mabango yake tunaingia pale nchini, ilikuwa wanasema wafanya kazi thelathini na tano elfu. Na wafanyakazi thelathini na tano elfu kwa nchi kama Liberia, nchi ndogo kwa idadi ya watu, ni kundi kubwa sana. Wale ndio waajiri. Sawa. Lakini, kwanza iko hiyo, lile zao la mpira lilikuwa la muhimu sana, kwa hiyo na Waliberia wakubwawakubwa, kuanzia rais na mawaziri na wao walikuwa wakulima wa mpira. Rais alikuwa ana shamba kubwa! Rais Tubman, shamba kubwa; na makamu wake, shamba kubwa; na mawaziri na Waliberia wengine ambao hawamo serikalini lakini ni matajiri.

Sasa walikuwa na tatizo la wafanyakazi, utawapataje wafanyakazi kwa utaratibu wa kawaida tu? Ah! Lakini ukatumika utaratibu kama wa ukoloni, kwa sababu ukoloni hata hapa, kuanzia Wajerumani, ili Waafrika waweze kufanya kazi kwenye mashamba yao ama mashamba ya Wajerumani, walikuwa wanawalazimisha kwa kuwatoza kodi. Ndio mwanzo wa kodi ya kichwa: unalazimishwa kulipa kodi, sasa pesa za kodi utapata wapi? Kwa hiyo, lazima utafute kazi: unaenda kwenye shamba la mzungu. Lakini kule sasa, nadhani hata huo mpango wa kodi

haukufua dafu. Na Liberia wakati ule walikuwa wanaheshimu utaratibu wa machifu. Kulikuwa na mpangilio wa uchifu, kulikuwa kuna *paramount chief*, halafu kuna *lower chiefs* mpaka huko chini huko. Sasa, kazi ya mkubwa, serikali kuu inamwagiza *paramount chief* wa eneo fulani: 'Wewe bwana, mwezi fulani kuanzia tarehe fulani lazima utoe watu kadhaa'. Akiambiwa alete watu mia tano, halafu yeye atawagawa kwa ma-*sub-chief* wake, kama ana ma-*sub-chief* watano, mia mia watoe. Na yule *sub-chief* akiwa na wenzake wa chini yake kadhaa, anagawa. Kwa hiyo, mwisho watapatikana wale watu ili waende kwenye mashamba, kwenye mashamba ya kampuni ya *Firestone* ama kwenye mashamba ya Waliberia wakubwa wenye mashamba yao.

Sasa, hilo nalo tukajifunza, tukaelezwa ndivyo inavyofanyika; ni kazi ya kulazimisha hii – *forced labour* hii. Tena wengine wakatuambia, 'Hata mkicheki taarifa za *International Labour Organisation [ILO]* imewakemea sana; serikali imekemewa huko Geneva.' Kwa hiyo, kulikuwa na watu wana-*agitate* kimya kimya. Ah! Lakini ilikuwa kubwa mno. Kwa hiyo, mambo ya namna hiyo – tabaka waziwazi, pili, watu kama vile wanaburuzwa tu kwenda kwenye mashamba ya watu wengine kwenda kulima – yakatu[shtua], 'Jamani, hivi na sisi tukipata uhuru ndio tutaendeshwa hivyo? Ndicho hiki tunachopigania? Lazima tujiulize.' Kwa hiyo katika mazungumzo yetu, tukazungumza, tukaandika kumbukumbu – *memorandum* – kuleta kwenye Kamati Kuu.

**IS**: Na wote, Watanganyika, walikutana kwenye hiyo *memorandum*?

**KNM**: Eee, wote tulikutana. Wote tulikuwa watu wa TANU, wapigania uhuru wote. Na tukasema mambo tunayopigania ni utu wetu, ukoloni umetunyang'anya utu Waafrika, ukoloni umetukandamiza, ukoloni umetunyanyasa. Sasa, tunataka tutendewe kama watu, kwa hiyo lazima tudai usawa. Sasa sera gani? Na sisi tulikuwa na masomo yetu wenyewe Watanganyika tunasoma ujamaa (*socialism*).

**IS**: Mlikuwa mnasoma socialism?

**KNM**: Eee, wenyewe lakini, kwa sababu sisi wengine – mimi nilianza kufuatilia sera ya ujamaa tangu niko hapa.

**IS**: Ulikuwa umeshasoma Marx?

**KNM**: Marx nilikuwa nimesoma *Manifesto*, nimeisoma mwaka 1956. Kuna rafiki yetu mmoja, jamaa yetu mmoja, alikuwa anasoma India – amefariki juzi tu hapa tena – alikuja na *Das Kapital*. Lakini *1956, ex-twelve,* wakati ule *standard twelve of course* sio kama *standard twelve* ya sasa, lakini, manake nilikuwa naweza kusoma. Nasoma lakini kavu mno ile. *Das Kapital* nimeisoma vizuri nilivyokuwa Liberia, hapa niliipitia tu. Lakini *Manifesto, of course* ni *political document*; ile ndio ilinichangamsha.

Lakini nilipata *document* nyingine siikumbuki jina, niliipata kwa afisa kilimo mmoja kijijini kabisa huko Rufiji. Nimekwenda kufanya mkutano, baada ya mkutano wa hadhara kumbe mmoja pale alikuwa Bwana Kilimo, kijana tu kama mimi wakati huo. Wale wazee pale wakamuita wakamwambia, 'Wewe umemsikia mwenzako anavyoongea?' Akasema, 'Mimi nilikuwa nasubiri niwaombeni ruhusa akalale nyumbani kwangu'. Kwa hiyo aliwaomba wazee wale nikalale kwake, nisilale kwenye mapokezi ya Chama. Kwa hiyo nikaenda kulala kwake: alikuwa na vitabu, *of course* aliyeandika nani, ni Stalin. Ameandika Stalin anamsifu Lenin, lakini *style* yake ya kuelezea *Leninism* ilinivutia sana. Kwa hiyo sasa nikichanganya, na wakati huo nilikuwa nimesoma mambo mengi, Tom Paine unamkumbuka? *The Age of Reason* na nini.

**IS**: *Yes*.

**KNM**: Nimeisoma, basi kwa hiyo nilivyokuwa nimeondoka, tayari nilikua nimeshachangamka kichwani. Kwa hiyo tulikuwa kama tuna *cell*.

*cell* yetu ya kujifunza ujamaa. Sasa kwa sababu vitabu vilikuwa *available* zaidi, tunajadili masuala ya ujamaa. Kwa hiyo katika mkutano wetu…

**IS**: Lakini katika mijadala hii kina Paul Rupia walikuwepo?

**KNM**: Enh, wote. Wote walikuwepo katika *group* yetu. Tulivyofika sisi sasa hata wao wakaingia katika joto hilo kwa sababu sisi tumekwenda pale tulikuwa *very political*. Hata Gisler Mapunda alikuwa political, Kisenge alikuwa vilevile *very political.* Kwa hiyo sisi tumekwenda pale kama *activists* kabisa na wenzetu wengi tu walikuwa na wao wana mwamko mkubwa.

Wakati wa kupigania uhuru yanakuja mawazo mengi kwa hiyo tukaandika *memorandum*. Na ndio tukapendekeza sera ya *socialism*, hatukusema ujamaa.

**IS**: Hii ni hamsini na tisa hii?

**KNM**: Hamsini na tisa. Tukapendekeza kwamba tutapopata uhuru… tunajua karibu tutapata, tuongozwe na sera ya *socialism*. Tukajaribu ku*argue* kwa nini tunafikiria hivyo.

**IS**: Tunaweza tukawa na nakala ya hiyo? Inaweza bado ikawepo?

**KNM**: Sijui, niliwahi kuwauliza kwenye *archives*, inawezekana ikawepo. Lakini inawezekana ilishatupwa. Kwa sababu utaratibu wa *archives* umeanza kushughulikiwa katika *eighties*, *nineteen eighties*. Sasa huwezi kujua nyuma ya hapo kulikuwa na utaratibu gani.

**IS**: Na hii ilienda kwa Kamati Kuu?

**KNM**: Eeh, tuli*address* kwa Kamati Kuu, mwenyekiti wa Kamati Kuu.

**IS**: Mlipata *feedback*?

**KNM**: Kwa sababu na sisi wenyewe baadaye tuka… palitokea matatizo pale Liberia. Chuo kile kikawa *radicalized, politically*, kikawa na msimamo mkali. Watu wanazungumza mawazo ya *socialism* wazi wazi. Na wakati ule wa *cold war*, Marekani

walikuwa na mashaka na kila kitu. Lakini na wakuu wa nchi ya Liberia walikuwa *holier than the Pope.* Na sasa kwa sababu mambo yanachukua mrengo wa kushoto, wana fikra kwamba wameingia wakomunisti, ni watu hatari sana.

*Nineteen sixty* akaja rais kwenye *graduation ceremony*. Si kawaida yake, wanasema mara ya kwanza tangu chuo kianzishwe. Rais Tubman hotuba yake sehemu kubwa akaitenga kuzungumza juu ya maadui wa sera ya msingi ya *free enterprise*. Na watu wanakuja na *philosophies* hapa wanavuruga vuruga, akatoa *warning*. 'Ma*lecturers* wanaowadekeza, wanaofanya urafiki na wanafunzi, wenye fikra hizo, tutawafukuza. Hawawezi kufundisha katika vyuo vyetu hapa Liberia. Na wanafunzi ambao wana mitizamo hiyo tunajua la kuwafanya, wamepotea njia kuja hapa.' Alikuwa *rough* kweli kweli.

**IS**: 1960 hiyo.

**KNM**: 1960. Vijana wa Kiliberia tumekaa wanatugonga hivi, wanatuambia 'Anakusemeni nyinyi hapo.' Huyo bwana akasema sana, basi.

Halafu yule Mkuu wa Chuo alikuwa ni *Father* Edwards, Mmarekani mweusi, mtu mzima. Alikuwa mtu mstaaarabu sana. ni *father* padre alikuwa ni kama baba kweli, alikuwa ana*behave* kama mzee. Nadhani walizungumza nao huko wakamwambia 'Bwana mzee wenu huyu mtafutieni kazi huko huko Marekani. Na sisi sasa tunaona hapa lazima mkuu wa chuo awe ni Mliberia.'

Wakamleta bwana mmoja Dokta Baker, Mliberia kuja kuwa Mkuu wa Chuo. Kaja pale ndio kivumbi, kama vile ameambiwa akapambane na *foreign students*. Mikwaruzano na wanafunzi, na bahati mbaya alikuwa zaidi na wanafunzi wa Tanganyika ndio walikuwa *radical*. Walionekana ndio wakomunisti. Mimi ndo kabisaa, mimi ndio nilikuwa mwenyekiti wa *steering committee* wa kamati ya wale *foreign* wote na vile vile kamati ya Watanganyika.

Sasa siku moja akaniita, Dokta Baker akaniita akaniambia '*Look, my friend*'; mjeuri sana alikuwa huyu bwana akaniambia *'This place is too small for the two of us*. *Either you be here and I go or I be here and you go*.' Nikamsikiliza, nikamwabia '*What is happening*?' Akasema '*Oh! You have too much leadership ability, this place is too small*.' Basi kwangu mimi bahati nzuri ilitokea. Ma*comrade* wawili walikuja katika *delegation* ya wanafunzi wa *French-speaking African countries*. University of Dakar, ilikuwa ina*cater for* wanafunzi wa *West Africa*, wa nchi zote karibu za *French-speaking*. Kwa hiyo walikuwa na *organisation* yao. Na wanafunzi wa Kiafrika Ufaransa walikuwa na *organisation* yao. Tulikuwa tunaita FEANF[9], *Federation* sasa walikuwa wanafanya kazi pamoja. Na walikuwa *very anti-imperialist, anticolonialist, very progressive*.

Sasa kumbe walikuwa wamekutana wakaamua watume *delegation* kutembelea vyuo vikuu vya *West Africa* vya *English-speaking countries.* Kwa hiyo wakaenda Nigeria, wakaenda Ghana, wakaenda Sierra Leone, wakaja Liberia. Liberia wakaenda *University* ya Liberia, wakaja Cuttington. Sasa Cuttington pamoja na kuzungumza na *student organisation* yote, wakazungumza na mimi, waka*take interest*.

Kwa hiyo mimi na wao wawili hatukulala, tukazungumza *the whole night*. Na wao walikuwa wanaondoka siku ya pili, tukazungumza. Wakani*brief* juu ya *situation* ya *universities* hizo walizotembelea. Na wakani*brief* pia *organisation* yao ya *West Africa* na nini. Wakastaajabu wakasema 'Wewe umetoka wapi? Mbona sisi tumetembea kote, Nigeria wapi hatukukuta mtu kama wewe. Wewe imekuwaje?' Maana yake wale vijana wote ni *Marxists,* wale wote. Mmoja Dan Soko Amath 00:43:55, mwingine huyu Abdulrahman… nimemsahau jina, jina lake. Watu safi sana. Nikawaambia sasa sikilizeni, mimi niko hapa

[9] Federation des Etudiants d'Afrique Noire en France (Federation of Black African Students in France).

lakini sidhani kama nitamaliza kwa sababu ya hali ilivyo, nimekwishakuelezeni. *Regime* ni *very hostile* na sio *regime* peke yake, pamoja na Marekani, *directly* wanaingilia hapa. Sasa wamemleta huyu *gorilla* wao, huyu nini… Mkuu wa Chuo hapa sasa hivi wamempa kazi hiyo tu. Kwa hiyo sina hakika kama naweza kumaliza.

Wakaniambia ‘Bwana eeh, *don’t worry*, ukipata *problem* yoyote wewe njoo Dakar. Ukifika Dakar tu tunaku*assure* tutatafuta sisi *scholarship* utapata na utaendelea. Na ukitoka hapo Dakar ukitaka Ufaransa.’ Wakaniambia ‘Sisi wenzio *we are very strong*.’ Nikasema basi vizuri. Yule wa Dakar akanipa anwani yake na kila kitu.

Basi nilikaa pale, hali inazidi kuwa mbaya tu. Yule bwana akaunda mazingira mabaya kweli. Watanganyika wale jamaa wakaniambia ‘Bwana sikiliza, sisi tunatoroka, tunaondoka. Hatuwezi kukaa hivi hawa watu wanaweza hata kutufunga na sisi hatujafanya lolote.’ Basi wale vijana wa Tanganyika wakaanza kutoroka kidogo kidogo.

**IS**: Kati ya wale kumi na tano?

**KNM**: Eeh, mimi nikawaaambia mimi sitoroki. Sitoki hapa, wanitoe wao. Basi nikakaa mwisho na mimi nikaona nitoke, nikatoka.

**IS**: Ilikuwa *nineteen sixty* hiyo?

**KNM**: Sasa *sixty-one*.

**IS**: Ulikuwa bado hujamaliza masomo yako?

**KNM**: Eeh, bado miezi sita. Mimi na Mapunda ilikuwa bado miezi sita. Kisenge tulimbakiza, alibaki. Kisenge wale Wamarekani wanasema tunaomuharibu ni sisi, mimi na Gisler. Na walishamuahidi *scholarship* ya kwenda Marekani kufanya *Masters*. Wakati huo Paul Rupia na Mwarami walishamaliza.

**IS**: Wakarudi nyumbani?

**KNM**: Walikwisharudi nyumbani. Paul alikwenda Marekani, Mwarami alirudi nyumbani, alipata *cris*, alichanganyikiwa. Iliamrishwa akasaidiwa na daktari mmoja. Basi kwa kuwa wenzangu walishakimbia, walishatangulia… lakini walikuwa *stranded* Conakry. Na mimi nikaondoka. Nikadanganya, maana yake mimi niliondoka walitaka kunifunga lakini nikapata *information*. Kwa sababu mimi nilikuwa nafanya kazi, *political work*, sana. Kwa sababu kulikuwa na vijana ambao walikuwa wamemaliza masomo pale, walikuwa wanafanya kazi mjini. Sasa lakini walikuwa wanataka msaada wangu, mawazo. Hawajui namna ya ku*organise political parties* na nini nakwenda nafanya nao kazi. Najaribu kuwapa *ideas* na namna ya ku*organise*, katiba ya chama inakuwa kuwaje na nini.

Unajua Liberia waliiweka katika hali… walikuwa wameendelea *materially* kwa upande mmoja. Lakini katika mambo ya kisasa mengi bado. Kwa hiyo nilikuwa… Hasa mmoja huyo nilim*advise*, nilikuwa na mazungumzo naye. *He was very good*, namwambia haya mambo unaandika andika usiache karatasi zozote nyumbani kwako. Tafuta shangazi yako mmoja au bibi yako mmoja ndio unaweka vitu vyako, hapana kuweka nyumbani. Kwa sababu *regime*, kulikuwa na watu *unhappy with the regime*. *Working class* ilikuwa nayo ina manung'uniko yake na nilikuwa nakutana nao mimi.

Basi, nikaja kupata habari kwamba 'Wewe bwana wanakutafuta, *any time* watakukamata. Na wakikukamata hawa huwezi kujua *future* yako. Kwa hiyo bora uende.' Nikapata mtu mzuri sana msamaria akani*drive all the way*, tena msichana, mpaka mpakani. Akawababaisha pale anajitia mimi *boyfriend* wake, akasema 'Mtu wa ovyo huyu, mimi nimemwambia twende wote Conakry, lakini unajua watu wa ma*coastal*…' Maana yake wageni wanawaita *coastals*, watu wanaotoka *from the coast*. 'Hawaaminiki hawa, sijui anakwenda huko … Unafikiri atarudi huyu, ameniahidi atarudi lakini harudi lolote huyu. Bila shaka ana *girlfriend* mwingine huko.'

Basi kawadanganya pale, nikavuka. Nilivyovuka moja kwa moja. Baada ya wiki kukawa na *strike* kubwa kweli. Wakanitafuta, walifikiri bado nipo wanikamate, niko Conakry. Yule rafiki yangu akakamatwa, walimfunga *life*. Wamekuja kumpa msamaha baada ya Rais Tubman kufa. Sijui kama yuko hai tena. Wanasema walimkuta na makaratasi na nini sijui. Mimi nilimueleza kabisa, maaadamu una*take interest* ya kutaka ku*organise* mambo na *regime* yenu iko hivi… Manake walitueleza wale mambo yote ya undani ya *regime*. Na uchaguzi… sisi tumefika *fifty-eight*, uchaguzi wa mwisho ulikuwa *fifty-six*, na walitueleza ulivyokuwa mbaya sana.

Kwa hiyo nikamwambia huwezi kukaa na *documents*. Wakitaka kukuonea wakuoneee tu, lakini usiwape ushahidi. Kwa hiyo ndio nikaenda Conakry nikawakuta wenzangu. *Central Committee* haijajibu.

**IS**: Mliwaandikia *Central Committee* kwamba tunaondoka?

**KNM**: Eeh, tukawapelekea *message* na mimi niko pale. Wakasema watajibu, watatafuta nafasi. Soviet Union na GDR.

Basi mimi nikawaambia wenzangu jamani mimi nakuacheni hapa. Nakuacheni niende Dakar. Nikapanda meli pale, sio mbali sana. Nikaenda nikawakuta wenzangu, nikamkuta… hakuwepo yule, ilikuwa wakati wa likizo. Lakini hawa nilipowaambia mimi namtafuta nini, fulani wakasema ‘Ah! Unamtafuta fulani? Wewe unatoka wapi?’ nikawaeleza. Wakasema ‘Basi.’ Tena wakanitafutia na chumba Chuo Kikuu.’ Nikaaambia ‘Bwana, ntakupa chumba msubiri.’

**IS**: Senegal uhuru bado?

**KNM**: Wakati huo wameshapata, *sixty-one*, wamepata *sixty* wale. Kwa hiyo alipokuja pale wakakutana na wenzake, wakasema ‘Jamani lazima, huyu bwana nilim*promise*, lazima tumpe bwana *comrade* huyu. Kwa hiyo tumtafutie *scholarship*.’ Wao wamehangaika mimi wala sina habari. Mara wamekuja kuniambia ‘Bwana wewe umeshapata *scholarship full*, kila kitu.’

**IS**: Ukijiandikisha pale University of Dakar sasa?

**KNM**: Eeh, University of Dakar. Nimesoma vizuri sana pale. Na vile vile *political atmosphere* nzuri sana. Maana yake wale vijana walikuwa na mwamko wa hali ya juu zaidi. Na unajua kwa sababu ukoloni wa Kifaransa si una*centralise* kila kitu. Kwa hiyo *ideologically* yaliyoko Ufaransa ndio yaliyoko Senegal, Paris. Kwa sababu … kwanza hata *lecturers* kuna *range* yote pale: kutoka *Marxist* mpaka *neocolonialist* wakubwa katika ma*lecturers* wote wapo. Na vyama vya siasa vya Ufaransa kuna shade off zake huku. *Trade union* za Ufaransa, kwa hiyo pale Chuo Kikuu cha Dakar palikuwa na *cells* za *communist party*.

**IS**: *Communist party* ya kifaransa?

**KNM**: Walikuwa na chama chao cha Senegal. Chama cha *African Independence*. Sasa lakini wale *Marxist militant* pale chuoni walikuwa wote *united* wakitoka nchi zote: wa Cote d'Ivoire, wa Mali.

**IS**: Wengine pia walikuwepo pale?

**KNM**: Wote, wote, ilikuwa kwa ajili ya nchi zote hizi. Upper Volta, siku hizi Burkina Faso, wote walikuwa pale. Kwa hiyo ni *boiling pot* ilikuwa. Kwa hiyo…

**IS**: Unaweza kukumbuka wale uliokutana nao kwa jina ambao tunawafahamu?

**KNM**: Aah, he! Wengi nishawasahau, siku nyingi na mimi si mtu hodari wa majina. Tena najaribu kuwakumbuka wengine walikuwa rafiki zangu sana… kwa tabu sana. wengine wa Dahomey, … Wanavyopita hapa lazima wanitafute.

**IS**: Ulikaa pale kwa muda gani?

**KNM**: Nilikaa pale ukichanganya na Ufaransa…

**IS**: Ulienda Ufaransa pia?

**KNM**: Eeh, *six and a half years*. Nilikuwa nikienda kwa miezi kadhaa. Nilienda mara kadhaa lakini kama sehemu ya masomo

yangu: nilikwenda mara ya kwanza *cultural* tu, kwa ajili ya Kifaransa. Kwa sababu nilikuwa nafanya *advanced diploma* ya *French studies* katika *philosophy*. Kwa hiyo wakanipeleka *for three months* kule kwenye *University* ya Toulouse. Lakini nilikwenda tena kwa ajili ya masomo kama sehemu ya masomo yangu. Nilikuwa nachukua *sociology*.

**IS**: *University of Dakar* ulikuwa unachukua *sociology*?

**KNM**: Eeh, sasa *social psychology* ni sehemu ya masomo kama *programme*. Sasa kuna suala zima la mimi nili*specialise* katika *opinion polling*. Mambo haya wanayofanya kama ya [..…] Sasa pale Wafaransa wana *French Institute of Political Opinion*. Ile iko chini ya *Faculty* ya *Social Psychology*. Wakati ule profesa wake alikuwa Mpolish mmoja, waliokimbia huko zamani. Sasa profesa wangu wa Dakar alikuwa jamaa yake. Nadhani na yeye yule Mpolish maana yake jina lake Fugerolas, ni la Kipolish. Kwa hiyo akani*attach* kule miezi minne. Kwa hiyo muda wote kwa miaka sita na nusu nilikaa Senegal. Kwa hiyo nimekaa sana, nimepapenda.

**IS**: Kwa hiyo ilikuwa miaka sita na nusu kumaliza *degree* yako?

**KNM**: Kwa sababu kwanza nilikuwa sijui Kifaransa. Kwa hiyo ikabidi nifanye masomo *parallel*, ya Kifaransa na masomo yangu yale. Mwanzoni haikuwa rahisi kufuata *lectures* sawa sawa. Lakini nika*catch up*. Kwa hiyo tuseme miaka *full* hasa mitano.

**IS**: Na ulimaliza *degree* yako?

**KNM**: Nilimaliza, na walinitaka mimi nifanye wanayoita *doctorat du troisieme circle*. *Third cycle*, na nilikuwa *registered*.

**IS**: Wakati huo unasoma pale uliendelea kuwa na mawasiliano na chama hapa?

**KNM**: *Oh yeah*, *of course*, ndio.

**IS**: Kwa hiyo maana yake ni kwamba tarehe tisa wakati wa uhuru hukuwepo wewe hapa?

**KNM**: Sikuwepo, nilikuwa Dakar.

**IS**: Wakati wa *republic* sitini na mbili hukuwepo?

**KNM**: *No*.

**IS**: Muungano *sixty-four*?

**KNM**: Sikuwepo, mimi miaka yote hiyo sikuwepo. Mimi nimerudi *December* mwishoni *sixty-six*.

**IS**: *December* mwishoni *sixty-six!* Baada ya kumaliza masomo na kupata *degree*?

**KNM**: *Yeah*. Sasa walionivuruga ni watu wangu wa TANU kwa sababu niliporudi mimi nilikuwa tayari kule, nimechukuliwa nianze *research*. Na wameshanilipia na pesa kabisa, tena wakaniwekea benki. Sasa niliona nije kwa sababu nimeshakaa muda mrefu. Na mama yangu alikuwa analalamika kweli, halafu nirudi kwa profesa wangu tuweze kuelewana vizuri namna gani nitafanya na … Kufika hapa wote hapa wakasema hapana.

**IS**: Hiyo *December sixty-six* sasa tunazungumzia?

**KNM**: Niliporejea, ndio. Wanasema bwana lazima ukafundishe Kivukoni kwa sababu...

**IS**: *So* uliporudi ulikutana na Mwalimu?

**KNM**: *Oh, yeah*. Na kwanza Mwalimu tulikutana katikati, *sixty-four*.

**IS**: Alikuja kule…?

**KNM**: Alipita Dakar. Na Senghor, Rais Senghor alifurahi sana. Mwalimu alikuwa anakwenda Conakry kwa hiyo akasimama pale. Kwa hiyo aah, Senghor akasema nikae naye ili nionane naye rais wangu. Kwa hiyo alipokuja Mwalimu tu akamwambia ‘Lakini nna wanafunzi wako hapa.’ Akasema (Mwalimu) ‘Eeh?’ Mwalimu alikuwa hakumbuki vizuri. Nikaitwa pale. Anasema ‘Ah! We Ngombale uko hapa? Si tulikupeleka Liberia?’ Nikamwambia mbona tulikwishakuarifu Mwalimu. Akasema

‘Ah! Ndio, ndio. Kwa hiyo wewe uko hapa?’ Senghor akafurahi sana. Akasema ‘Unajua mwanafunzi wako huyu mtu mzuri sana. Anajua Kifaransa vizuri, anajua mambo yetu mazuri sana.’ Halafu akatuacha mimi na Mwalimu tuzungumze peke yetu. Senghor *was very nice*. Akaniuliza masuali, Vipi? Utarudi lini? Nikamueleza. ‘Basi bwana sie tunakusubiri.’ Lazima nirudi. Na mimi nilifurahi sana.

Niliporudi tu *of course* Mwalimu alipata taarifa. Kwa hiyo tukakutana hapa hapa kwenye chama. Basi, na kwa kuwa… kukawa na *pressure* kubwa lazima ukafundishe kwa sababu wanasema kule hakuna Mtanzania *qualified* kufundisha. Sasa na sisi tungependa wale… unakumbuka pale walikuwa wazungu watupu?

**IS**: Kivukoni? Ndio.

**KNM**: Ah, *pressure* kweli kina marehemu Anangisye, wakati ule Katibu Mkuu wa *Youth league*. Mzee Kawawa…

**IS**: Anangisye alikuwa Kivukoni wakati ule?

**KNM**: Katibu mkuu wa *TANU Youth League*.

**IS**: Lakini wewe ulikuwa unamfahamu kabla Anangisye?

**KNM**: Anangisye sikumfahamu kabla lakini mara nilivyokuja tu wote wakaja. Si walipata habari zangu na wanaambizana. Basi *pressure* ikawa kubwa mno ndio maana nikasema sasa… basi. Tena wao wakafanya mpango, sijui ndio Mzee Kawawa kwenda kuzungumza na *principal* wa Kivukoni wakati ule yule Mkanada. Ananiambia bwana anakusubiri ameomba kukuona.

**IS**: Alikuwa Cunningham?

**KNM**: Cunningham. Nikaenda kumuona Cunningham, nilivyomuona tena yeye ndio akawa *campaigner* mkubwa. Akasema ‘Lazima, hii lazima naenda kumwambia Mwalimu, lazima. Hii habari ya *research* yako sawa. Tukuchukue angalau *part time*.’ Ndio nikaenda.

**IS**: Sasa mimi naona hapa labda bila shaka utakuwa umechoka. Next time tutaanza na Kivukoni sasa, unaonaje?

**KNM**: Si ndio ulisema ndio ya mwisho hiyo?

**IS**: Kwa sababu hatujaja kwenye mambo mengi sana. Kwa sababu kuna suala zima la Azimio la Arusha na baadaye… kwa sababu Mwalimu hatujamzungumza kabisa itakuwa ni baada ya hapa.

**KNM**: Ndio maana nilikuwa nasema si tumzungumze Mwalimu maana yake mimi hii sio *biography* yangu, ya Mwalimu.

**IS**: Sawa, lakini leo tumepata *background* nzuri tu katika *context* yake. Sasa wewe sijui unaonaje, tupange lini ili tuweze ku… Kesho una nafasi?

**KNM**: Kesho Jumatano?

**IS**: Jumatano, kesho ni sikukuu mi naona. Tarehe nane *August*, Nane Nane.

**KNM**: Nane Nane. Na mimi nilikuwa na jambo, hata Alhamisi nina jambo. Tufanye Ijumaa.

**IS**: Ijumaa sawa.

**KNM**: Tufanye Ijumaa.

**IS**: Kwa hiyo saa hizo hizo saa tano?

K**NM**: Saa tano eeh.

**IS**: Asante sana Mzee.

**KNM**: *Yeah*, mimi nashukuru

## 10 Agosti 2012

**IS:** Sawa. Mimi naona, Mzee, tuanze moja kwa moja kwa sababu mara ya mwisho ulinieleza ulirudi kutoka Liberia mwezi wa Desemba mwishoni. Na sasa ndio…

**KNM**: Nikaenda Kivukoni.

**IS**: Sasa hiyo ya Kivukoni ilitokeaje?

**KNM**: Wenzangu katika Chama walinishauri sana, kama vile, nikazibe pengo pale – nikubali kwenda kufundisha kule *political science*.

**IS**: Unaposema 'wenzangu' unamaanisha nani na nani hasa?

**KNM**: Nasema katika Chama.

**IS**: Wakati huo Oscar Kambona alikuwepo?

**KNM**: Oscar alikuwepo lakini sikuwa karibu nae, kwa hiyo yeye hakuhusika. Lakini Mzee Kawawa alihusika; katibu mkuu wa vijana, huyu marehemu Anangisye; na wenzangu niliokuwa nao Liberia, wao walikuwa wamesharudi wako kwenye Chama – akina Mapunda, akina Kisenge. Kwa hiyo kulikuwa na *pressure* kubwa, kwa hiyo *in fact somebody* akafanya *appointment* na *Principal* wa Kivukoni, wakaja kuniambia, 'Bwana una *appointment*, nenda kazungumze nae *Principal* Cunningham'. Nikasema, 'Aah! Safi'. Nikaenda nikazungumza nae, nikazungumza nae muda mrefu, tukaelewana, na yeye akawa anataka sana niweze kwenda kufundisha pale. Yeye nilimweleza vilevile *problem* yangu kwamba mimi nimeji-*register University of Dakar* kufanya *research;* sasa wale wamenipa na *full scholarship,* nimekuja tu nyumbani niweze ku-*touch base,* nielewe mambo yalivyo halafu vilevile itanisaidia katika kukamilisha mpango wangu wa *research* na profesa wangu. Kwa sababu yeye alitaka kujua kama ninataka kufanyia hapa nchini ama kufanyia kulekule *West Africa*. Kwa hiyo yeye ali-*propose* akasema, 'Katika hali hiyo basi uwe *half-time* profesa, sio *full*

*time* kabisa, *twenty-four hours*.' Basi nikasema, 'Basi vizuri'. Kwa hiyo nikaenda kwenye *interview*, nikafanya vizuri sana.

**IS**: Kwenye *interview* alikuwepo nani?

**KNM**: Bodi ya Kivukoni, ambayo mwenyekiti wake alikuwa Mzee Kawawa na miongoni mwa wajumbe kulikuwa na Katibu Mkuu wa *TANU Youth League*; Mwenyekiti wa *CUT, Cooperative Union of Tanzania,* wakati ule ilikuwa *of Tanganyika* nadhani; na wengine siwakumbuki vizuri.

**IS**: Na Mama Wicken alikuwepo?

**KNM**: Wicken alikuwepo.

**IS**: Hii ilikuwa ni mara yako ya kwanza kuonana na Mama Wicken?

**KNM**: Eee, ndio. Ingawaje nilikuwa nazijua habari zake. Basi [*interview*] ikaenda vizuri, ndio nikaanza kufundisha Kivukoni. Na pale Kivukoni tulikuwa na *community* ya walimu – *lecturers* walikuwa karibu wote ni *expatriates* kutoka Uingereza, *Ireland*, Ujerumani, *Canada* na Marekani – *United States of America*. Na wakati ule kulikuwa na mmoja Mganda, toka Uganda. Na nilikuta *lecturer* mmoja ambae amechukuliwa tu lakini amepewa *leave* ya kwenda kuchukua diploma katika *adult education*, ndugu David Mwakawago, alikuwa Uingereza. Kwa hiyo mimi nilikuwa *lecturer* wa pili, katika maana hiyo, Mtanzania.

**IS**: Walikuwa wanafundisha nini hasa?

**KNM**: *Social Sciences especially*. Kivukoni kilikuwa ni chuo cha kawaida cha *social sciences*, cha kiwango cha kati, sio *university level*. Na tulikuwa tunachukua watu ambao wameonyesha uwezo mkubwa katika jamii katika kazi mbalimbali, na wamepata msingi wa elimu, kama sekondari, lakini walikuwa hawana sifa za kwenda chuo kikuu.

**IS**: Waliokuwa wanachukuliwa ni wanachama tu?

**KNM**: Pale mwanzoni hapakuwa na *qualification* ya uanachama, kwa sababu tulikuwa hatujawa chuo cha chama kama unavyotegemea. Ilikuwa ni chuo cha sayansi za jamii, lakini walio wengi walikuwa wanachama kwa sababu kwamba waliokuwa wanachukuliwa sana – kwa mfano, walimu kutoka nchi nzima – chuo kilikuwa kimeibua utaratibu wa kujitangaza na kuweka siku za kufanya usaili wa wanafunzi. Lakini hizo siku zilikuwa huko huko mikoani, na wale wahadhiri wa pale walikuwa wanatawanyika kwenda mikoani kuwasaili. Kwa hiyo waliweza kuwapata watu wa aina mbalimbali kutoka mikoani kabisa. Sasa, wengi wao walikuwa walimu lakini watu wengine walikuwa ni watu wanaojitegemea tu – mtu amesoma halafu ameamua kuwa mkulima, lakini sasa anataka kujiendeleza kidogo, kwa hiyo ameomba. Sasa, katika usaili ule anaweza akaonekana kwamba ana sifa nzuri sana, wanakuja wanamchukua, wanamwona anafaa. Kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba kulikuwa na watu wenye historia za aina mbalimbali na vilevile wenye vipaji vizuri sana. Kwa hiyo, ndiyo namna hiyo waliweza kupatikana akina marehemu [Henry] Mapolu. Manake yeye alikuja kuanza Kivukoni kama mwanafunzi, 1966.

**IS**: Hiyo ilikuwa ni 1966? Kwa hiyo wewe ulimkuta pale?

**KNM**: Nimemkuta pale, sasa akachukuliwa, mimi nimekuja mwishoni. Akachukuliwa *sixty-seven* kama *assistant tutor*. Yeye na Mangula walikuwa *batch* moja. Walikuwa wote wanafunzi *sixty-six*, halafu wakachukuliwa kama *assistant tutors*. Kwa hiyo ndio nikaanza hapo lakini sasa haikuchukua muda nianze tu kufundisha, manake nimechukuliwa tu nimeanza mwezi ule ule wa Januari *sixty-seven*. Mwisho wa mwezi, Halmashauri Kuu [ya TANU] imepitisha Azimio la Arusha.

**IS**: Mwezi Februari?

**KNM**: Januari mwishoni.

**IS**: Sawa, tuendelee Mzee. Enhee, kwa hiyo ikatokea mwishoni mwa mwezi…

**KNM**: Mwezi wa Januari mwaka 1967, nadhani tarehe 28 ile, Halmashauri Kuu ya Taifa ya TANU ikapitisha Azimio la Arusha, ambalo halikutangazwa mpaka tarehe 5 Februari.

**IS**: Sasa kabla hujaendelea, tuseme wewe ulipoenda Kivukoni kulikuwa na fununu yoyote – wewe ulipata ufununu yoyote – kwamba kutakuwa na kitu kama hicho?

**KNM**: Hapana. Kulikuwa na fununu baada ya NEC ya Arusha ilipokutana; aah, ndio sasa fununu zikatoka kwamba Chama kitatangaza sera mpya. Na ndio maana tukatafutanatafutana, sera mpya ya ujamaa na nini, kwa hiyo ndio maana na mimi nilitoka Kivukoni kwenda kwenye mkutano wa hadhara huko ambako Mwalimu alitangaza…

**IS**: Hiyo ni tarehe 5 sasa?

**KNM**: Tarehe 5, yah.

**IS**: Mkutano wa hadhara ulikuwa wapi?

**KNM**: Mnazi Mmoja. Sasa kwa hiyo, baada ya kupitishwa Azimio la Arusha, na katika Azimio lililohusu uongozi, manake Azimio lina sehemu mbili: kuna upande wa sera – siasa ya ujamaa na kujitegemea – na pili, miiko ya viongozi, ndio Azimio. Sasa upande ule kulikuwa na agizo kwamba viongozi wafundishwe siasa ya Chama kuanzia Azimio lenyewe la Arusha. Kwa hiyo, uamuzi huo ukaathiri vilevile maudhui ya mafunzo katika chuo cha Kivukoni katika maana mbili: moja ni kwamba walimu, hasa mimi niliyekuwa mwalimu wa Kitanzania wa siasa, ilinibidi nihusike sana na suala la mafunzo kwenye Chama. Na hiyo ilikuwa ni kwa agizo lake mwenyewe Mwalimu kwa sababu katika kutekeleza lile Azimio, ilibidi kuanza kuwafundisha mabalozi wa nyumba kumi wa Dar es Salaam Azimio la Arusha na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Na Mwalimu wakati ule, nadhani Ikulu ilikuwa inafanyiwa ukarabati, alikuwa anafanyia kazi moja kwa moja ofisi ndogo ya Chama hapo Lumumba. Sasa mimi nilikwenda pale Lumumba, sio kwa ajili ya kumuona Mwalimu, lakini kwa kuzungumza na makada pale. Sasa

Mwalimu alitoka, ilikuwa kama saa kumi ama kumi na nusu, na mimi nilikuwa nataka kuondoka; aliponiona Mwalimu akasimama, akageuka, akaniita: ‘Mwalimu Ngombale, hebu njoo’. Akawauliza maafisa wa pale, ‘Suala hili la kufundisha mmemhusisha mwalimu Ngombale?’ *Of course* walikuwa hawajawa na *programme* wakasema, ‘Tutamhusisha’, likaisha. Likaishia hapo, akaondoka.

**IS**: Unajua hiyo ilikuwa mwezi gani?

**KNM**: Aaah! Mwanzoni sana. Nadhani ni Februari hiyo hiyo kwa sababu tulianza kuwafundisha mabalozi mapema sana, mwezi Februari huo huo. Sasa, katibu wa itikadi wakati ule aliteuliwa Reverend Mushendwa, ambaye ni *classmate* wangu Tabora. Tulikuwa wote *Tabora School*, tena tulikuwa tunaishi bweni moja. Sasa, Rev. Mushendwa alikuwa mjanja kweli, kwa hiyo akanipigia simu Kivukoni anaomba kuniona. Nikafika pale akaniambia, ‘Bwana, mimi nataka kukuona kwa sababu wewe rafiki yangu tuko marafiki tangu kule shuleni. Nataka utusaidie, tunatakiwa leo tupitishe *syllabus* ya kufundisha mabalozi wa nyumba kumikumi Ujamaa na Kujitegemea kwa mujibu wa Azimio la Arusha. Sasa bwana, njoo utusaidie’. ‘Mkutano saa ngapi?’ ‘Mkutano saa kumi’. Kwa hiyo, saa hizo saa tano na mimi nikasema basi ngoja nikae tu nijaribu. Tukajaribu pale haraka haraka tukapata *draft* ya mambo ya kuwapa, manake hawa ni mabalozi, kwa hiyo ni mambo ya kuwahimiza tu katika fikra za kijamaa. Kwa hiyo tukaenda kwenye mkutano saa 10, wadau wakubwa tukaunganishwa pale, *of course* mkutano haukuwa mwepesi, ulikuwa mgumu kwa sababu waliokuwa wanaamini wanajua mambo ya kufundisha walikuwa wengi lakini *finally* tukakubaliana jambo la msingi.

**IS**: Ile *syllabus* ilikuwa imeshakuwa *drafted*?

**KNM**: Ndio, tulimaliza kui-*draft* ikawa *presented* pale.

**IS**: Walio-*draft* ni …?

**KNM**: Ni mimi, sasa si ndio waliniomba nii-*draft,* lakini nilikuwa naye Mshendwa, na Gisler Mapunda, tukamaliza tukapeleka. Tukaenda kwenye mkutano wa wote. Sekta kubwa iliyowakilishwa pale ni upande wa *commissariat* ya jeshi kwa sababu nao walikuwa wanafundisha *political education.* Tukabadilishana mawazo pale, mwisho tukapata kitu kizima na baada ya pale wiki iliyofuata tukaanza mafunzo ya mabalozi. Tuliandaa timu ya makada ambao walipata mwelekeo, *orientation*, kwa kutumia ileile *syllabus.* Kwa hiyo, jioni baada ya kazi ndio walitawanywa – Magomeni, Ilala, Temeke, na kadhalika – kwenye matawi ya Chama, wanazungumza na mabalozi. Na mpango wetu ulikuwa kila Jumamosi asubuhi, wakati Mwalimu yupo Dar es Salaam – huo mpango alipanga mwenyewe – wale makada wote walioshiriki katika mchakato huo wa kutoa mafunzo kwa mabalozi, tulikuwa tunakutana Ikulu, kwake, kumpa taarifa juu ya mwenendo wa mafunzo na kama kuna matatizo mbalimbali.

Kwa hiyo hilo moja, lakini kwa upande wa Kivukoni, Mwalimu kama mwenyekiti wa Chama wa Taifa akaagiza tuanze kufundisha viongozi siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kwa mujibu wa Azimio la Arusha. Alimpa maelekezo mkuu wa Chuo, Cunningham, na kumwambia, 'Hiyo kazi mkabidhi Ngombale aandae *programme,* naleta viongozi'. Na viongozi wa kwanza aliowaleta ilikuwa ni wenyeviti wa matawi ya Dar es Salaam yote wakati ule. Wakati ule matawi hayakuwa mengi sana. Kwa hiyo, ikabidi sasa kukaa na kuandaa *syllabus* – walileta pale kwa wiki mbili – sasa kuandaa *syllabus* ya kufundisha wazee wa Chama hao kwa wiki mbili. Sasa tulikuwa na tatizo kwa sababu, kwanza, hakuna aliyesomea ujamaa (*socialism*), hakuna. Sasa mnapoambiwa mfundishe ujamaa lazima mtulize kidogo vichwa vyenu ili muweze kutazama mambo gani mnaweza kuyachukua kwamba ndiyo mambo ya kuwafundisha watu. Na hawa watu [ni] watu wa kiwango gani cha uelewa?

Lakini la pili, watu wetu hapa walifundishwa Kiingereza; waliokwenda sekondari na vyuo vikuu wamesomea kwa Kiingereza. Sasa hawa wanaokuja hawa unatakiwa uwafundishe kwa Kiswahili. Sasa hiyo kazi ilikuwa sio kazi ndogo. Lakini vilevile ziko dhana ambazo hatukuwa nazo katika Kiswahili; ziko katika Kiingereza. Lakini lazima ufikishe ujumbe ule kuwa dhana ile inasema nini [katika] Kiswahili. Kwa mfano, suala la *nationalization;* kwa sababu tarehe 5, pamoja na kutangaza Azimio la Arusha, Mwalimu alitangaza utaifishaji wa shughuli fulani fulani za kiuchumi. Sasa, '*nationalisation'* wakati ule hatukuwa na neno moja, kwa hiyo tulianza na '*fanya mali ya taifa*' – ndiyo lugha ya mwanzo tuliyoanzia nayo. Kwamba katika kuchukua hatua za kuanza kuelekea ujamaa tunachukua hatua za kufanya mabenki yawe mali ya taifa, kwa hiyo *aim* yake ni kufanya mali ya taifa. Ni baadaye, palepale Kivukoni, watu wakapata kitu – '*kutaifisha'*, na *process* ilikuwa inaonekana inavyokuja, maneno mapya yanajengeka kuelekea dhana fulani fulani.

**IS**: Ninyi mlikuwa wangapi mliokuwa mnafundisha pale?

**KNM**: Mwaka ule wa '67, baada yangu mimi, walikuja walimu wapya; mmoja namkumbuka, mwalimu Kazimoto, alikuwa mwalimu wa uchumi kutoka Chuo Kikuu. Sasa kwa mwanzoni tulikuwa tunafundisha zaidi mimi na yeye.

**IS**: Na mlikuwa mnatumia Azimio tu?

**KNM**: Kwa ajili ya wenyeviti tulikuwa tunatumia Azimio na *documents* zingine *relevant* za Chama lakini tulipomaliza na wenyeviti, tukawa tumepata na ka-*experience* zaidi kidogo, Mwalimu akawaleta vijana wa jeshi – Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, ili kuwajenga kuwa walimu wa siasa. Kwa hiyo tuliwafundisha makamisaa wasaidizi wa kwanza kama kuanzia mwezi Machi. Na hao ilikuwa *programme* yao – kwanza aliagiza wakae wiki mbili, lakini baada ya wiki moja wale vijana wakakutana wakafanya *caucus* yao wakasema, 'a-a, lazima tuombe tukae hapa muda mrefu'. Kwa hiyo Mwalimu

akapelekewa *message* na Mkuu wa Chuo, Cunningham, kwamba, ‘Wanafunzi wako wanakuomba muda uliopanga wa wiki mbili hautoshi’. Kwa hiyo nadhani walikaa wiki sita; tukarekebisha upya *syllabus* tukakaa nao wiki sita. Kwa hiyo timu nzuri, kubwa, ya makamisaa wa mwanzo, kwa kweli ndio makamisaa wa kwanza ambao walikuwa wamepata maandalizi rasmi ya kuwa walimu wa siasa katika majeshi.

Sasa, bahati nzuri pale Kivukoni palikuwa na aina mbili za masomo: muda mrefu ilikuwa ni miezi tisa na muda mfupi miezi mitatu, ukiondoa hizi maalum kama kwa maelekezo ya Mwenyekiti mwenyewe. Sasa kwa sababu mahitaji makubwa yalionekana kuwa ni ya kisiasa – kwa sababu Azimio la Arusha lilikuwa kama vile limechochea moto wa kisiasa, watu wanadai wenyewe huko mafunzo – kwa hiyo *short courses* zikaanza sasa kutumika zaidi kwa lengo la kuandaa viongozi, lakini wa kisiasa. Baada ya mwaka mmoja na nusu yalitokea mambo mengi, Kivukoni ikawa imebadilika na mvuto wake katika jamii uliongezeka sana. Mimi ikabidi niondoke Kivukoni kwa sababu kulianzishwa *Movement* – the *Pan-African Youth Movement* – ambayo, baada ya kuundwa kwa OAU baadae ikaonekana ni vizuri kuunda *movement* ya vijana lakini yote haya kwa lengo la kuunga mkono nguvu za kusaidia ukombozi wa Afrika. Tanzania ilikuwa imeteuliwa kushika ukatibu mkuu, sasa wenzangu katika *Youth League* wakaona mtu anayeweza kwenda huko ni mimi ingawa mimi wakati ule nilikuwa siko tayari kwenda kwa sababu, kwanza, wakati ule nilikuwa naupenda sana ualimu na *rapport* na wanafunzi. Nilikuwa nadhani nafanya kitu chenye matokeo makubwa na ndio maana nilikuwa nafundisha *part time* lakini wanafunzi walipogundua kwamba siwezi kutumia muda zaidi wa kuwa nao madarasani kwa sababu nina mambo mengine ya kufanya wakaanza *agitation*, *pressure* kubwa sana kwamba, ‘Hapana, lazima uchukue masomo zaidi ama muda zaidi katika masomo yako’. Sasa walimu, *lecturers* wa *political science* tulikuwa wawili – mimi na mama mmoja wa Kiingereza, mama mmoja hodari sana.

**IS**: Unaweza ukakumbuka jina lake?

**KNM**: Eee mama Belle Harris. Belle Harris, *nice woman*, mwalimu mzuri. Sasa wanafunzi wakaweka *pressure* kabisa wanasema, 'Hii haiwezekani'; eeh! ikawa ngumu sana. Wakati ule, Mwalimu alikuwa anakuja sana Kivukoni kuzungumza na vijana, wanafunzi. Na *sessions* zile zilikuwa nzuri sana kwa sababu wanamuuliza masuali juu ya *socialism* na nini, na Mwalimu ni mtu aliyekuwa na kipaji kikubwa sana cha kuelezea mambo kwa sababu uelewa wake ulikuwa mkubwa. Sasa wanaingiza lile, 'Sasa Mwalimu, kwa nini mwalimu wetu anafundisha nusu muda? Tunajua anataka kwenda kufanya udaktari, sijui nini, lakini hapa mahitaji ya hapa…' Wanafunzi walikuwa wanafanya kana kwamba mimi sina *interest* sasa ya hapa. Sasa, Mwalimu bwana, mjanja, akasema, 'Zungumzeni nae mwalimu wenu. Sasa mnaniambia mimi, nimpe amri?' Basi alikuwa na kipaji kikubwa sana! Mwisho ikabidi tukubaliane kwamba bora niache, ni-*postpone* kazi yangu ya Dakar, tuendelee hapa.

Sasa kwa hiyo nilikuwa napenda sana kazi ya kuzungumza na watu, lakini *Youth League*, Katibu Mkuu alikuwa Joseph Nyerere, rafiki yangu…

**IS**: Joseph Nyerere alikuja baada ya Anangisye?

**KNM**: *Oh yes*! Alirudi tena. Unajua yeye alikuwa huko nyuma Katibu Mkuu, akaacha, ndio akaja Anangisye. Sasa baada ya Anangisye kuondolewa ndio akaja Joseph.

**IS**: Sasa hebu tuzungumze zaidi kidogo, baada ya Azimio la Arusha Anangisye aliondolewa na Oscar Kambona pia akaondoka. Kuhusu haya matukio mawili haya – Anangisye na Oscar Kambona – unachokumbuka wewe ni nini au ulikuwa unafahamu kilichotokea ni nini?

**KNM**: Mimi ninachojua ya Kambona ni ya kuondoka. Anangisye… tena juzi nilikuwa na *veterans* wa *TANU Youth League*, mmoja wao ndio alikuwa ananikumbusha akaniambia,

‘Unakumbuka? Sisi ndio tuliokwenda kushusha bendera ya Mfalme!’ Baada ya kutaifisha mabenki, *Youth League* walijipa kazi, wao wenyewe walikuwa wanaamua, kupita kutaka ku-*check* kwamba kweli haya majengo ama hizi taasisi kweli zetu ama sio zetu. Sasa, kuna benki – nadhani ilikuwa ya Uholanzi, si wana mfalme wale? Ni Waholanzi ama Wadenishi? Nadhani Waholanzi. Wakaenda, wakakuta picha ya Mfalme wao. Wakaiporomosha chini. Sasa ile *incident* ikawa ya kisiasa, wale waliohusika pale kwenye *institution* ile wakalalamika serikalini kwamba mtawala wao, wa nchi yao, amevunjiwa heshima. Sasa Anangisye kama *secretary general* alitakiwa aka-*apologise.*

**IS**: Ila Anangisye mwenyewe hakuhusika moja kwa moja?

**KNM**: A-a. Ilichukuliwa tu kwamba, kwa sababu yeye ndiye mkubwa wa *Youth League*, kama hakuhusika kama kahusika *directly*, aka-*apologise*. *In fact* alisema kwamba hakuwepo katika kundi lile. Sasa, taarifa zilizokuwepo wakati ule ni kwamba kakataa. Sasa hiyo ndiyo ilimchefua Mwalimu: ‘Hii ni *diplomatic incident*, sasa wewe unakataaje? Wewe una-*represent* vijana wa Chama chetu, sasa unataka sisi kama taifa tu-*apologise*?’ Ndiyo, hiyo *incident* ilikuwa katika *light* hiyo.

Ya Kambona, yeye alifanya maamuzi yake ya kuondoka. Inaelekea hakukubaliana na Azimio la Arusha.

**IS**: Fununu ilikuwa nini, kwamba alilipinga Azimio katika mkutano?

**KNM**: Rafiki zake wanasema alikuwa anapinga chinichini. Si jasiri sana. Sidhani kama alikuwa na uwezo wa kutoa *arguments* za kupinga lakini alikuwa hodari wa kuzungumza na watu. Na hasa miiko ya viongozi, enh. Kwa hiyo, pengine alikuwa na mambo yake mengine manake mimi sikuwa katika *leadership*, wakati huo mimi nilikuwa mwalimu tu wa Kivukoni. Ndio akaondoka.

**IS**: Si umesema kwamba wakati huo, tuseme ’67, wewe ulikuwa Kivukoni mpaka ’68?

**KNM**: Ee, mpaka ’68.

**IS**: Okay, ’67 na ’68, Mwalimu alikuwa anakuja sana pale Kivukoni.

**KNM**: Ndiyo.

**IS**: Sasa katika mazungumzo yake na wanafunzi pale na walimu, unaweza kukumbuka hasa alikuwa anaegemea upande gani katika ufafanuzi wake alivyokuwa anazungumzia nadharia ya ujamaa?

**KNM**: Aah! Sasa unajua Azimio lina, katika sehemu yake ya nadharia ya ujamaa, suala la unyonyaji na kadhalika. Kwanza aliyekuwa akija pale Kivukoni si Mwalimu peke yake. Viongozi wengine nao walikuwa wakipata nafasi wanakuja, na wakati mwingine walikuwa wanaalikwa. Sasa mimi nikiwa mwalimu pale nilikuwa na matatizo sana. Wale viongozi wengine karibu wote wanavyokuja kwa sababu wengi walikuwa wanasigana na wanafunzi. Sasa kwa sababu wanafunzi wanayakubali mafunzo ya ujamaa, na tulikuwa tunatumia – msingi wetu ulikuwa – Azimio la Arusha, pamoja na kufafanua.

**IS**: Lakini mlikuwa mnagusia historia ya *socialism* na hao wengine wafuasi kwa mfano akina-Marx, mlikuwa mnawafundisha?

**KNM**: Ehee, ndio. Na aina ya wajamaa duniani. Tunaeleza, wale wa *revolutionary* wanasimama wapi, wanataka nini; hawa *evolutionary socialists* wanataka nini, wanataka kutengenezatengeneza kidogo lakini *system* iliyoko pale ibaki *intact*. Aaa, tulikuwa tunafundisha, lakini nasemaje yale mawazo ya msingi yale ya kupinga unyonyaji, suala la umiliki na uundaji wa sekta ya umma, suala la wafanyakazi na wakulima kuungana katika kuhakikisha kwamba madaraka haya yanatumika kusogeza mbele maslahi yao. Lakini walipokuwa wakija viongozi wengine wengi kulikuwa na ushindani na wanafunzi: wanafunzi wanakuwa *idealists*, wanataka mabadiliko sasa. Sasa wakubwa wanaona kama wanakuwa *criticized* wao kwa hiyo wanavyojibu ama kujieleza inaleta zogo manake na wao wanafunzi wanaanza

kutokubaliana nao. Kwa hiyo, mara nyingi walipokuja viongozi walio wengi mimi nilikuwa napata tatizo kidogo manake ilikuwa inanibidi wakati mwingine niingilie kati ili nisaidie, ama nimsaidie mgeni aliyekuja ama niwasaidie wanafunzi.

Lakini alipokuwa akija Mwalimu, sikuwahi kuwa na tatizo hata mara moja. Kwamba atatoa majibu yanayotofautiana na [ambayo] mimi ningetoa haikutokea hata mara moja. Kwa hiyo anapokuja Mwalimu nilikuwa kabisa nimetulia, vijana wanauliza.

**IS**: Lakini pamoja na [hayo], mtazamo wenu haukuwa *exactly the same*, siyo? Kwa mfano, mtazamo wako ni sahihi kusema kwamba ulikuwa ni wa Ki-*Marx*, Mwalimu *of course* sio moja kwa moja alikuwa na mtazamo wa Ki-*Marx*. Kwa mfano suala zima la mapambano ya kitabaka. Katika hili je?

**KNM**: Aah! Sasa lingekuja kama suali ningemsikiliza Mwenyekiti anavyojibu kwa sababu mara nyingine alikuwa ananitupia mimi nijibu. Kwa mfano, acha tu Kivukoni, nilipokuwa Mkuu wa Mkoa nilimpangia kutembelea matawi ya sehemu za kazi kwenye viwanda, na wakati ule tulikuwa tumeanzisha ulinzi wa Mgambo baada ya Mwongozo ya 1971. Kiwanda kimoja cha nguo cha Mchina mmoja, baadhi ya wafanyakazi wakamuuliza suala *tricky* kidogo manake wanasema, 'Ninyi mnaruhusu wananchi tufundishwe silaha kulinda nchi yetu na wanaotufundisha ni wanajeshi. Sawa. Lakini huko nchi nyingine huko wanajeshi hao hao ndio huwa wanabadilika hao wanataka kuondoa ile serikali iliyochaguliwa na wananchi ili wakae wao. Sasa hapa je, ikitokea hivyo, sisi nafasi yetu ikoje?' Eh! Eh! *Quiz* kubwa! Sasa, *of course*, Mwalimu akasema, 'Aah! Muulizeni katibu wenu wa mkoa. Mwambieni. *Comrade,* hebu wajibu'. Sasa sikumbuki nimewajibu vipi lakini hatukugongana, manake niliwafanyia *analysis* nilipomaliza, Mwalimu aka-*take up,* akapanua zaidi. Tukawa tumekwenda vizuri kabisa.

Sasa, suala la *Marxism*, mimi unajua niliamua tangu mwanzo. Kwanza nilishukuru sana kwamba nilikuwa na bahati nzuri. Nimerudi, na mara Azimio la Arusha linatangazwa. Na ukilisoma

linakupa *framework* nzuri kwa sababu ni *progressive document* ya watu ambao wanataka ku-*move forward*. Na mimi katika ile *paper* niliyoandika katika *MBIONI*, *analysis* yangu ilikuwa ya Ki-*Marxist*. *In fact* wale ma-*lecturer*, hasa wa Kimarekani tuliokuwa nao pale Kivukoni, wako wawili hao, mmoja msichana na mwenzie. Walikuwa vijana kama mimi wakati ule, akanifuata akaniambia, '*Why are you putting your neck so openly. Don't you think that you are exposing yourself*?' Nikawaambia, '*No. I can't hide my true self. Those who don't agree with me, they are free to criticize me*'.

Sasa nasema lakini mimi ni tangu mwanzo niliamua kwamba, kwa *framework* hii ya Azimio la Arusha, tunaweza tukasukuma mabadiliko ya nchi yetu na tukizingatia kwamba *level of development* ya *productive forces*, ambazo zina-*include* watu, bado iko chini. Kwa hiyo mkiwafikisha watu kwenye kuelewana kwamba unyonyaji ni *problem* na kwamba tutilie mkazo *cooperative effort* ya watu wetu, hilo mimi ntakwenda nalo, nitalisukuma sana. Na katika hilo, nikapata *encouragement* kubwa sana kwa Mwalimu. Mwezi *October sixty-seven* ile ile walimu wa Kitanzania tuliomba kuonana na Mwalimu, *in fact* mimi niliomba; nilipokubaliwa nikawaambia nakuja na walimu wenzangu. Kwa hiyo, tulikwenda kama walimu watano, yaani, *lecturers* tulikuwa wawili – mimi na Kazimoto – Mwakawago alikuwa bado hajarudi; na ma-*assistant tutors* akina marehemu Mapolu, hata huyu katibu mkuu mstaafu, Mangula, tulikwenda wote.

Sasa, kule mimi nilikuwa na mapendekezo *radical* hivi kuhusu elimu ya watu wazima: namna gani tuweze kutumia *educated population* iliyopo sasa hivi kujaribu ku-*educate* wananchi walio wengi angalau wajue kusoma na kuandika, na kadhalika. Sasa Mwalimu alikuwa na Wicken…

**IS**: Oh! Mama Wicken alikuwepo?

**KNM**: Alikuwepo. Wicken alikuwa anapinga, kila nikizungumza jambo alikuwa anakataa. Mwalimu anamwambia, '*No no no. Joan, wait, wait. Let him explain himself*'. Basi, tulizungumza

vizuri, nilikuwa na mawazo mengi kidogo. Akaniambia, ‘Unajua bwana, si unajua mimi hali yangu ni tofauti na watu kama Fidel. Fidel mwenzangu ana *rebel army*, ile ndiyo *base* yake, ndiyo ameweza kuitumia ile kushika nchi sawasawa na kuunda mazingira ya kuwa-*mobilise* watu wote waliosoma kwenda vijijini kufundisha watu na nchi haikuweza kuyumba. Kwa hiyo wamefuta ujinga kweli. Mimi lakini sina *rebel army* kama ya Castro’. Akasema, ‘Sina mimi *green guards* kama wale wa Mao Tse Tung’.

**IS**: *Red guards*!

**KNM**: Eee, *red guards* ee kama wa Mao Tse Tung. ‘Kwa sababu wale ndio *guarantors* wa nchi kutulia. Wewe una-*mobilise* nchi nzima lakini wale wapo, hakuna mtu anayeweza kuwachezea. Mi sina hao.’ Halafu akasema, ‘Halafu, *you will be surprised* hawa watu wetu walio wengi, pamoja na waliosoma mpaka vyuo vikuu, kuna mambo mengi sana hawajui. Hasa hili eneo la Ujamaa na nini, kabisa hawajui. Kuna mambo wanayaogopa tu. Kwa nini? Wameambiwa.’ ‘Kwa hiyo’, akasema, ‘Sisi tujipe kazi moja kwa sasa: kufundisha – kufundisha *leadership* ya Chama na ya Serikali ya ngazi zote, angalau tuelewane juu ya Ujamaa na Kujitegemea.’ Akasema, ‘Ukiweza kufanikiwa hilo utakuwa umejiwekea msingi mzuri wa kupiga hatua nyingine.’ ‘Kwa hiyo’, akatuambia, ‘ninyi sasa Kivukoni mmeanza vizuri kufundisha viongozi. Lakini sasa nitataka tuone namna ya kwenda nchi nzima.’

Ndiyo maana mwezi Desemba mwishoni akaniita mimi na Gisler – mimi nilikuwa Kivukoni, Gisler alikuwa kwenye Chama – kwa ajili ya kuandaa timu za makada za kwenda nchi nzima kwenye mikoa kuwafundisha Azimio la Arusha. Ndio tukaanza sasa *wave* ya kufundisha – *seminars* zile za kufundisha Azimio la Arusha nchi nzima. Kwa hiyo tukaenda, mpaka maaskofu tukakaa nao, mpaka wanajeshi tukakaa nao, viongozi – sijui ma-*administrative officers*, sijui ma-*RC* na nini... Hiyo ilikuwa ni *concept* yake. Na vyuo – chuo cha Chama kikafungua matawi – vyuo vya kanda, mpaka mwisho vikafika vinane; vyuo vya kanda vinane, yote

katika kutaka ku-*train leadership.* Kwa hiyo, katika hayo hatukuwa na tofauti kubwa hata kidogo.

**IS**: Katika mazungumzo yako na yeye, uliona kwamba alikuwa anasoma soma Marx na Lenin, na msimamo wake ulikuwaje? Mliwahi kujadili hili?

**KNM**: Mwalimu amesoma lakini asichokubaliana, mimi nilivyomwona, ni ile *Weltanschauung* wanasema Wajerumani – ile *world outlook* ya *Marxists,* ambayo ina-*include metaphysical questions* kwa sababu wanaamua vilevile masuala ya: Je, Mungu yupo ama hayupo? Sasa yeye akifika hapo anaona wana matatizo. Kwa hiyo, ndiyo maana nadhani yeye amechukulia *socialism* kwa msingi wa *world outlook* yake. Yeye ni muumini wa Kikristo lakini bila kuwa na *contradictions* za waumini wengine wa Kikristo – *he is more scientific*.

**IS**: Lakini ninyi *personally* hamkuwahi kujadili suala hilo?

**KNM**: No, no, kwa sababu anajua *position* yangu kwenye hili. *1970* tuliwahi kujadili *one aspect*, wakati ule [mimi] bado ni Katibu Mkuu wa *TANU Youth League.* Tumekutana kwenye NEC, Dodoma, sasa watu wanatoa ripoti, zinatolewa ripoti juu ya Ujamaa Vijijini. Na unajua, tulipoanza Ujamaa Vijijini ilikuwa hasa watu wanaanzisha shamba, wale washiriki wanajulikana. Sasa ikabidi waanzishe na utaratibu wa kujua *contribution* ya kila mtu. Sasa, Butiama wao wakaanzisha utaratibu kwamba mtu anayekwenda kushiriki kwenye shamba kwa kazi ya siku moja, anapewa kitu – waliita 'heshima'. Inaandikwa. Kama hushiriki, hukwenda, hupati. Kwa hiyo, zile heshima zinaorodheshwa kwa kila mtu, baada ya mavuno wanatazama mavuno yaliyopatikana na wanajaribu kuyagawa kwa wale washiriki, na wanayagawa kwa msingi wa heshima. Lakini, sasa ndio wakasema, wanatazama vilevile kila mtu katika hao walioshiriki familia yake ikoje: ina watu wangapi? Kwa hiyo mahitaji yao yatakuwa makubwa. Kwa hiyo, wangegawana kwa kutegemea mahitaji sio tena na ile heshima. Sasa akasema, 'Hii sawasawa hii'.

Sasa mimi nika-*raise objection,* nikamwambia, ‘Mwenyekiti, utaratibu huu ni mzuri sana kwa sababu unazingatia mahitaji ya watu katika kijiji. Lakini tunajenga Ujamaa. Ujamaa tunaoujenga ni wa nchi sio wa jadi ambao wa kutaka kutosheleza kuifanya jamii iendelee katika hali yake tu ya kawaida. Tunataka shughuli wanazofanya katika kijiji zitoe mchango vilevile katika kujenga Tanzania mpya. Kwa hiyo tunahitaji watoe ziada, na kama tunataka watoe ziada, tunataka kila mtu atoe mchango wake katika kuzalisha ambao unafanana na uwezo wake wa kweli. Lakini kama utaratibu wenyewe ni huu, hauwezi kumfanya kijana [ambae] hana mtoto lakini ana nguvu nyingi atumie uwezo wote alio nao kuzalisha kwa ajili ya kijiji. Kwa hiyo, kama nia yetu ni kuleta maendeleo ya kijiji na nchi, kugawana huku hakutufikishi mbali.’

Ah! Mwalimu akawa *interested*, akasema, ‘Sasa wewe unafikiri mambo yakoje?’ Nikamwambia Mwalimu, ‘Mimi ngoja niseme: wewe unawajua watu hawa ma-*Marxist.* Sasa, Marx, Engels hata Lenin na wenzao, wao walikuwa na mtazamo tofauti kwa kuogopa hilo hilo ulilolisema ambalo ni zuri kabisa katika *traditional society*, katika jamii ya kawaida. Ndio ilikuwa inafanyika hivyo katika *community societies* – unatazama mtu anahitaji nini manake ana *family* kubwa. Sasa wenzetu wanasema, ‘Ukitaka kuleta maendeleo katika nchi, katika hatua hii ya kutafuta nguvu ya kujenga Ujamaa – *Socialism* – kwa hiyo tutake kila mtu atoe mchango kwa jamii kulingana na uwezo wake.’ Kwa hiyo mkulima anayechangia pakubwa katika shamba la Ujamaa siku ya siku lazima uzingatie mchango wake ametoa kiasi gani. Na hivyo hivyo hospitali, daktari ambae anatoa mchango mkubwa zaidi mkitaka aendelee kutoa mchango huo mtambue kuwa mchango wake mkubwa anaoutoa katika hospitali ile. Msiseme kwamba nesi wake ana watoto ishirini, kwa hiyo mshahara mkubwa apate huyu nesi, daktari apate nusu kwa sababu ana watoto watano. Mtampunguza ari, ataacha kufanya kazi kwa kadri ya uwezo wake, na kidogo kidogo, hospitali yenu haitaweza kutoa [huduma]. Hivyo hivyo walimu…’

Akasema, ‘Sasa bwana, hiyo bwana haiwezekani. Sisi katika jamii zetu usipozingatia mzee fulani ana watoto wengi, mambo yote yataharibika’. Wakabisha sana pale lakini alipofunga kikao akaniita, akasema, ‘Ngombale, hebu twende’. Nikaenda nyumbani kwake. Akaniambia, ‘Hebu kaa. Hebu nieleze vizuri maelezo yako, hawa wanasemaje hawa jamaa?’ Nikamweleza. ‘Ah!’, akasema, ‘Sasa bwana, *logic* ya *modern society* sawa. Sasa sijui tutafanyaje na wale Wazanaki sijui nitafanya nao vipi? Kwa sababu *logic* yake naiona sasa’.

Sasa mambo mengine hakuyapitia na mimi nilikuwa na hakika baada ya pale alikwenda kutafuta. Ndio tabia yake. Lakini ku-*differ* hasa hapana, hatukuwahi ku-*differ*. Tulikuwa tunaweza ku-*differ* katika *analyses* za *issues*: yeye anafikiria tungekwenda hivi, sasa unaweza ku-*differ* nae lakini akitoa maelezo yeye mara nyingi unakubaliana nae kwa sababu mara nyingi *he was right* kwa sababu alikuwa na mtazamo mpana zaidi.

**IS**: Wakati huo unaweza kukumbuka *debates* zingine za kiitikadi, kwa mfano, kulikuwa na *debate* kuhusu *mass party* na *vanguard party*?

**KNM**: Aaa. Hiyo ilikuwa ngumu sana, kubwa. Kubwa sana. Sasa unajua, mambo mengine baadhi ya watu wetu huwa wanayapinga lakini hawayajui. Lakini vilevile wanaweza kukutuhumu wewe kwamba wewe ndio msimamo wako huo kumbe sio. Sasa tatizo moja hili la *vanguard party:* Kivukoni tulikuwa tunafundisha aina za vyama. Kwa hiyo tunaelezea *mass party*, mwanzo wake na ilivyofikia sasa; *vanguard party*, mwanzo wake, lakini muundo wake hasa na halafu tazama katika hali yetu tunaweza kuwa na *vanguard party* na ikawa *effective*. Sasa, lakini wanafunzi waliipenda sana dhana ya *vanguard party* kwa hiyo wanasemasema, ‘lazima chama chetu kiwe *vanguard* bwana, hatuwezi kuwa…’ Sasa katika vyama hamkosi kuwa na watu ambao hawaelewani ama wanapingana. Watu wengine wanapingana kwa sababu ya vyeo, ya matarajio yao, manake ninafikiria mimi cheo kile fulani anaweza kuninyang’anya kwa

hiyo mnaanza kupigana vita. Lakini wengine wanaweza kutofautiana kwa itikadi tu, jinsi mnavyoelewa mambo. Sasa hili suala la *vanguard party* ni moja ya mambo lilitaka kutumiwa dhidi yangu na baadhi ya watu katika Chama. Kwa hiyo nikashtakiwa kwenye Kamati Kuu…

**IS**: Ilikuwa lini?

**KNM**: *Effectively* ni '75 mwanzoni. Wakati huo niko Mkuu wa Chuo cha Kivukoni, kwa sababu mwanzo nilikuwa *lecturer* nikatoka nikaenda Algeria, [nilipotoka] Algeria nikaenda JKT, nikaenda Katibu Mkuu wa Vijana, nikawa Mkuu wa Mkoa, nikarudi tena Kivukoni sasa kuwa Mkuu wa Chuo. Sasa ikajengwa hoja kwamba mimi nimekibadilisha Chuo badala ya kuwa chuo cha Chama… kwa sababu sasa niliporudi Kivukoni mara ya pili mwaka '72 kuwa Mkuu wa Chuo ndipo sasa nikachukua hatua za kukifanya Chuo kiwe chuo cha Chama, pamoja na jina kabisa: Chuo cha Chama sio *Kivukoni College* basi, *no*, Chuo cha Chama cha Kivukoni; na *syllabus* na kila kitu na utaratibu ambao nilikuwa nimepigania huko nyuma kwa kuleta watu kwa mahitaji ya Chama.

Basi wakasema, 'Amekibadilisha Chuo kutoka kuwa Chuo cha TANU kimekuwa Chuo cha ki-*communist*, cha Ki-*marxist.* Na jambo moja la ushahidi ni kwamba wanasema wanafunzi wake, kwa mfano, kwamba, 'Chama lazima kiwe *vanguard*, kama hatuwezi kufanya TANU kuwa *vanguard* hatuwezi kujenga ujamaa'. Sasa wanakwenda huko wanatangaza. Kwa hiyo, *it was a serious charge.* Kwa hiyo nikaitwa kwenye Kamati Kuu, *charge* ikasomwa. Hee! Sasa nilipata *inkling* kama siku moja kabla. Kuna jamaa fulani waliniambia, wakasema, 'Wewe bwana wewe una habari kwamba wenzako wameshapanga Kamati Kuu ya kesho si unakwenda? Ukitoka hapo utakuwa sio mwanachama, utafukuzwa'. Tena watu wakubwa wale waliniambia, ah! Nikawaambia kuna nini? Wakaniambia, 'Wewe, wenzako wanasema tumeshampata, tunammaliza'. Basi, kulikuwa na *attempt* ya kutaka mimi, wakati wa kuzungumza suala hilo,

nisiwepo. Kwa hiyo, mjumbe mmoja, mzee mtu mzima, ndiye alipangwa aombe kwa Mwenyekiti kwamba sasa, 'Kwa utaratibu wetu, tunapomzungumza mtu, anakaa nje tunamzungumza halafu ndio tuweze kuzungumza kwa uhuru'.

**IS**: Wewe hukuwa member wa *Central Committee* wakati ule?

**KNM**: A-a. Nilikuwa nahudhuria kama Mkuu wa Chuo. Sasa, Mwalimu akakataa, akamwambia, 'Hapana. Haiwezekani. Mmeweka agenda kuzungumza hali ya Kivukoni, mtu tuliyemkabidhi Chuo cha Kivukoni ni Ngombale. Sasa mnasema atoke kusudi mzungumze kwa uhuru, atakayewajibu nani? Mwache akae hapahapa mseme, halafu mwisho ntamwita aeleze na ajibu kama yanayosemwa ni kweli, kama hayakueleweka basi atatupa maelezo. Kwa hiyo abaki, Ngombale baki hapo na sikiliza vizuri maneno ya wenzako'. Kwa hiyo ukaanza mjadala, mjadala mgumu! Wakasema, wakazungumza lakini kwa sababu nilikuwepo basi. Siku hiyo ilikuwa Jumamosi, tumekaa mpaka saa mbili usiku, wanazungumza hao hao tu *charges* zao. Baada ya pale Mwalimu akasema basi, 'Kesho saa tano, Ngombale jiandae uje kutueleza'. Kwa hiyo nikaja nikawajibu: pamoja na kuelezea juu ya Kivukoni, na yaliyosemwa kwamba mimi napaharibu na nini, nikajibu nikajaribu kuweka sawa. Sasa likaja hili suala *theoretical*, *ideological* la chama, nikawaeleza, kwanza, *vanguard party* ni nini na *mass party* ni nini.  Nikawaeleza kifupi, halafu nikawaeleza mimi ninavyoona katika hali ya Tanzania tunafanyaje. Na wakati huo nilikuwa nimetoa interview katika *Daily News*, a-a, ilikuwa bado *Tanganyika Standard*. Kulikuwa na yule mwandishi Philip Ochieng, alikuwa ameni-*interview* juu ya *vanguard party*, kwa hiyo nilikuwa nimefanya *analysis* yangu ya jumla na kwa *application* yake katika hali ya kwetu. Kwa hiyo nikawaambia, 'Kwanza kuna hiyo *interview*, kwa hiyo ni *documented*. Lakini niwaeleze tu kwamba mimi ninaamini kwamba *vanguard party* kama ilivyo, inavyotumika katika nchi za ma-*comrade* wa *socialist contries* haiwezi kutufaa sisi. Na ni jambo la kweli tu kwamba kwa kiwango chetu cha maendeleo na

hali ya wananchi wetu bado ni tofauti. Kwa hiyo aina ya chama tunachohitaji sisi ni hiki tulichonacho – *mass party* – chama ambacho ni *accessible*, ni rahisi kwa mtu kujiunga nacho. Hakina masharti magumu mradi tu muelewane juu ya mambo ya msingi ambayo mnakubaliana kwamba ndiyo imani za chama chenu.'

'Lakini', nikawaambia, 'mimi ninachoamini [ni] kwamba haitoshi tu kuwa na *mass party* kwa sababu wale *vanguard* wanachukua wale wao, chama chao, ni kiongozi wa nchi, wa *society*. Kila mwanachama wao wamemuandaa awe kiongozi katika nchi, akikaa mahala anaweza kuwasaidia watu na kuwapa watu miongozo. Wamemuandaa. Sasa, tatizo lake ni kwamba sisi hatuwezi kufanya kazi kama ile kwa sasa hivi tulivyo, lakini hatuwezi kuwa na chama ambapo mwanachama na kiongozi wote *level* yao ni ile ile. Haiwezekani. Hivi kama wewe Mwalimu ingekuwa kiwango chako ni sawa na sisi wote wengine tungefika tunakokwenda? Kwa hiyo, lazima tuwe na *mass party* lakini ambayo viongozi wake wameandaliwa vizuri, wana uadilifu ulio wazi, na wana uwezo wa kutenda ambao unaonekana, unajulikana ili waweze kuwaonyesha njia wanachama wenzao'.

'Sasa, maana yake hii ninayosema lazima kuunda *vanguard* ndani ya *mass party*. Kwa hiyo, mimi ninachoamini ni hicho – tusitosheke na *mass party*, a-a, lazima *mass party* ambayo ina uongozi wa kweli ulioandaliwa vizuri. Na ndiyo maana, *practically*, Mwalimu umekuwa ukijaribu hilo, ndio maana tuna Kivukoni; ndio maana kutokana na maamuzi yetu katika Chama kuna vyuo vya kanda ili watu watoe uongozi kweli, sio wababaishebabaishe watu wengine'.

Sasa nilipofika hapo, unajua tulianza saa tano?

**IS**: Mmm.

**KNM**: Tulimaliza saa mbili usiku!

**IS**: Ala!

**KNM**: Mimi nilizungumza *for two hours,* nilipomaliza, Mwalimu aka-*take up*. *In fact* nilivyofika hapo kwenye *vanguard*, nilipoeleza Mwalimu akanikatiza, akaniambia, 'Ngombale hebu kaa kwanza, pumzika'. Akawaambia wajumbe, 'Sikilizeni, sasa hapa hatumzungumzi Ngombale. Ingawaje najua baadhi yenu mlikuwa mnafikiri mmekuja hapa kuja kumzungumza Ngombale. Hapa tunazungumzia itikadi ya TANU. Eee? Mmemsikiliza vizuri Ngombale? Hapa ni itikadi ya TANU, na mimi nataka sasa tuzungumzie itikadi ya TANU', akanirudisha, 'endelea!' Nikafafanua pale juu ya Chama ninavyokiona, kiweje na nini, nilipomaliza akachukua yeye aka-*elaborate* zaidi.

Sasa wale waliokuwa wamepanga kuwa watamalizia kwa azimio la kunifukuza kwenye Chama wakawa wanaandikiana *note*, 'Ona, Mwalimu keshalivuruga hili suala.' Kwa hiyo tukaelewana, tukaelewana. *It was a difficult…* oh! Nalieleza hivi lakini lilikuwa gumu kweli kwa sababu *it was well organized.*

**IS**: Lakini ilikuwa idadi kubwa sana ya wajumbe wa Kamati Kuu?

**KNM**: Wajumbe sio wengi sana…

**IS**: Lakini wazito?

**KNM**: Ee, sasa Kamati Kuu ikiamua, kwa kawaida NEC itakubali tu. Sasa tukamaliza, tukatoka saa mbili. Siku ya pili, nikaletewa simu, 'Unaitwa Msasani!' Nikaenda kwa Mwalimu. Ah! Mwalimu akaniambia, 'Eh! Sikujua mimi!' Kwa sababu wale watu walioibuka pale kutaka kunikandamiza, wengine walikuwa rafiki zangu sana. Basi akasema, 'Ah! Fulani namwelewa, yule hawezi, hawezi kabisa. Yeye anafikiria wewe ni *competitor* wake sijui kwa sababu gani?' Mwalimu alikuwa anatujua kweli. 'Eeh', anasema, 'yule naelewa, lakini yule na yule na yule?' Kawataja mpaka… Nikamtajia wote sababu zao, nikamwambia, 'Sasa nisingekuelezeni pale sababu zake'. Tukazungumza vizuri sana, aka-*appreciate* sana akasema, 'Umefanya vizuri sana, na maelezo yako, safi kabisa!' Akanisifu sana, mambo yangu na nini,

akanambia ananisifu sana, lakini hii *off record*, akasema, 'Mimi sipendi kuwambia watu mambo yako lakini ngoja nikwambie ukweli mimi'. Basi nikaondoka.

Siku ya pili nikapigiwa simu tena toka Msasani, 'Eh?', nikamwambia anayenipigia simu, 'Mimi nilikuwa huko jana, wewe umekosea wewe'. Akasema, 'Hapana. Leo tena unatakiwa na Mzee'. Nikamwambia, 'Natakiwa namna gani? Nani? Mimi peke yangu?' Akaniambia, 'Hapana, kuna wenzako'. Basi nikasema, 'Kama kuna wengine na mie nakuja pengine kuna mambo mapya'. Nikaenda. Nikaingia. Kumbe Mwalimu ameita *personalities* kadhaa, tulivyofika wote pale, akatuambia, 'Sikilizeni. Nimewaiteni niko na jambo nataka kuwaambia. Jana nilikuwa na Ngombale hapa, nilizungumza nae sana. Sasa, kuna mambo niliyozungumza nae sitawaambieni. Lakini kuna jambo nataka kukuambieni.' Akasema, 'Ninyi wote ni rika moja, watu wa TANU, bado vijana, na Chama kimewaheshimu sana, kimewapa madaraka ninyi wote, madaraka makubwa. Tumekupeni madaraka kwa kuamini kwamba mtasukuma mbele maendeleo ya chama chetu na maendeleo ya nchi yetu. Lakini naona kuna ugonjwa hapa: badala ya kushirikiana na kusaidiana ili mambo ya Chama, mambo ya nchi yaende mbele, mara nyingi mnapoteza muda kwa kutafutana, kusengenyana, na wakati mwingine kufanyiana fitina. Sasa, nataka kuwaambieni: kama majukumu haya tuliyokupeni hamuwezi kuyatekeleza, mseme. Tena nakwambieni, msitafute urafiki, mimi sitaki muwe marafiki; la urafiki ni lenu wenyewe mtaamua huko. Rafiki ndiye unaenda nae kunywa bia, unakwenda nae kuvuta sigara, lakini muwe marafiki katika kufanya kazi za nchi. Ndivyo tulivyokuwa tunafanya wakati wa kupigania uhuru; wengine ninyi mmeshiriki moja kwa moja katika kupigania uhuru, sasa naona mmesahau.' Alitusema sana.

**IS**: Na hao walikuwa ni walewale wajumbe wa *Central Committee*?

**KNM**: Baadhi. Baadhi walikuwepo. Eh! Kwa mfano, aliwaambia kabisa, 'Asante sana. Ngombale hapa nimemchagua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani na katibu wa mkoa wa Chama. Baada ya miezi sita, Dar es Salaam imebadilika kabisa *politically*'. Akasema, 'Mimi, kwa sababu mimi ni kiongozi wa TANU, kiongozi wa Tanzania, sasa mtu anafanya kazi namna hiyo, sasa mimi si ninafurahi, ninapata nguvu kwamba kuna mwenzangu nae anatoa mchango wake? Lakini nyie *style* yenu, sasa inakuwa nongwa, ni maneno ya pembeni. Na nyinyi wengine katika sehemu zenu mmefanya kazi nzuri sana lakini wengine wamekuwa wakisema maneno hapa. Kwa hiyo, acheni mambo hayo, kazi yetu ni moja'. Kwa hiyo akaturudisha kwenye mstari, akatusema, tumeondoka pale kama wapumbavu wakubwa! [Kicheko]

**IS**: [Kicheko] Naona hutaki kutaja majina, walikuwa ni nani hao?

**KNM**: Sitaki kutaja.

**IS**: *Section* gani hiyo?

**KNM**: Eh! Hapana. Sitaki kutaja kwa sababu sio vizuri bwana, wengine wamekufa, wengine wapo.

**IS**: Lakini katika hali hiyo, kwa nini katika muda mfupi tu wakati ule, mimi nakumbuka, ulikuwa unabadilishwa sana vyeo?

**KNM**: Nayo hiyo, nilikuwa ni *problem* kwa watu wengine, ndiyo *subject* aliisema. Kwa sababu mmoja katika wale jamaa, niliwaambia kwenye Kamati Kuu kwamba, 'Huyu bwana ana *problem* zake, ni rafiki yangu lakini simuelewi. Kawaulizeni wale wafanyakazi wa feri ndio walioniambia, anakuja kwa wenzake pale akifika pale anakuwa huru tu anajisemea, 'Sasa huyu Mwalimu, kwa nini kila cheo Ngombale, kila cheo Ngombale, watu wengine hawapo?''.

Ah! Sasa wakati ule mimi sielewi lakini ilikuwa nadhani Mwalimu na Mzee Kawawa, unajua wakati ule kulikuwa na mambo yanabadilika yanakuja haraka sana, sasa walikuwa

wanaona tu kwamba hapa pana *problem* mpelekeni huyu bwana. Kwa mfano, kwenda Algeria kama katibu mkuu wa *Pan-African Youth Movement*…

**IS**: Ilikuwa baada ya Kivukoni?

**KNM**: Ee, *sixty-eight*. Kamati Kuu ya Chama ndiyo iliidhinisha. Kwa sababu ilionekana kweli *Youth League* wanadai kwamba hawana mtu mwingine. *Of course*, na *advantage* moja walifikiria, mimi najua Kifaransa. Lakini nilipokuwa kule, kukaja tatizo kubwa la JKT. JKT kukawa na matatizo ambayo Mwalimu mwenyewe alinieleza nilipoitwa kurudi, kwamba, 'Bwana kuna matatizo. Tunapeleka vijana waliosoma.' Ilikuwa ule utaratibu wa *compulsory, form six, university graduates*. Akasema, 'Sasa, wale vijana wanauliza wana masuali mengi, kwa sababu wakati wanakaa wana masuali juu ya serikali, mambo ya serikali, sera za serikali, wana masuali juu ya nchi yao. Wanahitaji majibu ya kuridhisha, kama hawayapati si vizuri. Sasa tumetazama nani anaweza kuja kutusaidia hapa, tukaona urudi wewe uende pale, uende uwe mkuu wa siasa katika JKT. Tunaamini unaweza kutusaidia kuwaridhisha wale wapiganaji, wale askari, kwa kuwaeleza mambo ya Chama, mambo ya serikali, mambo ya nchi, wakaridhika. Lakini vilevile hata makamanda wetu pale wanahitaji msaada vilevile wa kueleweshwa juu ya mambo, tunajua utaweza vilevile kuwasaidia. Ndio maana nimekwambia uje na nitataka unipe majina ya nani unafikiri unaweza kuwa nao wakusaidie katika kazi hiyo.' Ndio maana nikaenda.

**IS**: Ilikuwa lini hiyo?

**KNM**: Ilikuwa *sixty-nine*, early. *In fact*, waliamua *sixty-eight* ileile mwishoni.

**IS**: Kwa hiyo hukukaa sana huko?

**KNM**: Sikukaa sana. Ikabidi tukubaliane hapa na *Youth League*. Kwa sababu *members* kule ni *Youth League*, na *in fact* ni serikali, Rais aliniambia nikawe Katibu Mkuu. 'Nyinyi mjue namna gani ya kuwaeleza kule kwamba unahitajika hapa kwa kazi.' Kwa hiyo

ikabidi mimi niwe *withdrawn temporarily* kwa kazi maalum nyumbani. Kule nilikwenda na barua hiyo, tukakubaliana tumteue *Acting* Katibu Mkuu. Wakaniomba mimi katika wale ma-*deputy* wangu, manake nilikuwa na ma-*deputy* watano, ilikuwa kwa kanda, basi tukampata mmoja tukamfanya *acting*, ndio nikarudi.

Sasa, wakati nimerudi JKT nimeanza kazi, mambo yanakwenda vizuri, nikagundua kuna tatizo. Mimi ni *civilian* na ni kamisaa[10] wa jeshi, haifanani. Sijui mambo ya jeshi. Kwa hiyo nikaripoti kwa Mwalimu na Mzee Kawawa, nikawaambia, 'Jamani, kule kuna *contradiction*. Mimi *civilian*, wale wote maaskari wale.' Ah! Mwalimu akasema, 'Basi, unasemaje? Nenda kachukue *programme*, kwenye *programme* ya u-*recruits*. Lakini ukienda kwenye u-*recruit*, wakati wa vipindi vya *political education* lazima wewe mwenyewe uchukue *charge* kwa pale Ruvu.' Sawa, kwa hiyo ikabidi *1970 early* nikaenda, *three months*, *programme* ya u-*recruit*.

**IS**: Ulienda wapi, Monduli?

**KNM**: Hapana, JKT. Palepale kambini, mimi *Chief Political Education Officer* nimekuwa *recruit*. Lakini nimefanya miezi miwili, unajua vijana [*Youth League*] kulikuwa na matatizo, kukafanyika *reshuffle* halafu Katibu Mkuu mwenyewe akajiuzulu, Joseph, akaamua kurudi kijijini Butiama. Sasa, katika kutafuta nani awe Katibu Mkuu wa vijana katika hali hii, naona Msekwa – si alikuwa Katibu Mtendaji Mkuu – mara siku moja asubuhi, Msekwa akaja Ruvu JKT. Ah! Mara Msekwa akaingia. Na mimi ni *recruit*, mimi nilikuwa na marehemu Gama, ndiye alikuwa Mkuu wa Chuo, kamanda. Nilikuwa na *programme* – nilipendekeza pale na Gama alikubali, ya kufundisha wanavijiji, wananchi katika *radius* ya kilometa kumi kuzunguka Jeshi la Kujenga Taifa pale Ruvu – kuwafundisha elimu ya watu wazima pamoja na elimu ya siasa kila siku jioni. Sasa tulikuwa tuna-

---

[10] *Commissar*.

*finalise programme* pale, na Gama kama kamanda ameshakubali. Basi, [Msekwa] akaja akaniambia, 'Nina ujumbe wako'. 'Vipi?' Akasema, 'Mwalimu anasema saa kumi itatangazwa wewe ndiye katibu mkuu wa *TANU Youth League*.'

**IS**: Hukuwa *consulted*?

**KNM**: *No*! Alisema, 'Lakini, kwa kuwa uko hapa jeshini, kama mkuu wa kambi atakupa ruhusa, uende Msasani'. Nikamwambia, 'Haya bwana.' Kwa hiyo nikaruhusiwa pale siku ya tatu nikaenda Msasani, akani-*brief* pale akaniambia, 'Bwana, sikukuarifu kabla, nimeona lakini wewe utaelewa'. Kwa hiyo, mwanzoni alikuwa anataka nibaki JKT na *Youth League* lakini baadae akaona *contradiction* kubwa, sio vizuri, manake hiki ni Chama, JKT ni *state*, sasa inakuwaje? Basi tukaelewana pale lakini nilikuwa sijamaliza u-*recruit* wangu kwa hiyo nikarudi kwenye u-*recruit* wangu kwa ajili ya mwezi wa mwisho, mpaka kumaliza ndio nikaja *Youth League*.

Sasa, *Youth League* nako sikukaa sana kwa sababu mambo nayo yalikwenda haraka sana. Vurumai, mambo ya Uganda, Iddi Amin akamwangusha Obote akaanza *hostility* na nini, mpaka ile *February I think* kulikuwa na *clash* pale mpakani, akauwawa RPC wetu, Hans Poppe. Kwa hiyo ndiyo kukawa na suala la kuhusisha *NEC*. *NEC* ikapitisha Mwongozo wa 1971, ambao ndani yake kuna suala zima la ulinzi wa mgambo ambao mimi ndio niliu-*champion* katika *NEC* upitishwe. Kwa hiyo, ili kutekeleza hilo, Mwalimu akani-*appoint* kuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam ili niweze kuanzisha ulinzi wa mgambo.

**IS**: Hivi Mwongozo wa '71 ulikuwa *drafted* na nani?

**KNM**: Ulitolewa na Chama kwa sababu *NEC* iliunda *committee,* mwenyekiti Mzee Kawawa. Kamati ile wakaniomba mimi nifanye *drafting*. Kulingana na mchango wangu katika *NEC* nilipoanzisha mjadala ule wa *NEC* kwa hiyo wakaniomba mimi nikafanye *drafting*. Na mimi nikawaomba, 'Mimi peke yangu

hapana’. Nikapendekeza niwe na Hashim Mbita, wakati ule akiwa Katibu Mtendaji Mkuu wa Chama. Kwa hiyo, *drafting* tumeifanya mimi na Hashim Mbita. *Of course*, draft inakuja kwenye Kamati, inatazamwa, mnakubaliana. Mkishakubaliana na Kamati, ile *final version* tunampelekea Mwenyekiti. Mwenyekiti anaitazama, yeye ana fursa na madaraka ya kufanya marekebisho kabla ya kufikisha kwenye *NEC* yenyewe. Kwa hiyo, ndivyo tulivyofanya.

**IS**: Sasa, wengine katika Chama, ambao hawakuwa wajumbe wa Kamati, walihusika au walikuwa wanawa-*consult*?

**KNM**: A-a. Ni *NEC* imezungumza, kwa kweli tunatakiwa tuendeleze yale ya *NEC* ili kupata hiyo version. Kwa hiyo kuna Kamati, baadhi ya wajumbe wa Kamati wenye *interest* maalum wanaweza kuja kwa watu wanao-*draft*.

**IS**: Lakini mimi nafikiria wale ambao walikuwa wanajulikana kama ni *left*, hasa *Marxist left*, kwa mfano akina Babu na nini, hao walihusika?

**KNM**: Babu alikuwa mjumbe katika Kamati.

**IS**: Babu alikuwa mjumbe wa kamati hiyo ya ku-*draft* Mwongozo?

**KNM**: Ndio. Na, mimi wakati nafanya *drafting*, yeye Babu kwa sababu alikuwa rafiki yangu, alipita wakati fulani tukazungumzazungumza akaondoka. Babu alikuwa *integrated* kwa sababu kikao kile cha NEC kilikuwa kikubwa, kinazungumzia usalama wa nchi, mawaziri wote na manaibu wao walialikwa.

**IS**: Sasa ilikuwa ni *logic* gani yenu katika ku-*include* ile ibara ya 15?

**KNM**: Ibara ya 15 ilikuwa inajibu madai ya *situation* ya wakati ule. Kwa sababu wakati wa ukoloni, uendeshaji wa shughuli (*management*) kwa ujumla ilikuwa ya mkubwa na mdogo. Kwa hiyo wafanyakazi walikuwa ni watu wa kupewa maagizo na amri.

Sasa, hali hiyo iliendelezwa. Na wakati ule, tangu wakati wa ukoloni, watu wanaotumiwa na *administration* kusimamia mambo walikuwa wanaitwa wanyapara. Kwa hiyo neno mnyapara ilikuwa ni kama ndiyo alama ya utawala wa mkubwa na mdogo, manake nyinyi wadogo hamna sauti, mnyapara ndiye mwenye sauti.

Lakini baada ya uhuru, na mara baada ya Azimio la Arusha hasa, manake Waingereza hawakuacha viwanda hasa lakini kutokana na Azimio la Arusha [na] utekelezaji wake, utakumbuka, sekta ya umma ikaanza kujitokeza kwa nguvu kubwa. Kwa hiyo, wafanyakazi wakaanza kuongezeka kwa sababu viwanda vinaanzishwa, na kadhalika. Lakini mtazamo wa wale mameneja na waendeshaji wengine ulionekana kwamba ni uleule tu wa mkubwa na mdogo. Kwa hiyo, suala lile la ibara ya 15 tuliliona ni muhimu katika kuleta mawazo mapya juu ya uendeshaji wa shughuli katika nchi yetu. Na hasa wakati ule, rais Nyerere alikuwa ametoa ile *circular* yake ya ushirikishwaji wa wafanyakazi.

**IS**: *Workers' Councils*?

**KNM**: *Yeah*. Kwa hiyo suala lile lilikuwa linazungumzika lakini wakubwa walikuwa na kigugumizi. Kwa hiyo tuliona kwamba Chama kitoe msukumo kwa kuweka ile ibara ambayo ililalamikiwa sana na hao wakubwa kwa sababu waliona tunavuruga nidhamu. Na utakumbuka, Mwongozo ule ulijadiliwa kwenye matawi yetu katika sehemu za kazi na nini na uliunda mwamko mpya wa wafanyakazi. Na kwa kweli walianza kuhoji aina fulani fulani za uendeshaji wa shughuli na kukawa na wimbi la migomo na kuwafungia wakubwa. Na mimi kwa wakati ule sasa nilikuwa mkuu wa mkoa kwa muda, ilinipa kazi kubwa sana. Manake migomo ile ikitokea na mimi lazima niende, sasa nikienda, mara nyingi nikizungumza nao wafanyakazi walikuwa wananikubalia ninachowashauri. Kwa hiyo ikaanza kutafsiriwa na baadhi ya viongozi wenzangu kwamba 'Yeye huyu ndie anachochea mambo yake ya Mwongozo.' Kwa hiyo ilikuwa

ngumu sana; wakubwa walifanya jitihada sana ya kutafuta njia ya kuzima kabisa ule mwamko wa wafanyakazi. Na nadhani baadae kidogo walifanikiwa.

**IS**: Walifanikiwa?

**KNM**: Ndio.

**IS**: Kwa sababu Mwalimu si alikuja kutoa ile *speech* yake ya Mei mosi, ya ’74 nafikiri. Katika hili sasa hamkujadili kabisa na Mwalimu? Yeye alionaje vuguvugu hili?

**KNM**: Hapana. Mimi sikujadiliana nae tena, wakati huo sasa mimi niko Tanga – *RC* Tanga, ’74, na miaka 20 ya TANU. No, tulikuwa tukipata nafasi tukikutana tunajadili mambo lakini sikuwahi kuzungumza nae juu ya [Mwongozo].

**IS**: Labda kabla hatujamaliza session hii, wakati huo pia kulikuwa na lile vuguvugu la mijadala pale Chuo Kikuu. Sijui kwa kiasi gani wewe na kwa kiasi gani Mwalimu mwenyewe alivyokuwa anaona yanayotokea hapo?

**KNM**: Kwanza, jambo moja kubwa ni kwamba, hasa baada ya Azimio la Arusha, ule mwamko wa kisiasa uliojitokeza katika nchi, kitovu kimoja cha mwamko ule ilikuwa ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Na kwa sababu pale palikuwa na bahati yake moja nzuri – sijui, wewe unajua zaidi kwa sababu wewe ulikuwa palepale, mwanafunzi. Kwa upande mmoja kulikuwa na baadhi ya wahadhiri waliokuwa na mtazamo wa kushoto; watu wenye fikra za kijamaa na za kupinga ubeberu duniani. Lakini vilevile bahati nzuri kukawa na kundi la wanafunzi ambao nao walikuwa na mtazamo wa kimaendeleo, wa kijamaa, wa kupinga ubeberu. Kwa hiyo, ule mchanganyiko wake ulileta vuguvugu ya aina ya kipekee.

Hata mimi nikiwa Kivukoni bado *as a lecturer*, kama mwalimu, niliwahi kuwa na mpango mmoja wa kutoka na baadhi ya wanafunzi kwenda kuungana na watu vijijini, wananchi vijijini. Sasa *this time* tulikuwa na *problem* Bagamoyo. Vijana wa

Bagamoyo walikuwa wamepanda mpunga, wakafanikiwa sana, shamba lao la pamoja, barabara ile inatokezea Msata pale kwenye bonde lile la mto Ruvu. Mpunga wao mwingi, wakawa wanapata taabu ya kuuvuna. Kwa hiyo tukaamua twende tukaungane nao, lakini tukafanya mawasiliano na *TANU Youth League* ya Chuo Kikuu. Kwa hiyo baadhi ya vijana wa Chuo Kikuu na wale wanafunzi wa Kivukoni tukaungana tukaenda Bagamoyo kwenda kuungana na vijana wa Bagamoyo kwenda kushughulikia ule mpunga. Tukashinda pale siku nzima, jioni tukaenda kuzungumza na *DC*, ambae alikuwa katika wale *veterans* wetu wa uhuru, mzee Saadan Kandoro. Unamkumbuka?

**IS**: Ndiyo.

**KNM**: Ee, ndiye alikuwa *DC* pale. Tukaenda pale, tulifanya maandamano mjini Bagamoyo makusudi kuwasisimua wananchi kidogo, tukamalizia pale. Mzee Kandoro akafurahi sana, akatoa hotuba nzuri sana ya kutukumbusha mambo ya kupigania uhuru na namna ya kuungana na wakulima na wafanyakazi, alitoa hotuba nzuri sana. Kwa hiyo hilo moja, lakini la pili, Mwalimu mwenyewe alikuwa na tabia ya kuwa tayari wakati wowote akikaribishwa kwenda kuzungumza na jumuiya ya Chuo Kikuu. Na wakati mwingine anataka yeye mwenyewe, anaomba anakwambieni, ‘Nitengenezeeni, nataka kukutana nao’. Na mimi nilikuwa mmoja wa wale ambao tulikuwa tunatoka Kivukoni tunafuatana na Mwalimu kwenda pale Chuo Kikuu. Unakumbuka pale palikuwa na joto kubwa pale?

**IS**: Ndiyo.

**KNM**: Kulikuwa na wakati mwingine mnaandaa semina za *teaching*, na Mwalimu anakuja kufungua pale kwa jumla, *community* nzima, halafu sisi wengine tunakuja kutoa mazungumzo, na kadhalika. Kwa hiyo, wakati ule Chuo Kikuu pale kilikuwa ni kituo chetu kikubwa sana cha vuguvugu la kimapinduzi.

**IS**: Uliwahi kumsikia Mwalimu akizungumzia hilo *at any time*?

**KNM**: Oh! Sana. Tena alikuwa ana mawasiliano ya moja kwa moja na baadhi ya viongozi wa vijana wa pale Chuo Kikuu. Wakati mwingine mimi nilikuwa natafutwa, napigiwa simu, 'Njoo Msasani, unaitwa!' Nikienda kule namkuta Mwalimu kazungukwa na timu ya vijana wa kutoka Mlimani. Kabisa, yeye alikuwa ana matumaini makubwa sana na uongozi wa vijana wakati ule. *Of course*, kulikuwa na nyakati tulikuwa na matatizo kidogo. Kwa mfano, baada ya kuuawa Dr. Mondlane, FRELIMO walikuwa na msukosuko mkubwa sana kabla hawajapata uongozi mpya. Sasa, kulikuwa na baadhi yetu viongozi wa Tanzania – katika kuwa karibu na wenzetu wa FRELIMO – nadhani tulikuwa tunaingia mno na kujifanya ni sehemu ya makundi yao. Kwa hiyo kulikuwa na Simango, manake kulikuwa na makamu wawili – Marcelino dos Santos na Rev. Simango. Simango alikuwa na msimamo wake tofauti, Marcelino msimamo wake tofauti. Mimi nilikuwa nimezungumza nao wote wawili baada ya kuuawa Dr. Mondlane. Maelezo ya Simango juu ya yalivyotokea mambo mpaka kuuawa kwa Dr. Mondlane, maelezo yake sikuyaelewa. Na yeye ndiye alikuwa wa kwanza niliyemkuta pale mpaka nilipoonana na Marcelino ndiyo akanieleza na nikamuuliza, 'Mbona huyu bwana kanieleza hivi na hivi?' Akanieleza na yeye kwa nini yule bwana ameeleza hivyo. Sasa, pale Mlimani, baadhi ya ma-*comrade* walikuwa wamechukua upande, walikuwa upande wa Simango. Walituma wenzao kuja kuniona, wakati niko JKT pale. Wakaja kuniona, wakajieleza, mie nikawaeleza. Niliwaeleza tu, 'Sasa, mi nasemaje, nyinyi hili suala la FRELIMO na uongozi wao, kwa sababu ni tata, tumwachie Mwalimu. Yeye analijua vizuri sana na liko mikononi mwake. Tusijiingize na kuchukua *positions*, tutapata matatizo.'

**IS**: Hao waliokuja walikuwa vijana wa *TANU Youth League* au wa *USARF*?

**KNM**: Wa *TANU Youth League*. Lakini na wao si walikuwa *USARF*?

**IS**: Ndio.

**KNM**: Ndio wale *progressive*?

**IS**: Ndio, akina marehemu Moronda, Shija…

**KNM**: Na hata hawa akina Kamala walikuja baadae. *In fact*, aliyekuja ni Kamala halafu akarudi. Kwa hiyo, mimi nikasafiri, nilikuwa na *programme* Same. Niko Same napigiwa simu na Butiku. A-a, nilizungumza nae tuko hapahapa. Alinipigia akaniambia, 'Bwana, tunasikia huko Mlimani vijana wanayumba, vipi wewe unazo habari?' Nikamwambia, 'Hapana. Ninazo habari lakini amekuja mwenzao mmoja ambae ni kiongozi, nimemweleza hivi hivi hivi. Waache hili jambo, *leadership* ya nchi inalishughulikia. Kwa hiyo usiwe na wasiwasi.' Kwa hiyo, niko Same ananipigia tena simu ananiambia, 'Mi nilimwambia Mwalimu kwamba umeshazungumza nao lakini mbona wametoa *statement* wanamuunga mkono Simango?' 'Ah!' nikasema, 'Oh! Sa la la!' Sasa mie niko Same pale, tena usiku saa hizo, nikasema 'Bwana, wamefanya maamuzi yao wenyewe sasa. Tuwaache, wamefanya wenyewe maamuzi'.


Kwa hiyo nasema wakati mwingine tulikuwa na *problem* lakini hilo tatizo alilimaliza Mwalimu baadae. Kwa sababu ilibidi Mwalimu awaite wote, Samora, Marcelino, Rev. Simango, akina Chissano, wote lakini akawaita na viongozi wa kwetu wote, *ministers*, *commanders* wa majeshi, wote, akawapa msimamo. Akawaambia, 'Sikilizeni. Mimi Mondlane aliniambia mambo mawili. Kwanza, FRELIMO imedhamiria kuikomboa Msumbiji, kwa hiyo, vita. La pili, akasema ana kamanda wake wa vita, ndiye anaongoza vita, Samora Machel. Aliongea hayo mawili. Kwa hiyo, mimi nasema namtambua Samora ndiye kiongozi wenu. Sasa nyinyi, Marcelino dos Santos, Rev. Simango, mkitaka kufanya *politics* zenu, nani mkubwa nani nini, nyie endeleeni. Lakini Tanzania inataka kama alivyosema Mondlane, kuikomboa Msumbiji na tuna kamanda wa kuikomboa, kwa hiyo ndiye ataongoza. Atawaongoza. Mkishashika nchi yenu, hiyo tena mtaendelea na democratic *process* na nini.'.

Ndio yakamalizika. Na ilikuwa nzuri kwa sababu zote mbili: kuwaambia akina Simango, lakini vilevile kuwaambia timu yetu ya Tanzania, 'Wale wanaotaka kuingiaingia waache'. Na *from there …* manake Samora na dos Santos, baada ya mkutano huo walinitafuta wakaja kuni-*brief*, mi sikuwepo. Wakanambia, 'Bwana, mambo yamekwisha. Sasa jambo moja tu – vita! Basi. Mwalimu ametumalizia *problem* yetu'.

**IS**: Sasa Simango haikuchukua muda. akaja kuonyesha ukweli wake.

**KNM**: Naam. Mimi alinipa hadithi ya ajabu, juu ya kifo cha nani…[Mondlane]. Sasa nimesahau kidogo lakini alinipa *story* ambayo hata nini… *In fact*, wakati ule, nimerudi kutoka Algeria kama juzi yake, na kule Waalgeria walikuwa wamenipa barua yake Dr. Mondlane. FRELIMO walikuwa wameomba mambo fulani fulani ya msaada manake *Algerians* walikuwa wanatusaidia. *Liberation struggles*? *Oh! They were first ones*! Kwa hiyo ndio nikawa hapa, siku ya pili ndio ameuawa. Kwa hiyo siku ya tatu nikaenda, ndio akanipigia *story*. Kumbe alikuwa *part of the plot*!

**IS**: Sawa, mie naona tumalizie hapa.



## 16 Agosti 2012

**IS**: Sasa leo Mzee kidogo tutabadilisha utaratibu wetu. Badala ya kwenda *chronologically*, nina masuali juu ya mambo mbali mbali. Tunaweza tukawa na mazungumzo tu kuhusu masuali haya. Ni *kind of cluster of questions* na hasa *emphasis* yetu ni kuangalia *attitudes, opinions*, uhusiano wa Mwalimu na viongozi wenzake na mambo mbali mbali yaliyotokea nchini.

Labda tuanze na uhusiano wake na viongozi wenzake, labda tuanze na Mzee Kawawa. Wakati unawafahamu wewe na umeshuhudia wakiwa pamoja. Uhusiano wake na Mzee Kawawa ulikuwaje?

**KNM**: Mimi nnavyojua Mwalimu alikuja kumtambua Mzee Kawawa mapema kidogo katika historia. Kwa sababu sina hakika kama Mzee Kawawa alimjua Mwalimu kabla ya Mwalimu kuanzisha TANU. Lakini najua kwamba mwaka ule wa hamsini na nne wakati pirika pirika za kuanzisha, mpaka TANU inaanzishwa, Mzee Kawawa alikuwa ndiye kiongozi wa chama cha wafanyakazi Waafrika serikalini. Chama hichi kilikuwa kinaitwa kwa kifupi TAGSA: *Tanganyika Government Servants Association* na yeye ndiye alikuwa *President*. Na mimi kwa bahati nzuri mara tu baada ya kumaliza shule mwisho mwa mwaka '93.

**IS**: '53.

**KNM**: '53. Sasa kwa sababu mimi sikuandikishwa kwenda Makerere, mimi nilikuwa na nia ya kwenda India. Nilikuwa nataka kusomea sheria *in fact*. Tungekuwa wanasheria wote. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo nilipomaliza shule tu nikapewa *direct employment* kama karani. Kwa hiyo mwezi *January* '54 nikaajiriwa na serikali PWD: *Public Works Department*, karani. Na bahati nzuri katibu wa TAGSA, katibu mkuu alikuwa mzee Ally Sykes sasa. Yeye ndiye akaniita akasema 'Bwana wewe sasa umemaliza shule umeanza kazi. Uko wapi?' nikamwambia niko

PWD kwa sababu tunafahamiana. Tulikuwa tunafahamiana sisi wadogo yule kaka yetu mkubwa. Akaniambia ‘Bwana wewe mimi nakutaka uje, tukutane Arnatouglo.’ Akanipa tarehe, ‘Tuna mkutano.’

Nikaenda, ndio kwenda akaniambia ‘Bwana nimekuita makusudi, tuna chama hapa cha wafanyakazi wa serikali, na nimezungumza na wenzangu kwenye kamati, nimependekeza wewe uingie katika kamati, *national committee* ya TAGSA.’ Kwa hiyo mimi nilikuwa nje, nikaambiwa basi nimsubiri kidogo, ‘Tumalize mazungumzo.’ Walipozungumza wakakubaliana, wakanialika. Kwa hiyo tangu pale nikawa mwanachama ndani ya kamati. Lakini wakati huo Mzee Kawawa hakuwa Dar es Salaam, alipata *transfer* ya kikazi.

Lakini TAGSA pamoja na kwamba ilikuwa chama cha wafanyakazi tu lakini tulikuwa tunazungumzia mambo ya siasa sana. Kwa hiyo ilipoundwa TANU, tulipopata taarifa ilitoka kwenye magazeti. Kwa hiyo tukamtafuta Mzee Ally Sykes. Nikamwambia bwana itisha kikao cha TAGSA ili utueleze, maana yake yeye ni mmoja wa waanzilishi wa TANU. Basi na bahati nzuri yeye ndiye aliyekuwa ameandaa hata kadi za chama cha TANU kwa niaba ya chama chenyewe. Wakati ule kulikuwa hakuna *Secretary General* wala nani. Yeye ndiye alikuwa anafanya mambo practical. Maana yake alikua yeye *labour officer* hapa hapa Dar es Salaam.

Kwa hiyo akaitisha kikao, bahati nzuri akaja na kadi za TANU. Baada ya kutueleza kilichofanyika na madhumuni ya chama kwa hiyo tulio wengi pale, karibu wote pale tukadai tuingie katika TANU.

**IS**: Na unakumbuka kama Mzee Kawawa alikuwepo? Alichukua kadi yake?

**KNM**: Hakuwepo. Yeye alikuwa *transferred* wakati sisi tunajiunga. Mimi nimejiunga kama wiki moja baada ya TANU kuanzishwa. Kwa hiyo TAGSA ilikuwa *very*… ilikuwa *active* sana na baada ya pale Mzee Kawawa naye akarudi kama

president. Harakati zikawa… za TAGSA ilikuwa kubadilisha, sio kubadilisha… Kuanzisha mchakato wa kuanzisha *central organization* ya *trade unions* ili vyama vya wafanyakazi viunganishwe na chombo kimoja. Mzee Kawawa alivyorudi akajiunga moja kwa moja na TANU, sikumbuki tarehe yake. Na najua baada ya hapo akafahamiana, akajiunga na kuwa karibu zaidi na Mwalimu.

**IS**: Lakini wewe kwa upande wako mara ya kwanza ilikuwa lini wakati ulipowaona wakiwa pamoja kwenye kikao au kwenye mazungumzo? Unakumbuka?

**KNM**: Sasa hivi siwezi kukumbuka. Sasa nnachojua ni kwamba hasa baada ya kuundwa kwa *Tanganyika Federation of Labour* Mwalimu alikuwa karibu sana na Mzee Kawawa kama kiongozi wa *Tanganyika Federation of Labour*. Baada ya kuchaguliwa kwenye *Tanganyika Federation of Labour* sasa akaacha uongozi wa TAGSA. Na imekuwa hivyo na ndio maana mpaka tulipofika mwaka '58 kwenye Mkutano Mkuu wa Tabora watu wawili muhimu sana hawakuwepo kwenye mkutano ule kwa maelezo ya Mwalimu wakati ule kwa sababu mimi nilikuwa mjumbe. Mmoja ambaye hakuwepo alikuwa Rashidi Mfaume Kawawa. Na yeye mwenyewe Mwalimu akawaeleza watu na akaeleza kwa nini hakuwepo. Wakati ule chama cha wafanyakazi kilikuwa na mapambano na waajiri.

Na kwa mfano, moja ya matatizo yaliyotokea wakati ule ni kiwanda cha bia, *Breweries* wafanyakzi ilibidi wagome. Sasa walipogoma waajiri wakaamua kukaribisha watu ambao sio Waafrika kuja kujaza nafasi za wale Waafrika waliokuwa wanafanya kazi pale. Kwa hiyo wakawakaribisha Waasia. Kwa hiyo Wahindi na Waarabu. Sasa kitendo kile kiliwakera sana viongozi na wanachama wa TANU. Kwamba sasa suala la kawaida la wafanyakazi, linanza kupewa sura ya rangi na kwa hiyo ubaguzi.

Kwa hiyo kwa sababu hiyo, rais wa TANU, Mwalimu, akazungumza na kusema tuwaunge mkono wafanyakazi wa

*Breweries* na TFL kwa ujumla, yaani TANU iwaunge mkono. Na wakati ule kwa sababu lilitokea lile la mgomo ule kuvunjwa kwa namna ambayo haikupendeza, ulitangazwa mgomo wa bia. Kwamba Waafrika sasa waache bia, wasinywe.

**IS**: Na hii ilikuwa ni uamuzi wa TANU?

**KNM**: Ulikuwa uamuzi wa TANU katika kuunga mkono…

**IS**: Na ulizungumzia mkutano wa '58.

**KNM**: '58 Mwalimu aliuzungumzia, na kuwataka viongozi wa TANU tukimaliza mkutano pale lazima kupeleka ujumbe kwamba lazima tuwaunge mkono mpaka washinde. Sasa kwa hiyo kutokana na tukio lile la mgomo ule ndio maana mzee Kawawa hakuwepo kwenye mkutano mkuu wa Tabora. Na mwingine ambaye hakuwepo alikuwa ni Paul Bomani. Ambaye alikuwa ndiye kiongozi wa vyama vya ushirika vya Nyanza, Ziwa. Na chama chetu kule ukanda wa Ziwa kilikuwa na msisimko mkubwa sana, msisimko mkubwa. Na nguvu kubwa kwa sababu vile vyama vya ushirika vilisaidia kuinua mwamko wa watu TANU ilipoundwa.

Kwa hiyo Mwalimu aliwazungumzia sana, akawasifu sana wote wawili. Akasema vijana wazuri, safi kabisa, wazalendo wanatufanyia kazi nzuri sana. Na ndio maana mzee Kawawa alichaguliwa kuwa mjumbe wa NEC pamoja na kuwa yeye mwenyewe alikuwa hayupo.

Na wakati wote walikuwa pamoja katika siku zile za mapambano. Hata sisi katika kwenda kwetu nje, tumepelekwa na TANU. Na uamuzi ulifanywa Mzee Kawawa alikuwa si mjumbe wa Kamati Kuu, wala hakuwepo. Lakini ilipokuja kwenye safari yetu sasa, ile kuondoka, tulikuwa watatu. Ile kuondoka si lazima tupate *passports* na nini? Na passports zinataka wadhamini. Sasa sote watatu kutokana na familia zetu. Mimi baba angu asingeweza kuchukua dhamana ya shilingi elfu tatu, siku zile zilikuwa shilingi elfu tatu, elfu tatu zilikuwa nyingi sana.

Lakini siku moja Mwalimu akatuambia 'Nyinyi mshapata *passport*?' Anatuuliza, tukamwambia bado tunatafuta wadhamini sasa. 'Mmeshapata?' tukamwambia bado, 'Kwa nini? Wewe Ngombale wewe humjui Kawawa? Nenda, nendeni kwa Kawawa.'

Kwa hiyo tukaenda wote watatu. Yeye Mzee Kawawa tulikuwa tunafahamiana tangu shule. Akasema 'Vipi?' Tukasema sisi safari yetu imefika lakini hatuna wadhamini wa *passport*. Akasema 'Ah! Basi, mimi nita… mwingine nani?' Tulikuwa tumeshamzungumza Mzee John Rupia. Akasema 'Basi akishaandika Mzee John Rupia nileteeni na mimi ntaandika.' Basi.

**IS**: Uhusiano huu wa karibu uliendelea katika muda huu wote walipokuwa pamoja katika uongozi?

**KNM**: Nnavyojua mimi ingawa mimi baadae nilikwenda nje lakini sikusikia tofauti yoyote kati ya Mwalimu na Mzee Kawawa. Na kwa kweli mambo yote yalionesha kwamba waliendelea kuwa karibu zaidi.

**IS**: Katika vikao vya chama kwa mfano, na wewe bila shaka ulihudhuria vingi tu, ulionaje uhusiano wao? Anapozungumza, anapounga mkono, anapotoa hoja?

**KNM**: Katika vikao Mwalimu sasa alikuwa ndio mwenyekiti. Na Mzee Kawawa kwa muda mrefu alikuwa makamu, baada ya Mzee John Rupia kustaafu. Na baadae akaendelea kama mjumbe wa Kamati Kuu na Halmashauri Kuu. Sikumbuki kuona kwamba walikuwa wanahitilafiana, kimsingi, kwa sababu pengine … sababu moja *style* ya Mwalimu ya kuendesha mkutano. Alikuwa anatoa nafasi kwa wajumbe wazungumze. Na kwa kawaida alikuwa haingilii kati mtu.

**IS**: Mpaka anamaliza?

**KNM**: Eeh, anamuachia mtu ajenge hoja yake mpaka alipomaliza.

**IS**: Lakini alikuwa anaweka *time* au bila kikomo?

**KNM**: Hapana, yeye anatoa tahadhari tu, mtu asichukue muda mwingi mno na kuwafanya wengine wakose nafasi ya kushiriki. Lakini alikuwa siyo *mechanical*, haendeshi mikutano kama mashine. Alikuwa anataka … mtu yule alikuwa anataka kutoa mchango gani. Kwa hiyo anatoa nafasi hata pale ambapo hakubaliani. Kwa kawaida atakuja kuzungumza mwisho atapofanya majumuisho, *summing up* yake.

Kama unazungumzia jambo kubwa, watu watatoa maoni watazungumza, watazungumza, watazungumza … Sasa mwisho ndio nafasi yake kama mwenyekiti kufanya majumuisho. Na pale ndipo anaweza kusema ‘Lakini kuna wajumbe wamesema hivi, ama fulani alisema hivi lakini hii sio sahihi. Maana yake ingekuwa hivyo, mbona kuna hivi na hivi na hivi.’

Kwa hiyo, kwa utaratibu wake ule, ilikuwa si rahisi sana kumuona anatofautiana na mtu. Isipokuwa kama jambo mtu anasema la uongo, yeye atalirekebisha.

**IS**: Palepale?

**KNM**: Enh, tena anaweza kukuingilia katikati. Kukukatiza na kukusema kwamba bwana, hilo unalolisema sio sahihi. Mbona ukweli ni huu na huu na huu. Lakini vinginevyo watasema, watu watazungumza, mwisho yeye atafanya *summing up*. Atafanya majumuisho, kwa lengo la kufikia maamuzi kwa utekelezaji.

**IS**: Sasa katika mazungumzo, yeye kama mwenyekiti bila shaka alikuwa anawachagua watu wa kuzungumza. Sasa wewe mwenyewe… kwa sababu hivi tuna*record* ya historia, ulipata *impression* kwamba alikuwa anawachagua wale ambao alifikiri kwamba wanatoa mawazo ambayo yeye anakubaliana nayo? Au hakuwa *selective* katika hilo?

**KNM**: Hapana, kwa kawaida Mwalimu nilivyomuona mimi kwanza alikuwa anatoa nafasi kwa wote bila kubagua. Hata akijua huyu mjumbe fulani hana mchango hasa. Akiinuka ni anastawisha

baraza tu, atampa nafasi. Akijua kama hakubaliani ndio atapenda azungumze. Atapenda mawazo yake yaje uwanjani, hilo la kwanza. Kwa hiyo alikuwa habagui, la kwanza.

Lakini la pili alikuwa hodari katika maana kwamba alikuwa anajua yeye ni kiongozi wa chama; na chama kina sera zake, kina fikra zake na kina muelekeo wake. Sasa kwa kuwa alikuwa anawajua wajumbe wake, kwa hiyo alikuwa anawajua watu wanaoweza kumsaidia katika kutoa mchango wa kuimarisha msimamo wa chama. Watu ambao wanaweza, wakifafanua mambo wanawasaidia wajumbe wengine kuelewa jambo. Kwa sababu wajumbe wengine hawasaidii mkutano kwenda mnakotaka kuelekea. Wanazungumza kwa ajili ya kuzungumza tu. Kwa hiyo mara nyingine mnaweza mkikaa mnaweza kufanya vikao havina matokeo. Kwa hiyo Mwalimu kwa hilo alikuwa hodari.

Anajua nani aanze, anafikiri msemaji huyu akianza ataanza vizuri na wengine watapata mwanga wa tunachotaka kuzungumza ni kipi. Kwa hiyo muelekeo wa mazungumzo utakuwa mzuri. Na anaweza vile vile mwingine akamuweka akiba kusudi kama mjadala unaanza kuyumba anajua nani wa kumtafuta. Akimpa nafasi anaweza kusaidia mkutano usiyumbe, urudi kwenye mstari. Kwa hilo alikuwa fundi. Kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa anajua kule ambako angependa mkutano uende. Kwa hiyo alikuwa anaweza kuongoza vizuri.

**IS**: Na katika hili kutokana na uzoefu wao wa muda mrefu tu, unaweza ukatutajia majina ya wale ambao aliwaona… aliwatumia kwa ajili ya kuanza mjadala, au kuelekeza mjadala? Au wale ambao alikuwa anaweka akiba?

**KNM**: Hapana, ni vigumu kidogo, ni vigumu.

**IS**: Lakini wachache bila shaka una…

**KNM**: Ni vigumu lakini sasa unajua …

**IS**: Tuseme kwa mfano katika mkutano wa NEC…

**KNM**: Eeh, ndio. Unajua Profesa hili vizuri nadhani hivyo nilivyolieleza linatosha kwa sababu ukianza kutaja watu kwa majina ni tatizo. Kwa sababu muda mrefu umepita, watu wengine hawapo wameshatoka duniani, wengine wachache wapo. Lakini wale ambao hawapo unaweza kuwa huwatendei haki maana yake…

**IS**: *Okay*, basi sawa tuache hiyo. Sasa, ningependa kuuliza suali, je uhusiano kati ya Mzee Kawawa na Mwalimu, zaidi ilikuwa kwa upande mmoja loyalty ya Mzee Kawawa kwa Mwalimu, na kwa upande mwingine ile *trust* ya Mwalimu kwa Mzee Kawawa, zaidi kuliko *identity* yao ya mawazo yao kuhusu itikadi. Nikisema hivyo unafikiri nimekosea?

**KNM**: Ndio na hapana, katika maana kwamba watu wawili wale walikuwa wanaaminiana sana, sana. Lakini kwa sababu, kila mmoja naamini mimi alikuwa na sababu zake. Mzee Kawawa alikuwa anamuamini na kumheshimu Mwalimu Nyerere, kama ambavyo wakati ule vijana wengine waliokuwa wakweli na wazalendo wa nafsi walivyomuamini na kumheshimu Mwalimu. Kwa sababu sote tuliokuja kumjua Mwalimu tulimheshimu kwa sababu nyingi tu. Moja ni uwezo wake wa mawazo, alikuwa na kipaji kikubwa cha kuchambua mambo na kuyafafanua na kuyaeleza. Na alikuwa na uwezo wa kuyaeleza mambo kwa watu wa viwango mbali mbali, hiyo moja.

Lakini pili kila tulivyozidi kumfahamu tulibaini kwamba ni mtu mkweli. Waingereza wana neno wanasema *integrity*. Kwa hiyo hili sababu nyingine. Mtu anaonekana hana tamaa.

**IS**: Pamoja na kutokuwa na tamaa, lakini ukweli kuwa alibaki madarakani kwa muda mrefu.

**KNM**: Ndio, kwa hiyo wakati watu katika ule katika mambo yaliyowafanya watu wengi sana waseme huyu lazima atakuwa mtu wa namna yake tu alipokwenda Umoja wa Mataifa mara ya kwanza mwaka ’55 alitumwa na chama. Wenzake katika chama, wazee wa Dar es Salaam wakachanga changa pesa wakamkabidhi

kwa ajili ya safari yake, akaenda akarudi. Sasa hatukuweko sisi wengine kwenye mkutano wa Kamati Kuu. Lakini aliporudi kuja kutoa taarifa, anatoa taarifa ya safari yake, akatoa taarifa vilevile ya pesa alizotumia. Pesa alivyopewa safari pamoja na masurufu. Na akarudisha pesa zilizobaki. Sina hakika sasa hivi, nadhani ilikuwa shilingi elfu mbili na kitu.

Habari zilizotoka sasa, zilizovuja, zikaenea. Wale wajumbe wa kamati kuu ambao walikuwa zaidi wazee wa Dar es Salaam, hawakumuelewa. Wakasema 'Kwa nini unaturudishia?' Akasema 'Nawarudishia kwa sababu pesa hizi mlinipa kwa ajili ya kazi. Mlinipa kwa ajili ya safari mlionituma Marekani, Umoja wa Mataifa. Kazi nimeifanya vizuri, kazi imekwisha na pesa zimebaki. Kwa hiyo sasa hizi nawarudishia mlionipa.' Wanasema wakapigwa… wanasema huyu mtu gani huyu? Sasa watu wengi wakaanza kusema huyu mtu namna gani? Si kawaida. Sasa mambo kama hayo, kila linavyotokea jambo watu wanazidi kumuelewa zaidi. Mambo gani anayathamini na mambo gani anayafikiria hayana maana.

Kwa hiyo nasema Mzee Kawawa kumheshimu na kumuamini Mwalimu alifanya kile ambako wengi, wazalendo wengi wakati ule ambao ni wa kweli ndio hisia walizokuwa nazo kwa Mwalimu.

**IS**: Lakini pamoja na hiyo, sizungumzii kipindi maalumu lakini walikuwepo viongozi wachache ambao walikuwa wanamtii kutokana na uoga kuliko kumuamini na kukubaliana naye. Hata wale ambao hawakuwa na uzalendo wa kutosha.

**KNM**: Hawawezi kukosa hao, hawawezi kukosa, kwa sababu katika nyendo zozote zile, *movement* yoyote. Katika nyendo na harakati hizi, watu wanakuwa na matarajio mbali mbali. Wengine wanaingia katika harakati kwa sababu ni jambo ambalo linatoka moyoni mwao, kwamba wanafikiria jambo ndio sawa na ni haki. Kuna wengine wanafikiria kwamba wakiwemo humo wanaweza wakafaidika huko njiani. Sasa kwa watu wa namna hiyo watakuwa na misimamo ya kinafiki, ya uoga. Kwa sababu

asipofuata msimamo anaweza kukosa mambo ambayo alikuwa anahitaji ayapate kwa ajili yake mwenyewe.

Mimi naamini katika nyendo karibu zote utakuta baadhi ya watu wana matatizo. Kila harakati zinavyopanuka, tatizo la watu wa namna hiyo linakuwa kubwa zaidi.

**IS**: *OK*, kabla hatujaendelea na mengine, suali la mwisho langu kuhusu Mzee Kawawa. Ni kwamba kumekuwa na fununu za muda mrefu tu wakati wa utawala wa Mwalimu, kuwa mara nyingine Mwalimu alikuwa anamtumia Mzee Kawawa kutekeleza yale ambayo yeye mwenyewe hakuwa na uhakika nayo, kwamba kwa kiasi gani yatakuwa yanakubalika.

Na ilipotokea ilipotokea watu kulalamika au kuwa na *blame* Mzee Kawawa alikuwa anabeba mzigo huu kumbe *originally* ilikuwa ni maelekezo au uamuzi wa Mwalimu. Na wengine wanasema kwamba hii ilijitokeza sana mwishoni alipokuwa anar*esign* Mwalimu. Na kwa kiasi fulani alisema hivyo ingawa katika lugha ambayo ni *more diplomatic* lakini alisema hiyo alipokuwa anamsifu mzee Kawawa. Kwa hiyo kadri unavyojua wewe kuna ukweli wowote humo?

**KNM**: Ngumu sana hiyo.

**IS**: Lakini wewe mwenyewe uliwahi kupata hisia kama hizo?

**KNM**: Mimi sijawa nazo. Kwamba Mwalimu alikuwa anamtumia Mzee Kawawa kufanya jambo ambalo yeye mwenyewe analikubali lakini anaona akilifanya yeye pengine yale matokeo yake hayatakuwa mazuri kwake, maana yake kwake. Kwa hiyo anamtosa Kawawa. Hapana, mie sijawahi kuwa na hisia kama hizo.

Isipokuwa nasema, Mwalimu na Kawawa walikuwa ni watu wa aina mbali mbali, kila mtu ana silka yake. Kwa mfano hili suala la *Africanisation*. Katika hili, hatua zile ngumu ngumu zilichukuliwa wakati Mwalimu amejiuzulu. Kwa hiyo unaweza kusema lilifanyika chini ya Mzee Kawawa mwenyewe. Lakini suala lile

lilikuwa lazima lifanyike katika kipindi kile kwa vyovyote vile. Na ndio maana ya kujitawala, maana yake hamuwezi mkachukua, mkashika nchi halafu mkaacha nafasi zile zikaendelea kuwa kama zilivyokuwa wakati wa ukoloni. Maaana yake ni mgongano wa ajabu sana.

Lakini ilikuwa bahati nzuri kwamba ile kazi ilipata mtu hasa anayeiweza. Na wakati katika kipindi kile Mwalimu anafanya kazi kubwa ya kutafakari namna ya kujenga nchi mpya, namna ya kufanya muundo gani wa chama unaofaa zaidi, kutafakari mambo ya serikali. sasa Mzee Kawawa akaifanya kazi ile vizuri sana ya *Africanisation*.

Lakini huwezi kusema alimpa yeye kusudi likiharibika liwe la kwake. Kwa sababu lile si jambo la kuharibika lile. Maana yake likiharibika ni mmeharibikiwa wote. Kwa sababu kutotekeleza vizuri *Africanisation*, kungekuwa ni *a false start*.

**IS**: Kitendo kingine ambacho kilikuwa kinazungumziwa sana wakati ule lakini, ilikuwa ni utaifishaji wa maduka madogo madogo, *retail business*.

**KNM**: Sasa hilo suala la kufunga maduka, suala lile nnavyojua mimi ni uamuzi wa Mzee Kawawa mwenyewe. Na lilituletea matatizo, matatizo ya aina mbili. Matatizo kwa sababu ufungaji wa maduka uliunda mazingira yaliyowapa wananchi taabu kwa sababu maduka yana jukumu lake la kutoa huduma. Sasa mkifunga kwa pupa bila kuwapa kitu mbadala mtapata matatizo. Kwa hiyo tulipata tatizo hilo. Lakini la pili ilikuwa tatizo la kinadharia, la kisera. Na wakati ule ilikuwa tunazungumza juu ya kujenga ujamaa katika nchi. Sasa ndivyo mnavyojenga ujamaa kwa kufuta kwa mpigo huduma ndogo ndogo wanazozitoa wananchi na kuunda mazingira magumu kidogo. Ilikuwa ngumu.

Mimi mwenyewe nilikumbana nalo lile. Kwa sababu nilikuwa wakati ule ni mkuu wa mkoa wa Tanga. Kwenye kikako cha halmashauri kuu ya mkoa, DC wangu mmoja, kwa sababu maDC walikuwa ndio makatibu wa wilaya. Siku zile tuna kofia mbili

kwa chama. Mimi ndio nilikuwa katibu wa mkoa na mkuu wa mkoa. Sasa DC mmoja akauliza ndani ya kikao cha halmashauri kuu ya mkoa, anasema 'Mikoa yote huko watu wanafunga maduka, mbona hapa sisi hatufungi?' Ikawa ngumu kweli. Kwa sababu mimi nilikataa. Mtu akinijia namueleza, namwambia hapana.

**IS**: Lakini kulikuwa na agizo kutoka juu, kufanya hivyo?

**KNM**: Enh, ingawaje mimi sikuliona, lakini inaelekea sijui aina fulani ya maelekezo. Sasa ilibidi niwaambie mle kwenye NEC, madhara yanayoweza kutokea mkijaribu kufanya hilo. Na nikawaambia sisi kazi yetu ni kufungua maduka. Na kazi tunayofanya ni kuzungumza na wananchi, kuanzisha maduka ya ushirika. Kwa hiyo usifunge duka la mtu, kama wewe unapiga vita ubepari anzisha ushirika. Wewe katika wilaya yako zungumza na wananchi kuanzisha ushirika.

Na wakati ule mimi nimeshaanza vuguvugu kubwa la kuanzisha ushirika. Na pale mjini Tanga palikuwa na maduka makubwa ya ushirika. Tena sio Tanga tu, wilayani kote. Na sio maduka tu, nilianzisha mimi ushirika wa ujenzi. Unganisha mafundi ujenzi, wananchi wanaunda ushirika wao wanapewa *tender* za kujenga. Miradi midogomidogo kama kujenga zahanati, kujenga kituo cha afya walikuwa wanapewa *tender* ushirika wa ujenzi.

Kwa hiyo nikawaeleza na nikawa*challenge*. Nawaambia kazi yenu ni kujenga ujamaa. Kama unataka kujenga ujamaa, jengeni ushirika. Kwa sababu ushirika kwetu sisi hapa ndio sehemu kubwa ya ujamaa kwa nchi kama ya kwetu ya ma*peasant* na nini ni ushirika. Bahati nzuri *majority* mle wakaniunga mkono moja kwa moja. *Of course*, walikuwa wanakataa vile vile ufungaji wa maduka. Kwa sababu walikuwa wanapata taarifa za huko Mbeya na wapi na kadhalika.

Sasa ile ilikuwa *problem* kweli na Mwalimu alikuwa safarini. Aliporudi akai*handle* vizuri, akai*defuse*. Mwisho ilikufa, ile sera ilikufa hivi hivi.

**IS**: Ilizungumziwa katika chama, katika vikao vya chama?

**KNM**: Kwenye NEC sikumbuki vizuri. Lazima ilizungumziwa, ndio kwa sababu ya matatizo yaliyotokana na ufungaji. Kwa sababu wakati ule mimi nilipelekwa Mbeya baada ya pale, baada ya muda. Mbeya kule marehemu Wambura ndio alikuwa RC alikuwa amefunga maduka. Nikakuta wamefunga maduka yote. Chunya wamefunga maduka yote. Sasa ilikuwa hali ngumu kweli kweli. Na ilibidi kuzungumza, sisi tulizungumza kwenye halmashauri kuu yetu, tunafanya nini? Namna ya kurudisha huduma kwa wananchi. Sasa yalifungwa kwa mfano Kyela kulikuwa na *problem* kweli pale mjini pale. Karibu huduma zilikufa kabisa, maduka yote yamefungwa.

Kwa hiyo ilibidi kuchukua hatua taratibu na nini bila kukashifiana na nini, lakini kufanya kazi *political work* na nini mpaka mwisho tukaondoka kule tulikofikishwa tukarudi kwenye…

**IS**: Kwa hiyo kama kulikuwa na mazungumzo kati ya Mzee Kawawa na Mwalimu hatuwezi tukajua.

**KNM**: Nadhani bila shaka watakuwa walizungumza.

**IS**: Lakini nje haikuoneshwa kabisa?

**KNM**: Ndio.

**IS**: *Okay* sasa twende kwa wengine kwa sababu ya muda. Ningependa sana jinsi wewe ulivyoona uongozi wa marehemu Sokoine na uhusiano wake na Mwalimu.

**KNM**: Haya, ndugu Sokoine kwa bahati mbaya mimi sikumjua huku nyuma. Nimemjua akiwa naibu waziri katika ofisi ya Waziri Mkuu-Ulinzi. Na nilikuja kutambua kwamba Mwalimu anamfikiria vizuri marehemu Sokoine mwaka ’71 ilipoitishwa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa lengo la kuzungumzia hali ya usalama wa nchi yetu. Nadhani niliwahi kukuambia kwamba nilihusika kwa kupendekeza haja ya kuwa na kikao kama hicho. Sasa siku ile ya kikao … wakati ule mimi bado katibu mkuu wa *TANU Youth League*.

Na Mwalimu tulivyokwenda kwenye kikao cha NEC alichoitisha, baada ya yeye kutoa maelezo ya mwanzoni ya ufunguzi akasema tuanze mjadala. Tulinyoosha mkono watu wengi tu lakini akanitaka mimi nizungumze - kwa hiyo nikawa wa kwanza kuzungumza. Na nikazungumza kirefu kidogo. Sasa ilikuwa kama alitaka niweke misingi ya kuongoza mjadala ule, mambo gani hasa tunataka tuyape uzito. Na moja kubwa lilikuwa wananchi wafundishwe ulinzi wa nchi yao. Na hilo nililieleza vizuri, wazi wazi kabisa, na mambo mengine.

Sasa katika mambo ya kuamua katika hotuba ile yale mazungumzo yangu niliyotoa moja lililotaka uamuzi ni hilo. Kwamba NEC lazima itoe uamuzi, wananchi wafundishwe silaha na ulinzi wa nchi yao ama la. Sasa watu waliosaidia suala la wananchi waweze kufundishwa silaha, yaani suala la ulinzi wa mgambo, mmoja ni mwenyekiti wa Mara, Mzee Nyulandi Chacha, wa pili Edward Moringe Sokoine, na Mzee Kawawa. Katika watu waliochangia sana mimi nilivyowaona. Maana yake suala pale ilikuwa kuufanya mkutano ukubali watu wafundishwe silaha. Maana yake huko nyuma jambo lilikuwa linakataliwa, linaogopwa. Lakini baada yangu mimi kuzungumza na hawa, hasa hawa kuja kuchangia ndio walisaidia sana.

Sasa *session* ile ya asubuhi, iliendelea mpaka kwenye saa nane. Sokoine alizungumza kwenye saa saba hivi, vizuri sana. Alivyoahirisha, Mwalimu anatoka hivi akaniita, akanishika mkono tukatoka wote nje tukasimama pembeni kwenye gari lake. Akaniambia ‘Umemsikia vizuri yule kijana?’ Nikamwambia yupi? ‘Sokoine.’ Nikamwambia ndio nimemsikia. ‘Unamuonaje?’ Nikamwambia ametoa mawazo mazuri sana. ‘Kijana safi sana,’ ananiambia. ‘Kijana safi sana lakini sasa yeye tatizo lake sio kama wewe na baadhi ya wenzako.’ Akasema ‘Yeye hakupata nafasi hakupitia *Youth League*, hakupitia JKT.’ Akasema ‘Tatizo lake hilo hakupitia kama nyinyi kwenye harakati za siasa.’

**IS**: Wakati huo yeye alikuwa ni mjumbe kutoka mkoa…?

**KNM**: Ah, Mwalimu kikao kile cha NEC aliwaalika mawaziri wote na manaibu wao.

**IS**: Kwa hiyo wakati huo Sokoine *already* alikuwa na wadhifa wa serikali?

**KNM**: Alikuwa *deputy minister*.

**IS**: Sabini na moja?

**KNM**: Eeh. Sasa ndio akaniambia 'Usimuache, uwe karibu nae anahitaji kuingizwa katika vuguvugu la siasa.' Kwa hiyo hilo jambo nalikumbuka. Kwamba alikuwa ameshamjua na mchango wake pale umemfurahisha sana; na alikuwa anataka asaidiwe kisiasa. Basi nikamwambia Mwalimu basi vizuri. Na interesting *enough* maana yake siku ya pili jioni, namuona amekuja nyumbani.

**IS**: Yeye mwenyewe?

**KNM**: Eeh, Sokoine, kunitembelea. Nikasema Mwalimu kazungumza naye. Hilo la kwanza kubwa nikajua Mwalimu yuko *serious* naye huyu kijana. Halafu *nineteen seventy-seven* wakati tunaunganisha vyama, mimi nilikuwa Tanga bado. *Of course* nilikuwa katika kamati ile, kamati ya watu ishirini ya kuandaa katiba lakini nikaletewa *message* nije Dar es Salaam nionane nae Mwalimu.

Kuja kumuona akaniambia 'Sikiliza, nitaku*disappoint* lakini nadhani ni vizuri. Frelimo wana *congress*. Wakati sisi hapa tunaunganisha vyama wao wana *congress* yao. Sasa nataka wewe uende kwenye *congress* yao. Nataka uende na Sokoine kwa upande wa TANU. Na Zanzibar *Afro Shirazi Party* watatoa watu wawili.

**IS:** Ilikuwa ni kabla ya mkutano wa kuunganisha?

**KNM**: Kabla ya kuunganisha. Tunajiandaa kuunganisha. Kwa hiyo sisi tukaondoka kwenda Msumbiji. Hata tarehe tano hatukuwepo sisi, tulikuwa kule kwenye *congress* yao.

**IS**: Kwa hiyo kamati ya watu 20 ilikuwa inafanya kazi bila wewe kuwepo?

**KNM**: Sasa tulikwisha maliza kazi yote. Kazi zote zimekwisha imebakia nini tu… Hata mkutano mkuu wa pamoja ulikuwa tayari wa kuunganisha vyama. Kila kitu kilikwisha. Zile *last days* za kwenda kuanzisha kwenye chama kipya, sherehe zenyewe ndio sisi tukaenda huko. Nikasema huyu Mwalimu bwana bado *idea* yake anataka.

**IS**: Wakati huo Sokoine alikuwa *prime minister*?

**KNM**: Hajawa, ilikuwa *February* ile *seventy-seven*. Kuwa *prime minister later*.

**IS**: Lakini katika lile bunge maalum, kiongozi wa shughuli za serikali alikuwa marehemu Sokoine. Wakati ule walikuwa wanapitisha katiba ya nchi.

**KNM:** Sasa si ilifuata. Kwa sababu kwanza tumeunganisha vyama, halafu ile kamati yetu ikakamilisha ile kazi ya bunge maalum.

**IS**: Kuja kwenye bunge maalum yeye alikuwa ameshakuwa *appointed prime minister* au kiongozi wa shughuli za serikali.

**KNM**: Maana yake tumekwenda kule Msumbiji, tukarudi, tena mambo *interesting*. Mzee Diwani kamanda wa vijana akaniita akaniambia 'Unajua Mwalimu atafanya mabadiliko sikuambii lakini ngoja nikunong'oneze, yatamhusu Kawawa.' Akaninong'oneza, nikasema maana yake nini? Basi mimi nikaondoka. *In fact* nilikwenda Tanga. Nikakaa kule haikupita siku inatangazwa Sokoine *Prime Minister*.

Nikasema huyu mzee mkorofi kweli huyu. Maana yake huko nyuma amewahi kuniambia mambo kama haya ya aina hiyo hiyo na yakawa. Nilivyokutana naye nikamwambia wewe mchawi. Usiniseme mambo haya kunihusu mimi, sitaki.

**IS**: Mzee Diwani alikuwa karibu sana na Mwalimu?

**KNM**: Mi nadhani. Ndio alikuwa, wakati mwingine anamtania tu. Anaweza kuzungumza nae *jokingly* lakini *message* inamuingia hata mzee anasikia. Lakini mwenyewe yule anaweza hata kuanzisha mambo.

Kwa hiyo ile *idea* yake kwamba tumsaidie *politically* nikaona. Hata kutupeleka pamoja alijua. Kwa sababu kule Msumbiji tulipewa *villa* moja na *most of the time* tulikuwa tunakaa tunajadili *issues* na nini.

**IS**: Na ulimuonaje mwelekeo wake? Alikuwa ameshasoma soma sana au?

**KNM**: *No*, alikuwa anajitahidi kusoma. Wakati ule alikuwa anajitahidi kusoma. Sasa sina hakika kama amekwishakuwa amejiandikisha kusoma. Maana yake baada ya kuwa *prime minister* alikuwa anajaribu kusoma hata hapa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupata *degree*. Ndio wakati ule alipoachia ngazi akaenda Yugloslavia. Lakini alikuwa anajitahidi kusoma sana. Na hotuba yake kule … kwa sababu mimi sasa kule tukiwa na wenzetu wa Zanzibar hatukuambiwa nani anaongoza *delegation*.

**IS**: Kwenda Frelimo?

**KNM**: Kwa hiyo tukafanya mkutano, mimi na wale jamaa zangu wa Zanzibar tukakubaliana sisi tumuweke Sokoine ndio awe msemaji wetu. Kwa hiyo akaandaa hotuba nzuri sana. Samora aliniuliza 'Huyu bwana unamuonaje?' Unajua Samora likuwa Marxist, watu wote anawauliza kwa msingi wa kiitikadi. Nikamuelezaeleza akasema 'Lakini sisi tunafurahi, ametoa hotuba nzuri sana.'

**IS**: Na wewe mwenyewe kwa uchambuzi wako ungem*place* wapi kiitikadi wakati huo Sokoine?

**KNM**: *Progressive, yes*. Lakini alikuwa hajajifikisha mahali pa kusema hasa… *progressive* ndio, *nationalist*. *Progressive nationalist* maana yake ma*nationalst* wengine magorila. Kwa hiyo nnachoweza kusema ni Mwalimu alimpenda sana Sokoine.

Na jambo moja ali*comment* mbele yangu. Alimuona kwamba ni *honest person*, mkweli, na *of course* mchapa kazi. Alikuwa anapenda sana, ni mtu hasa wa kujituma.

**IS**: Na yeye alikuwa Waziri wa Ulinzi wakati wa vita ya Kagera?

**KNM**: Waziri wa Ulinzi alikuwa Mzee Kawawa, yeye alikuwa *Prime Minister*.

**IS**: Ndio baada ya hapo ndio akaenda Yugoslavia?

**KNM**: Eeh, akapumzika, kisukari kilikuwa kinampa taabu sana ndio maana akaacha. Nadhani aliacha vile vile kwa sababu ya kusoma pengine nadhani alipata nafasi. Lakini na afya yake ilikuwa sio nzuri. Wakaenda kule wakajaribu kumsaidia.

Lakini alikuwa mtu *serious*, mtu makini sana.

**IS**: Sasa baada ya kurudi na kuwa *Prime Minister* for the *second time* sasa ambayo ilikuwa ni kama miaka ya themanini themanini ndio akajitokeza sasa *in public* Sokoine, akaanza kujulikana na watu.

**KNM**: Ndio.

**IS**: *Role* yake katika suala la *economic sabotage* ilikuwaje? Sijui kama unaweza kukumbuka na …

**KNM**: Unajua ndugu Sokoine sasa … unajua wakati ule baada ya yeye kujiuzulu mara ya kwanza na aliporudi akawa tena *Prime Minister*. Sasa ndugu Sokoine alikuwa… kwanza kipindi kile hali ya uchumi ilikuwa ngumu sana. Na kutokana na hali ile ngumu kulikuwa na watu ambao walikuwa wanafaidika sana na hali ile ngumu kiuchumi na hilo lilikuwa linamkera sana.

**IS**: Pamoja na viongozi wa serikali na chama?

**KNM**: Ndiyo, lakini namsema yeye Sokoine lilikuwa linamkera sana. Sasa yeye alikuwa katika sekreterieti ya chama kama katibu wa tume ya ulinzi na usalama kwa muundo wetu wa chama wakati huo. Sasa alikuwa na mawazo ya namna ya ku*deal* na *situation* ile. Upande mmoja alikuwa na mawazo juu ya namna ya

ku*deal* na hawa wanaofaidika na hali ngumu ya uchumi. Upande wa pili alikuwa na mawazo namna gani tunaweza kupunguza makali ya hali ile mbaya ya uchumi. Na yeye alikuwa na pendekezo moja, kwamba kwa nini watu ambao wana pesa zao nje, kwa nini tusiwaruhusu badala ya kuweka huko pesa zao nje walete *goods* hapa, walete mali.

**IS**: Ilikuwa ni pendekezo lake?

**KNM**: Eeh, na wakileta tusiwaulize wewe pesa umepata wapi? Maadamu wanaleta mali ama bidhaa ambazo wananchi wanazihitaji humu ndani waache walete. Kwa mfano usafiri, UDA ilikuwa inashindwa kuhudumia hasa usafiri wa watu. Kwa kweli ilikuwa ni wazo lake yeye. Kwamba kwa nini tusiruhusu watu wenye mabasi binafsi na wao wajiandikishe wachukue abiria kusudi kupunguza makali ya usafiri Dar es Salaam. Kwa hiyo alikuwa na mawazo kama hayo.

Na alileta kwenye sekreterieti tujadili, tunakwenda Msasani tunakaa na Mwalimu tunajadili naye halafu tunawaachia. Kwa hiyo hata ile ya kupambana na wahujumu uchumi ni wazo lake yeye. Ndio njia aliyoifikiria kupambana na wale wanaofaidika na hali ngumu ya uchumi nchini.

**IS**: Na Mwalimu alikubali?

**KNM**: Eeh, Mwalimu alikubali kwa sababu ulikuwa ni uamuzi wa kiserikali.

**IS**: Kwa hiyo hii ilimfanya awe *popular* sana?

**KNM**: Sokoine alikuwa *popular* na alikuwa *popular* kwa sababu kwanza ni mtu kama vile alikuwa ni wa aina mpya. Lakini vile vile hatua zake mbali mbali ziliwafanya watu waamini kwamba anafikiria sana wananchi, alikuwa *popular*.

**IS**: Viongozi wenzake walikuwa wanampenda kweli? Hasa mawaziri na viongozi wengine?

**KNM**: Kwa ujumla nadhani sikuona tatizo. Mimi nilikuwa RC wakati yeye Waziri Mkuu. Nikatoka Mbeya nikaenda makao makuu sekreterieti. Tulifanya naye kazi vizuri, hata kabla kwenye sekreterieti, tulifanya naye kazi vizuri sana, kwa sababu yeye ndio alikuwa mtu muwazi akiwa na jambo lake analisema.

**IS**: Na wewe na yeye mlikuwa karibu?

**KNM**: Ndio, tulikuwa tunaheshimiana sana, sana.

**IS**: Na uliona uelewa wake kiitikadi na kinadharia…?

**KNM**: Ulikuwa unazidi kuongezeka ndio. Kwa sababu kwanza ile nafasi aliyopata kwenda Yugoslavia alisoma sana. Na kufanya kazi na watu kunasaidia sana. Alikubalika vizuri sana.

**IS**: Lakini inawezekana kwamba mara nyingine Mwalimu alikuwa anaona kwamba anavuka mipaka katika kufanya kazi yake?

**KNM**: Mimi sikumbuki.

**IS**: Kwa sababu mimi nakumbuka wakati ule *rumors* zilikuwepo kwamba yeye alitaka katika hiyo *economic sabotage* hata viongozi wengine wa serikali *including* mawaziri wachukuliwe hatua na Mwalimu hakukubaliana naye sana juu ya suala hili.

**KNM**: Sasa pengine inawezekana, mengine ni … sasa kulikuwa na *cases* ama? Maana yake mimi sikumbuki, sikulisikia hilo.

**IS**: Kwa sababu mimi nakumbuka tulisikia sasa huwezi ukajua mara nyingine ukweli uko wapi. Tulisikia kwamba yeye *in fact* aliwaagiza hawa watu, polisi sijui waende kuzingira nyumbani kwa Msuya. Msuya akampigia simu Mwalimu, Mwalimu akawaondosha.

**KNM**: Hiyo sijawahi kuisikia hiyo.

**IS**: Halafu ile pia imemtokea Edward Barongo, hii nafikiri inajulikana, ya Edward Barongo.

**KNM**: Lakini ya Barongo Mwalimu mwenyewe kwani alikuwa nini…

**IS**: Alimtoa.

**KNM**: Ndio alimtoa, Mwalimu alimtoa yule.

**IS**: Na Sokoine ndio alimtia ndani sio?

**KNM**: Ndio lakini alimtoa baada ya… maana yake yale aliyoyafanya, Mwalimu hakuyapenda yale.

**IS**: Aliyoyafanya Sokoine?

**KNM**: Yule Barongo, si alikuwa *charged* na suala la kutoa vibali? Si alikua RC Kilimanjaro? Eeh, alikotiwa ndani si ilikuwa Kilimanjaro. Lilikuwa suala la vibali. Na vibali Mwalimu mwenyewe alitangaza marufuku.

**IS**: Wakati mmoja mimi nakumbuka tulikutana, tulipishana pale Kilimanjaro wewe na mimi. Wewe na mimi.

**KNM**: *Kilimanjaro Hotel*?

**IS**: Na uliniambia kwamba *in fact* ile list ya wahujumu uchumi hasa viongozi wa serikali aliyopeleka Sokoine kwa Mwalimu ili*include* karibu asilimia themanini ya mawaziri. Sasa Mwalimu akasema nikiwatoa hawa wote nitaendeshaje serikali?

**KNM**: Nilisema mimi?

**IS**: Sisi katikati yetu sio hadharani.

**KNM**: Asilimia themanini?

**IS**: Inamaanisa kwamba asilimia themanini ya *cabinet* yake awafukuze. Sasa ataendeshaje serikali?

**KNM**: Sikumbuki kabisa, kabisa.

**IS**: Inawezekana, ni muda mrefu sana.

**KNM**: Sikumbuki kabisa lakini hapana, inawezekana kukawa na *differences* za *opinion* juu ya *issues* fulani fulani. Kama vile

tumezungumza juu ya Mzee Kawawa na Mwalimu. Sio kwamba ku*differ* hawakuweza ku*differ*, hawakuweza ku*differ* katika kipindi chote. Hata kama mtu ambaye mna msimamo mmoja kabisa katika kuendesha serikali mnaweza kufika mahala mmoja anafikiria tutende hivi, mwingine anafikiria tutende hivi.

**IS**: *Exactly*. Halafu tuje kwenye marehemu Karume kwa kiasi unachofahamu wewe uhusiano kati ya Mwalimu na Mzee Karume.

**KNM**: Uhusiano kati ya Mwalimu na Mzee Karume siujui sana kwa sababu wakati Muungano unatokea… Naujua tu tangu *Afro* inaanzishwa. Na Mwalimu aliwahi kutuambia hapa baadhi ya vijana wake sisi kwa nini TANU lazima ifanye kazi kwa karibu na *Afro Shirazi Party*. Lakini kwa sababu mimi niliondoka baadaye kwenda nje, yaliyotokea huku nyuma sikuyaweza kuyaona.

Kwa jumla walikuwa wanashirikiana. Kwa mfano Azimio la Arusha alilitangaza yeye mwenyewe Mwalimu. Muongozo wa sabini na moja *of course* ulitangazwa na NEC lakini tulikuwa na utaratibu wa kupokelewa na wananchi. Kwa hiyo mimi nilikwenda kumuomba Mwalimu kwamba tunaandaa - nilikuwa bado Katibu Mkuu wa Vijana. - tunaandaa maandamamo na mkutano mkubwa ili aje kupokea Muongozo mwaka sabini na moja. Nilivyokwenda kumueleza Msasani akasema safi, sawa sawa. Lakini akaniambia ‘Sikiliza, hili suala kubwa. Suala la kisera hili. Mimi nadhani sasa mimi nimehusika moja kwa moja na kupitisha kwenye NEC. Sasa nenda Zanzibar kamuombe Mzee Karume. Nenda kamwambie Songambele RC uende nae kwa Mzee Karume. Muombeni aje kupokea maandamano yenu.’

Nikasema sawa, tukaenda mimi na Mzee Songambele tukazungumza naye akakubali. Akaja hapa akaupokea Muongozo. Akatoa hotuba nzuri tu ya kuhamasisha vijana.

**IS**: Na uhusiano wa Mwalimu na Mzee Jumbe?

**KNM**: Mwalimu na Mzee Jumbe nao siwezi kusema mengi sana kwa sababu sikuwa msaidizi wao wa karibu lakini ulikuwa mzuri sana. Na mimi Mzee Jumbe aliwahi kuniambia wakati ule niko Tanga, alikuja kututembelea Tanga. Alikuwa ananiambia mambo chanya kabisa, *very positive* juu ya uhusiano wake na Mwalimu Nyerere kama rais.

**IS**: Sasa kulikuwa na *basis* gani ya *eighty-three* ya machafuko ya hali ya hewa na ule mkutano wa NEC wa Dodoma? Na wewe ulikuwepo?

**KNM**: Ndio, kwenye mkutano ule ilikuja *issue* ya kwamba Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar ana mambo anayafanya chini kwa chini kuhusiana na suala la muungano. Anaandaa maadishi ya kutaka *restructuring* ya muungano. Na ushahidi upo. Kwa hiyo lilikuja katika sura hiyo. Sasa ikaonekana basi ni vizuri yeye aulizwe. Kuna hili, hili, hili linasemwa, lina ukweli gani? Sasa ili kutia nguvu ya hayo yanayosemwa baadhi ya wajumbe wakawa wanatoa ushahidi. Wanatoa ushahidi ... Basi mpaka mwisho ikaonekana ushahidi ule ni mzito na yeye mwenyewe anashindwa kujitetea sawa sawa. Sasa nadhani inaonekana alivyoona ushahidi uliomzunguka *overwhelming* ndio mwenyewe akatamka kwamba bora yeye ajiondoe kwenye madaraka.

Kama ni uhusiano mbaya kati ya watu wawili hawa basi ni jambo la miaka au mwaka ya karibu karibu, mwisho mwisho. Lakini tangu ashike uongozi wa Zanzibar wengine tulivyoona, mimi nilivyoona uhusiano wao ulikuwa mzuri tu.

**IS**: Wakati Mwalimu anapo*step down eighty-five* na chama kilikuwa kinazungumzia suala la nani atakuwa *successor*, wewe ulikuwamo katika mkutano wa *Central Committee*, ulikuwa *member* wa *Central Committee*?

**KNM**: Eeh. *(Anakubali)*

**IS**: *How did the whole procedure go*, ilikuwaje? Kwa sababu huku nje tulikuwa tunasikia kwamba Mwalimu alikuwa na *choice* yake ya Salim Ahmed Salim, sijui nini.

**KNM**: *Yeah*, unajua wakati ule wakati muda unakaribia yaani tarehe za kwenda kwenye uchaguzi zinakaribia bado kulikuwa na vuguvugu la wananchi waliokuwa wanadai wanataka Mwalimu aendelee. Kulikuwa na ujumbe mbali mbali na kwenda kumshawishi asiache. Sasa sisi katika sekreterieti tulikuwa tumefanya uamuzi kwamba hili suala la Mwalimu kuendelea ama kutoendelea ni vizuri kama chama tulifanyie kazi. Kwa hiyo tulijadili katika sekreterieti kwenye vikao kadhaa, kwa hoja mbalimbali na kutafuta taarifa nchini. Baada ya majadiliano … nadhani yalichukua muda mrefu, nadhani karibu miezi mitatu.

**IS**: Katika kutafuta…

**KNM**: Msimamo wa chama ambao tutaupendekeza kwenye Kamati Kuu. Basi tukaupata. Tukakubaliana tuishauri Kamati Kuu kwamba Mwalimu ametangaza nia yake ya kutoendelea kuwania nafasi ya urais. Lakini kumekuwa na wananchi mbalimbali wanaotaka asifanye hivyo, kwamba aendelee. Sasa sisi baada ya kulitizama suala hili kwa mapana yake, tukapendekeza kwa Kamati Kuu kwamba ni vizuri tukubaliane na Mwalimu katika msimamo wake wa kutaka asiendelee.

**IS**: Kwa nini?

**KNM**: Tulikuwa na hoja zetu. Kwa kifupi tu: ya kwanza ni yeye mwenyewe amesema hivyo. Alisema hivyo nyuma, alikuwa tayari kuachia ngazi mwaka 1980, wananchi wakakataa. Na kwa sababu ya hali ilivyokuwa wakati ule, mara tu tumetoka kwenye vita, akakubali maoni ya wananchi walio wengi.

Lakini sasa imepita miaka mitano amesema tena kwamba safari hii hatachukua tena. Kwa hiyo kwanza yeye amekwishasema na sisi tunamjua alivyo, tabia yake sio mtu anayebabaisha. Kwa hiyo ni vizuri tuheshimu matakwa yake kwa sababu na yeye anayo matakwa na anazo sababu anaona kwa nini asiendelee.

Lakini la pili kuna faida kwa nchi kwa sababu yeye anaacha nafasi hiyo haachi nchi. Yeye ni raia wa Tanzania tena ndio ni raia namba moja. Kwa hiyo kuacha kwake wakati yeye ana nguvu

na akili zake timamu, atatusaidia sana kwa busara zake kuendelea kulilea taifa hili kwa namna mbalimbali sio kuendesha nchi lakini kama mzee wa nchi. Kwa sababu ya historia yake na nafasi yake katika nchi hii, kuwepo kwake pale pembeni itakuwa ni faraja kwa wao walioko serikalini na wananchi wanakuwa na imani kwamba… wanasema 'Mwalimu yupo, mzee wetu yupo, hakiharibiki kitu hapa.' Kwa hiyo itajenga imani na hawa walioko madarakani wataweza kufanya kazi zao kwa utulivu.

Kwa hiyo tatu tulisema anatujengea historia kwamba ni utaratibu mzuri kwamba ukishika madaraka makubwa kama haya ni vizuri unatoka vizuri vilevile. Sio kutoka unanuka. Yeye atatoka lakini taifa litakuwa bado linamuheshimu na kumpenda. Na bahati nzuri ametuletea wazo la kuweka vipindi - katiba mpya iweke kikomo kwenye kushika madaraka ya urais. Kwa sababu lile ni wazo lake yeye. Na hili ni wazo zuri sana ametuachia. Nalo lengo lake ni hilo hilo tuweze kuwa na viongozi ambao watatoka katika hali ya amani na utulivu.

Kwa hiyo mengine tuliyosema siyakumbuki. Lakini kwa kifupi tulikuwa na hoja zetu kwamba tukubaliane naye kwa sababu anatujengea hatubomolei nchi. Kwa hiyo tukaenda kwenye kamati kuu tukatoa ripoti yetu.

**IS**: Wakati huo sekreterieti yenu ilikuwa inaongozwa na Mzee Kawawa?

**KNM**: Ndio alikuwa bado yeye. Baada ya pale sasa ndio Mwalimu akasema basi, akasema 'Kwanza nawashukuruni nyinyi sekreterieti; mngekuja na mawazo mengine hapa tungepambana. Kwa sababu kwanza ningewaulizeni kwanza nani kawapeni nyinyi madaraka ya kuja kuwaamulia watu hapa?' Kwa hiyo akafurahi sana. Tukasema sasa maadam tumemaliza hili, kikao hiki tunatakiwa tutoe pendekezo, watu. Kwa hiyo tuanze kazi ya kuzungumzia suala la urais. Kwa hiyo Mwalimu akapendekeza 'Suala la urais tusianze kuzungumza watu, kwanza tuzungumzie sifa za urais. Katika mazingira ya sasa hivi mnafikiria rais awe na sifa zipi? Na katika hili mimi napendekeza kila mmoja wetu

aseme, atoe sifa anazofikiria yeye, ndio wazo langu. Sawa?' Wajumbe wakakubali tuzungumzie sifa za rais.

Basi ikaanza duru ikazunguka, wote, kila mmoja. Wote tulipomaliza na yeye aka*sum up*. Yeye alikuwa anasikiliza tu kila mtu akizungumza alikuwa ana*jot down* mambo yake. Mwisho akajaribu ku*sum up*. Basi akasema 'Sasa basi tumeshapata mawazo rais tunayemuhitaji awe na sifa hizi. Sasa tuanze: Sheikh Mwinyi, Salim Ahmed Salim, Katibu Mkuu Ndugu Kawawa nyie tupisheni nendeni chumba cha pili huko wametengeneza'

**IS**: Yeye mwenyewe amechagua hawa watu watatu?

**KNM**: Yeye mwenyewe alisema 'Nyinyi tokeni tunataka kuanza kazi.' Mzee Kawawa akakataa. Akatuambia 'Mimi mwenyekiti wacha nibaki hapa hapa kwa sababu mimi sitaki mnifikirie. Si mnataka mtufikirie? Mimi sitaki mnifikirie nna matatizo mawili. Kwanza afya yangu sio nzuri, lakini la pili ambalo ni kubwa nalo mimi na Mwalimu huwezi kututenganisha. Mwalimu anaondoka baada ya miaka mingi ya uongozi. Lakini anaondoka kwa hiari yake mwenyewe na kwa maslahi ya nchi na anataka vile vile alete sura mpya. Sasa yeye anaondoka mimi nikibaki, mkikosea mkaniweka mimi si watu watasema hakuna lolote? Hakuna badiliko lolote? Kamuacha mwenzake huyu. Kwa hiyo mimi… '

**IS**: Ilikuwa ni *powerful argument* hiyo. 'Kwa hiyo mimi nakuombeni nibaki.' Ah wapi! Tukasema utoke. Basi akatoka shingo upande. Lakini tukasema mwenyekiti kwanza tuzungumze habari za Mzee Kawawa. Maneno aliyoyasema magumu yale. Na Mwalimu naye akasema 'Lakini kweli, Rashidi bwana mjue ndio hataki vile. Kwa hiyo mnasemaje?' Tukasema arudi. Kwa hiyo akaenda kuitwa arudi.

Basi Mwalimu akamwambia 'Bwana, tumekubali bwana hoja zako ngumu kweli kuzikataa. Kwa hiyo kaa bwana tushirikiane.' Kwa hiyo ndio tukaanza. Nani wa kwanza? Mwenyekiti akasema 'Wa kwnza lazima kumchukua *senior* kumjadili. *Senior* ni Makamu wa Rais.'

Ndio tukaanza kumzungumza Mzee Ali. Tukamzungumza, kila aliyemzungumza ni *positive*. Mazungumzo yakaenda kwa namna ambapo tulivyofika mahali hakuna mtu mwingine tena wa kutaka kusema, ikaonekana ni mtazamo wa wote. Kwamba yeye ndiyo mwenye sifa zile tulizotaka tuwe nazo.

Kwa hiyo mwenyekiti akasema 'Maadam tumeona huyu ndiyo mwenye sifa, hatuna sababu ya kumuita mwingine. Ama hatuna haja ya kumjadili mwingine. Sasa tumeshampata katika duru ya kwanza tumeshampata mtu tunamtaka.' Kwa hiyo tukakubaliana mtu wa kumpendekeza kwenye halmashauri kuu ni Sheikh Ali Hassan Mwinyi.

Kwa hiyo wakaenda wakaitwa Mzee Mwinyi na Sheikh Salim Ahmed Salim. Mwenyekiti akawaeleza uamuzi wa Kamati Kuu ni huu. Ndivyo mambo yalivyokwenda.

**IS**: Hakuna ukweli wowote katika hiyo *rumour* kwamba Mwalimu alikuwa anamtaka Salim Ahmed Salim lakini Wazanzibar walipinga kutokana na tofauti za huko huko Zanzibar?

**KNM**: Hakuna lililojitokeza kwenye Kamati Kuu. Kwanza kwamba Mwalimu angependa Salim sio jambo la kificho sana. Lilikuwa linajulikana lakini yeye mtu wa demokrasia. Ndio maana ya kuwa na utaratibu wa kidemokrasia kama tulivyoutumia. Watu wazungumze kila mmoja atoe maoni yake. Sasa maoni yote yameoana.

**IS**: Lakini hebu tuzungumze kwa kiasi tunavyofahamu wewe na mimi siasa zinavyoenda. Wakati ule kama Mwalimu kweli angemtaka Salim Ahmed Salim, angeshindwa? Au kulikuwa na pingamizi?

**KNM**: Hapana. Yaani angemtaka katika maana ya yeye angesema, kuiambia NEC, Kamati Kuu, kwamba tumpendekeze huyu?

**IS**: Kwamba mimi naona yeye ndio ana sifa. Kwa sababu ukiangalia sifa, ukilinganisha sifa za Salim Ahmed Salim na Mwinyi wakati ule, kwa *criteria* hizo tu, inakuwa vigumu kusema kwamba Mzee Mwinyi alikuwa na sifa zaidi ya Salim.

**KNM**: Aa! Sasa unajua, unazungumza sifa za kuwa rais. Kwa hiyo sifa zile ni pamoja na sifa ya kuweza kukubalika katika mazingira ya Tanzania ya sasa. Sasa hao wajumbe waliotoa maoni walikuwa wanatazama nani anaweza kushika kiti kile na akakubalika kote kote. Hilo lilikuwepo na ni *sentiment* ambayo ilitoka katika mazungumzo.

**IS**: Kote kote kwa maana ya pande zote mbili za muungano?

**KNM**: Ndio. Kwa sababu hata Zanzibar wenyewe sio kwamba wajumbe wote walikuwa wanamtaka Salim. Lakini vile vile huwezi kusema Wabara…

**IS**: Wote walikuwa wanamtaka Salim, ni kweli.

**KNM**: Eeh. Ni *complex* kidogo kwa sababu … ah! bwana we… individuals kila watu wana… Halafu kuna mazungumzo ya nje huwezi kujua watu wamezungumza vipi huko na nini. Maana yake kwenye vikao wakati mwingine ni *reflection* ya watu waliokubaliana huko nje. Ingawaje huko nje hakuna mkutano uliowachukua wajumbe wote wa maana. *No*, kwa wakati ule ilionekana kwamba… kwanza kitu chenyewe wakati huo unaogopa urais, si ndio mara ya kwanza mnabadilisha. Sasa mpateni mtu ambaye ataweza kukubalika.

**IS**: Kwa sababu kwa mfano, Mzee Kawawa aliweka wazi kabisa. Sasa kama Mwinyi pia angefanya hivyo?

**KNM**: Angefanya hivyo… maana yake kama wajumbe wangekubali… Maana yake Mzee Kawawa alitoa hoja zake na wajumbe wakazikubali. Sasa Mzee Mwinyi angetoa hoja … Manake kulikuwa na jitihada fulani ya kusema kwamba Mzee Mwinyi asichukuliwe kwa sababu anafaa Zanzibar, ilikuwa inasemwa, lakini watu waliikataa hiyo. Kwenye Kamati Kuu

haikuzungumzwa hiyo lakini kwenye NEC ilijitokeza. Kwa sababu sisi si tulipeleka kwenye NEC, kwenye NEC ilijitokeza. Lakini wajumbe waliikataa hiyo, hiyo hoja gani? Mnasema kwamba mzuri Zanzibar, hiyo iwe hoja ya kuwaambia huyu mzuri anayeonekana anafaa Zanzibar asiwe mzuri kwa Tanzania nzima?

Badala ya kusema hiyo hasa ndio sababu tunaona amepaweza pale, basi anapaweza pote. Angalau kafanya mahali… maana yake Zanzibar ni mahali pa *divisions* kuliko bara. Na visiwa wakati wote ni maeneo magumu sana kuya*handle*. Kwa hiyo tuliendelea hivyo.

**IS**: Nafikiri Mwalimu aliendelea kuwa mwenyekiti wa chama baada ya *eighty-five*, miaka miwili.

**KNM**: Ndio.

**IS**: Lakini baadaye muda uliengezwa, haku*retire eighty-seven*, ingetakiwa a*retire eighty-seven* siyo? Ilikuwa nini?

**KNM**: Ndio, sasa kwa sababu katika utaratibu wetu hatusemi mwenyekiti aliopo lazima aondoke ili ampishe aliye rais, ni kama *gentlemen's understanding*. Na kwa Mwalimu na Mzee Mwinyi ilikuwa ndio mara ya kwanza. Na huyu ndio *founding father*, sasa *problem*. Kwa hiyo *eighty-seven it was overwhelming* akachaguliwa tena Mwalimu. Sasa baada ya *eighty-seven* naona Mwalimu alikuwa anajiandaa kung'atuka. Kwa sababu *ninety* kung'atuka kwake alifanya *decision*.

**IS**: Kwa hiyo hakumaliza miaka mitano?

**KNM**: Ndio hakumaliza.

**IS**: Na kulikuwa na sababu maalum kwa nini yeye akakubali kuendelea baada ya *eighty-seven*?

**KNM**: *No*, kwa sababu *issue* haikujitokeza. Kwa Mwalimu haikujitokeza *issue* kwamba ampishe rais. Kwa wengine wanaofuata inajitokeza.

**IS**: *Okay*, nina masuali mawili tu ya mwisho. Moja ni Mwalimu na uhusiano wake na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *debate* zilizokuwa zinajitokeza pale *sixties, seventies* wakati wa enzi ya kina Walter Rodney na enzi yetu tulipokuwa tuna*publish* ile *magazine* yetu Cheche na makala mbali mbali tulizokuwa tunaandika. Katika mazungumzo yako na Mwalimu, sitaki kujua kiserikali lakini *personally* mazungumzo yako na Mwalimu alionaje hii?

**KNM**: Kwanza mimi nilivyomuona Mwalimu, alikuwa anafurahia sana juu ya muamko wa kisiasa uliokuwepo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hasa baada ya Azimio la *Arusha*, kuanzia pale alikuwa anafurahia sana. Na alikuwa anafurahia kwamba kuna wahadhiri na wanafunzi wenye mwamko huo. Na alikuwa anafurahia sana kila akipata nafasi ya kwenda pale. Na yeye kwa sababu ni msomi, ni *intellectual* alikuwa anafikiri anapata nafasi nzuri ya kutoa mawazo yake lakini vilevile anakuwa *challenged* na anaona raha sana. Halafu alikuwa anafurahia ana*communicate* vizuri sana alikuwa ana*communicate* na viongozi wa vijana pale Chuo Kikuu wa *Youth League* yetu pamoja na serikali ya wanafunzi. Alikuwa na *communication* nzuri sana, mahusiano mazuri sana ambayo na mimi alikuwa wakati mwingine ananishirikisha kwake kule Msasani.

Sasa kwa mawazo, sasa kulikuwa na nyakati alikuwa hakubaliani na baadhi ya mawazo. Kwa hiyo ilikuwa yanamkera mpaka wakati mwingine anasema 'Hawa vijana wangu namna gani, wanaelewa hawa mambo?' Nadhani nilikueleza juu ya suala lile lililotokea la Frelimo, hilo moja. Wakati mwingine *analysis* kali kali za *publication* yenu ile…

**IS**: Cheche.

**KNM**: Cheche, wakati mwingine alikuwa kidogo… Halafu kwa mfano Dk. Rodney kwa ujumla alikuwa anampenda sana ingawa wakati mwingine alikuwa kidogo na *reservations* anasema 'Hawa jamaa mbona maneno yao makali tu? Hawajui jinsi tunapambana katika hali ngumu? Wao ni ku*criticise* tu.' Lakini kwa ujumla

alikuwa anajiona yuko karibu sana na *intellectual community* ya Chuo Kikuu hasa ya wakati ule *sixties* na *early seventies*. Maana yake baadaye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilibadilika kwenye mawazo. Na alikuwa anajivunia *in fact*. 'Vijana wanasema nini Mlimani?'

**IS**: Alikuwa anakuuliza wewe?

**KNM**: Eeh, wanasema nini? Sasa kama ninazo habari, najua wanachosema kule namwambia. 'Sawa basi, sawa, hiyo sawa sawa, nzuri sana.' kwa hiyo mimi nadhani alikuwa anaona mtoto yule kama mtoto wake lakini mtoto mzuri sana. Kwa *role* ya wakati ule, *it was really*…

Unakumbuka kwa mfano kulikuwa na suala la Hilton Hotel kujengwa karibu ya Ikulu. Sasa nyinyi kule Mlimani mkatoa statement kali sana kupinga kabisa kabisa, msimamo wa vijana. Mimi ni katibu mkuu sasa ntafanyaje? Vijana wengine wa mjini nao wanaunga mkono lakini serikalini kwake walikuwa na mashaka sana na msimamo ule hawautaki. Na *ministry* haitaki. Sasa mimi nilijua kuwa ule msimamo una *problem*. Na Mwalimu amenyamaza, yeye hakusema. Sidhani kama angependa kuiunga mkono moja kwa moja hiyo *position*. Lakini nikasema sio kitu, mimi nikasema ngoja nita*deal* nayo hiyo. Sasa ili kulifanya lile suala kulitupa, kuwatupia upande wa serikali mimi nikatoa *statement* ya kum*challenge* Waziri wa Utalii.

**IS**: Alikuwa nafikiri marehemu Makame.

**KNM**: Ndio marehemu Makame. Kwamba sisi *Youth League,* mimi nitaitisha mkutano wa hadhara kule kule pwani pale wanapotaka kujenga hiyo *hotel*. Na vijana watakuja pale watajaa na wananchi wenye kupenda watakuja. Tutamuomba yeye Waziri aje awaeleze wale vijana na wananchi, kwa nini katika maeneo yote hapa Dar es salaam wameona pale karibu ya ikulu ndio panafaa. Nikaitoa *statement*, nikaitisha mkutano.

**IS**: Mwalimu alijua hiyo?

**KNM**: Ndio alijua.

**IS**: Na hakupinga?

**KNM**: Hakupinga, kanyamaza kimya lakini hakupinga. Sasa nikapata habari mke wake marehemu kanali (Ali) Mahfoudh, mke wake alipanda ndege na Waziri Makame, ndege moja toka Zanzibar wanakuja hapa. Sasa tukakutana na Ali, Ali akaniambia 'Ngoja shemeji yako akueleze maneno.' Akaniambia 'Wewe bwana unachukiwa wewe!' Akasema, 'Nikuambie vipi? Tena nimesafiri naye Waziri wa Utalii. Amesema maneno. Anasema 'Huyu Ngombale yeye anajifikiria yeye ni nani katika nchi hii? Yeye anatu*terrorise* na vijana wake. Sasa anaitisha mkutano eti niende mimi niende pale nikawaeleze. Nitaeleza kitu gani? Si huyu mtu hatari kabisa! Mwalimu kwa nini huwa anampenda sana huyu kijana? Hafai kabisa huyu.'' Akaniambia 'Bwana yule bwana amezungumza kwa hasira kweli, unawa*terrorise* watu'. Nikasema haya.

Sasa nilivyojua Mwalimu anafikiria nini, baada ya ule mwongozo wa *seventy-one*. Baada ya pale mimi akaniteuwa kuwa RC na katibu wa mkoa nianze kazi ya mgambo. Pale *TANU Youth League*, *deputy* wangu marehemu Michael Baruti, akamfanya Katibu Mkuu.

Sasa Michael marehemu alikuwa na wasiwasi sana. Na nilikuwa namjua, mambo haya mengine alikuwa anaona *extremist*. Anasema 'Wewe bwana unakubaliana nao vijana hawa wa Chuo Kikuu na nini.' Mimi nimeondoka anasema 'Sasa hili suala la hoteli ya Hilton na tumeshaitisha mkutano wa Waziri. Sasa tunafanyaje? Mwalimu anakubaliana nalo hili?' Nikamwambia 'Sikiliza, suala sio Mwalimu kukubaliana nalo, kama vijana wana maoni yao juu ya jambo hawawezi kungoja kwanza wamuulize Mwalimu, wewe Mwalimu unaonaje. Hapana, wao wanaweka msimamo. Na lazima wawe na hoja zao. Sasa wewe tatizo lako unafikiria Mwalimu analipinga hili? Basi kama ni hivyo nikamwabia twende kwa Mwalimu nikusaidie. Kama analipinga basi atalisema mbele yangu.' Tukaenda ofisini.

**IS**: Kwa Mwalimu?

KNM: Eeh. Nikamwambia Mwalimu, rafiki yangu hapa ana tatizo. Nimemuachia mambo magumu magumu. La kwanza nimemuachia hili suala la kubadilisha umri wa vijana ambalo nilitaka tuwe na *limit*. Maana yake kulikuwa vurugu tupu. Na walishindwa *of course* alishindwa kwenye mkutano ulioitishwa. Sasa hili nikamwambia Mwalimu rafiki yangu ana tatizo juu ya suala la ujenzi wa hoteli karibu na ikulu. Vijana tuliweka msimamo na msimamo ni kumuomba Waziri aje kuwaeleza vijana kwa nini anafikiria pale ndipo mahali hasa *appropriate*. Sio sasa wanachukulia wanapinga kujengwa hoteli. Aje kujenga hoja zake kwa nini pale ndipo panapofaa kuliko mahali popote hapa Tanzania ama hapa Dar es Salaam.

Mwalimu akasema 'Aah! Nyi mnajua mimi nimenyamaza kimya mlipoanza mambo yenu. Vijana wa Mlimani wametoa *statement* yao kali mimi nimesoma nimenyamaza tu. Nikawangojea nyinyi mta*react* vipi. Na nyinyi mkawa wajanja mkabadilisha mkafanya ni *challenge* kwa Waziri. Safi sana! Mimi sikubaliani na nyinyi juu ya *location* kusema hapa hapafai kujenga hoteli kwa sababu ni karibu ya ikulu. *Technology* ya siku hizi mnafikiria inajali haya mambo mnayosema nyinyi? Hivi sasa mnafikiri hawajui *what is happening* ikulu? Hivi sasa wanajua. Kwa hiyo mimi habari ya *location* mimi sikubaliani na nyinyi kabisa. Lakini nakubaliana na nyinyi, lazima waziri aje kueleza wananchi, ni *challenge* kwake lazima aeleze. Kwa nini unaona pale ndio panakufaa? Maana yake Dar es Salaam kubwa hii, kwa nini  lazima ijengwe karibu na ikulu? Sasa waziri anayekimbia anaogopa kwenda kueleza wananchi basi hafai na *project* yake haifai.'

Michael Baruti akapumua bwana akasema 'Aah! Sasa mambo mazuri sana. Mwalimu tena umenisaidia maana yake nilikuwa natafuta mahali pa kutokea.' Basi tukazungumza naye akasema 'Hapana mimi sina ugomvi na vijana sina ugomvi nao, wana haki ya kuhoji. Lakini hawa mawaziri wangu wakihojiwa na wanachi

lazima wajibu. Wakishindwa kujibu, wao ndio tatizo. Kwa hiyo waziri wangu yule nasikia anaogopa kukutana na wananchi.’

Kwa hiyo ndio nilikuwa nasema Mwalimu alivyokuwa anachukua *challenges*…

**IS**: Mkutano uliitwa?

**KNM**: Ah! Waziri alikataa; si alisema mimi nawa*terrorise* na nini. Alikataa lakini na hoteli yenyewe haikujengwa. Kwa hiyo alikuwa anapenda sana. Hali ya Chuo Kikuu ilkuwa inamtia moyo sana. Lakini kulikuwa na wakati yeye ambapo *we didn’t see eye to eye*. Maana yake nyie bwana wanamapinduzi zaidi sasa…

**IS**: Unaweza kukumbuka *incidence* zingine ambapo alikuwa na wasiwasi juu ya msimamo wa Chuo Kikuu?

**KNM**: Sasa hapo… sasa hivi sikumbuki. Na *of course* wakati ule kulikuwa watu ambao hawapendi msimamo wa wanafunzi na wahadhiri wa Chuo Kikuu, ule msimamo wa mrengo wa kushoto. Kwa hiyo kulikuwa na watu ambao walikuwa wanasemasema, wanagunaguna kwa nini bwana mkubwa anawaendekeza sana hawa. Enh. Na wengine walikuwa wanafikiria *problem* ni mtu kama Rodney. Hawawezi kuona kwamba ziko *ideas* ambazo ni *universal*. Watu wanakubaliana juu ya mambo fulani fulani, sio mambo haya ya wageni, ya nani.

**IS**: Pale mwishoni Mzee Ngombale uliwahi kumuona alipoenda hospitali ya St. Thomas kule Uingereza?

**KNM**: Rais Mkapa aliponipa jukumu lile la kwenda kushirikiana na familia kumuuguza. *Yeah* nilifika lakini nilifika wakati huo hana kauli.

**IS**: Ufahamu pia alikuwa amepoteza?

**KNM**: *Well*, sina hakika kama alikuwa nao. Kwa sababu alipokuwa alikuwa hana kauli, lakini alikuwa hali ilikuwa hali ngumu sana. Tulikua tunaishi kwa matumaini tu. Maana yake kila siku unakwenda unamtazamaa.

**IS**: Sawa, Mzee Ngombale nakushukuru sana sana sana. Kwa sababu lazima kila kitu kiwe na mwisho wake. *Otherwise* tungeweza kuendelea kuna mambo mengi sana.

**KNM**: Sasa, unataka kuyatumiaje haya mazungumzo yetu, manake mimi niko kwenye *process* ya kuandaa *biography* yangu. Tena nina *appointment* na Walter Bgoya nataka nishirikiane naye mapema kusudi baadaye wao wa*publish*.

**IS**: Kwa hiyo umeshaanza kuiandika?

**KNM**: Nimeanza kukusanya mawazo yangu.

**IS**: Kwa hiyo Mzee Ngombale nimefurahi sana, *it is very good*. Utuachie bwana *something*, maana vijana wetu… hii itakuwa ni safi sana. Tena ungechukua muda tena *concentrate*, *just concentrate* ili iweze kutoka mapema.

**KNM**: Nilikuwa nafikiri kuanzia *September* ntakwenda Kilwa nikae kidogo ni*study* ile *environment* yenyewe. Na kuna watu wachache *I hope* watakuweo bado nikienda *September* maana yake mjomba wangu mmoja yupo, *he is now seventy-eight*. Nina masuali naye kidogo. Na yuko baba mdogo *eighty-eight or so*. Lakini watu wengi wameshaondoka, *generations* zile. Bahati mbaya katika familia yetu kulikuwa na baba yetu mkubwa wa kati. Maana yake yule mkubwa kabisa Said Ngombale yeye wala hakuwa *literate* katika maana hii ya sasa. Lakini yule Mzee Ambrose yeye alikuwa kama *chronicler;* vi*notes* mbali mbali aliandikaandika. Sasa alipofariki kuna mjukuu wake mmoja kafanya mambo ya hovyo sana. Kaenda kwenye makaratasi yake na nini, mengine kayatawanya, mengine kayachoma moto. *A lot of information*.

Tena nilikuwa nataka wanitafutie barua yangu. Kwa sababu nilipoacha kazi ya ukarani ili nifanye kazi *full time* kwenye chama tulikosana na mzee wangu, baba yangu. Yeye alikuwa Bagamoyo huko anafundisha. Tulikosana sana. Akasema ‘Wewe unaaacha kazi unakwenda kwa Nyerere. Ulikuwa unapata mshahara mzuri na nini na nini.’ Yeye na baba mkubwa yule walikuwa kila kitu

wanaelezana. Yule kule mambo ya kule Kilwa lazima anamuandikia huyu anamueleza kila kitu. Na yeye huyu mambo yote ya familia na nini anampelekea. Sasa akamwambia habari zangu, ‘Mtoto huyu kachanganyikiwa siku hizi. Kaacha kazi anamfuata Nyerere huko sijui nini.’ Maneno chungu mzima. Yule mzee alikuwa katekisti, ndio aliyepeleka kanisa Kilwa. Unajua Kilwa yote ni ya Waislamu isipokuwa Kipatimu tu. Ndiye aliyeanzisha kanisa pale.

Basi akaniandikia barua *fourteen pages* ananiasa. ‘Wewe mtoto namna gani unataka kujiingiza katika mambo? Wewe hujui wewe mambo ya Maji Maji hapa, watu wamepata taabu? Sijui nini na nini.’ Halafu mambo ya dini ananiandikia humo meeengi kweli. Sasa mimi nikamjibu, *twenty-four pages*. Nikasema huyu mzee ngoja nitamzidi kwa kurasa na maneno. Lakini nilimueleza sana juu ya suala lenyewe la *liberation struggle* sasa hivi. Na vile vile atofautishe Maji Maji na mapambano ya sasa. Nikamueleza sana. Sasa nilikuwa naitaka ile barua.

**IS**: Hizi zikipatikana hizi, itakuwa safi sana.

**KNM**: Ningeipata ile barua… sasa ndio wakaniambia. Nikawaambia *look*, yule mjukuu wa Mzee amepoteza *documents* zote, *records* zote za Mzee alivyofariki hovyo kabisa. Kwa hiyo nitakwenda huko halafu nitatumia muda Rufiji. Lakini nitatembeatembea vile vile nchini, hata maeneo haya nimefanya kazi kama Katibu wa Mkoa. Kwa sababu kuna… nataka nizumgumzie vile vile *issues* mbali mbali. Mambo haya ya Ujamaa vijijini, *efforts* zetu zilivyokwenda na pale ndipo nafikiria tulikosea, nadhani ni vizuri kueleza. Kwanza… kusaidia *appreciation* za *effort* za Mwalimu vile vile. Lakini vile vile na *limitations*.

**IS**: Hii itasaidia sana, *in fact* ukiweza kutengeneza *draft* ya kwanza, ambayo ni muhimu sana. Baadaye nyingine inaweza ikafuata *edited* nini. Lakini *just first draft*, itakuwa safi sana.

**KNM**: Naona ni vizuri. Sasa ndio nilikuwa nasema…

**IS**: Sisi tutakachofanya, kazi yetu itachukua muda, lakini kuna kijana ambaye ana*transcribe*. Akiwa ameshamaliza ku*transcribe* tutakupatia *copy* ya hiyo *transcription*.

**KNM**: Tena atapata taabu kweli maana yake haya mazungumzo...

**IS**: Lazima aya*transcribe*. Lakini *audio* tutakuwa nazo, tunaweza tuka*produce audio*. *If you are interested* katika *audio* tunaweza tukakuletea katika CD ya *audio*. Na baadaye kwenye kitabu chetu itategemea sasa muundo wenyewe wa vitabu. Kwa sababu tulichotaka kufanya ni kwamba tuwe na *profile* ya wale watu ambao walikuwa karibu nae kwa upande mmoja. Lakini pia wao wenyewe walikuwa na nafasi yao ya kipekee katika historia yetu kwa hiyo tutakuwa na *profile*. Katika hili itatusaidia sana.

**KNM**: Hiyo itakuwa nzuri, unajua sisi tunaacha kabisa kumuenzi Mwalimu sasa.

**IS**: Na kumuenzi mtu kama Mwalimu sio kuweka jina lake kwenye mitaa na majengo na nini *no*, fikra zake.

**KNM**: Na huyu alikuwa na fikra kubwa.

**IS**: Sasa hii sisi kwenye Kigoda tunajaribu hiyo.

**KNM**: Nilikuwa namwambia… kuna jamaa nilikuwa nazungumza naye. Nikamwambia Kigoda cha Mwalimu Nyerere chini ya Profesa Shivji ndicho kinajaribu kuweka fikra za Mwalimu mbele.

**IS**: Bahati mbaya… *I don't know*. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba *Mwalimu Nyerere Foundation* ndiyo ingekuwa ni hasa mahali pa ku… lakini mimi kwa kweli mimi imeni*disappoint* sana.

**KNM**: Hawawezi, rafiki zangu wale na hasa Butiku mwenyewe hawezi. Kwa sababu kwanza hawakujaribu kujipa *time* ya kutafakari juu ya *Foundation* ile hasa ni nini. walifikiria wanaweza kufanya fedha nyingi, kukusanya kwa jina la Mwalimu pesa nyingi na nini basi.

**IS**: Wanafanya nini na pesa hizi? Kama wangekuwa na muelekeo mzuri kwa kweli *by now*, tungekuwa na *a good* Mwalimu Nyerere *library by now*. Kuhifadhi *paper* zake halafu kuhifadhi *paper* za *liberation movement*, *library* yake mwenyewe. Ingekuwa ni *centre* ya *excellence*. Watafiti kutoka duniani mbali mbali wanakuja huku kufanya utafiti. Unajua ndivyo walivyofanya Nehru? Baada ya Nehru kufariki, nyumba yake mwenyewe ikawa *turned to a major library*. Na *it is really a major library*.

**KNM**: Aha! Na Nehru lilikuwa ni somi kubwa lile.

**IS**: Na hapa kwetu hatufikirii mambo kama haya.

**KNM:** *No*, watu wana mambo yao binafsi. Ubinafsi ndio umechukua *centre stage* kabisa kabisa kabisa kila mahala.

**IS:** Sijui kwa nini imetokea kwa sababu kitu ambacho kina *immortality* ni fikra sio mtu. Sasa ukitaka kumuenzi Mwalimu unaenzi fikra zake.

**KNM**: Eeh, *yeah*.

**IS**: Lakini *anyway* nakushukuru sana Mzee Ngombale.

**KNM**: Mimi nakushukuru zaidi.

**IS**: Nakushukuru sana sana. Kama ikitokea chochote tunaweza tukarudi kwako kupata ufafanuzi.